

# SUNA ZA MTUME (SAW) NA NYIRADI ZAKE ZA KILA SIKU

Utunzi wa
**Dkt. Abdallah bin Hamud Alfareeh.**

Utangulizi wa
**Prof. Khalid bin Ali Almushaiqih.**

# SUNA ZA MTUME (SAW) NA NYIRADI ZAKE ZA KILA SIKU

Anasema Allah Mtukufu katika Hadithul Qud'siyyu

"Na Wala Hatoacha Mja Wangu Kujikurubisha Kwangu Kwa Kutenda Mambo Ya Sunnah Mpaka Ninampenda"


**Utunzi wa**

**Dkt. Abdallah bin Hamud Alfareeh.**

**Utangulizi wa**

**Prof. Khalid bin Ali Almushaiqih.**

Haki za kuchapisha kitabu hiki ziko wazi kwa yeyote anayetaka kukichapisha kwa madhumuni yasiyokuwa ya kibiashara au kukitafsiri katika lugha nyingine baada ya kuwasiliana na mtunzi.


Kitabu hiki kimefasiriwa katika lugha zaidi ya kumi.

بسم الله الرحمن الرحيم

# Faharasa ya maudhui za kitabu


| Maudhui | Ukurasa |
|---|---|
| **Utangulizi.** | 13 |
| **Tangulizi** | 16 |
| Maana ya Suna. | 16 |
| Mifano ya namna Wema Waliotangulia walivyojali Suna. | 16 |
| Katika matunda ya kufuata Suna. | 18 |
| Nyasia mbili za Imamu Nawawi – Allah amrehemu– | 19 |


## Suna zilizowekewa wakati maalumu




| Maudhui | Ukurasa |
|---|---|
| **WAKATI WA KABLA YA ALFAJIRI.** | 22 |
| **Kigawanyo cha Kwanza:** Kuamka kwake kutoka usingizini. | |
| Katika Suna za Udhu. | |
| **Kigawanyo cha Pili:** Kusimama kwake kwa ajili ya kuswali usiku na Witiri. | |
| Ni upi wakati bora zaidi wa kuswali usiku? | |

| Maudhui | Ukurasa |
| --- | --- |
| Ubora katika wakati wa kuswali usiku uko katika daraja tatu. | |
| **Suala:** Je, kuleta Kunuti katika Witiri kumethibiti kwa kauli ya Mtume -SAW- au kwa vitendo vyake? | |
| Je, Kunuti inakuwa kabla Rukui au baada ya Rukui? | |
| **Suala:** Na Je, mtu ananyanyua mikono yake katika Kunuti ya Witiri? | |
| **Suala:** Kwa kitu gani mtu anaanza Kunuti yake katika Witiri? | |
| **Suala:** Je, mtu anapangusa uso kwa mikono yake baada ya Dua ya Kunuti? | |
| **PILI: Wakati wa Alfajiri.** | |
| Adhana, na ndani yake kuna Suna nyingi. | |
| Suna ya Alfajiri, na ndani yake kuna Suna nyingi. | |
| Suna za Ratibu zilizotiliwa mkazo. | |
| Suna za Alfajiri zinahusu mambo mengi. | |
| Suna katika Swala. | |
| Nyiradi za asubuhi. | |
| **TATU: WAKATI WA DHUHAA.** | |
| Wakati wake, na wakati wake bora zaidi. | |
| Fadhila zake. | |
| Idadi ya Rakaa zake. | |

| Maudhui | Ukurasa |
|---|---|
| **NNE: WAKATI WA ADHUHURI.** | |
| **Jambo la kwanza:** Kuswali Suna ya Adhuhuri ya Kabla na ya Baada. | |
| **Jambo la pili:** Ni Sunnah Kurefusha Rakaa Ya Kwanza Ya Swala Ya Adhuhr. | |
| **Jambo La Tatu:** Kailula (Kulala Mchana). | |
| **Jambo la nne:** Wakati wa joto jingi ni Suna kuchelewesha Swala ya Adhuhuri mpaka joto lipungue. | |
| **TANO: WAKATI WA ALASIRI.** | |
| Je, kuna swala yoyote ya Suna kabla ya Swala ya Alasiri? | |
| Nyiradi za jioni. | |
| Nyiradi za asubuhi na jioni zinanza wakati gani? | |
| **SITA: WAKATI WA MAGHARIBI.** | |
| **Jambo la kwanza:** Ni katika Suna kuzuia watoto kutoka majumbani mwanzo wa magharibi. | |
| **Jambo la pili:** Ni katika Suna kufunga milango mwanzo wa magharibi na kutaja jina la Allah Mtukufu. | |
| **Jambo la tatu:** Kuswali Rakaa mbili kabla ya Swala ya Maghribi. | |
| Ni Suna kuswali Rakaa mbili kati ya kila Adhana Na Ikama. | |
| **Jambo la nne:** Ni Makuruhu kulala kabla ya Isha. | |

| Maudhui | Ukurasa |
|---|---|
| **SABA: WAKATI WA ISHA.** | |
| **Jambo la kwanza:** Ni Makuruhu kuwa na mazungumzo na vikao baada ya Isha. | |
| **Jambo la pili:** Iliyo bora zaidi kwa Swala ya Isha ni kuchelesha kuiswali, kama hakutakuwa na uzito kwa maamuma. | |
| Kulala, na ndani yake kuna Suna nyingi: | |
| Kulala kuna nyiradi kutoka katika Kurani na Suna. | |
| Suna katika ndoto anazoziota mwenye kulala. | |
| Mwenye kuota ndoto nzuri, ni Suna kwake kufanya yafuatayo: | |
| Mwenye kuota ndoto asiyoipenda: Ni Suna kwake kufanya yafuatayo: | |
| Mwenye kuamka usiku ni Suna kwake kusoma uradi huu: | |

# Faharasa ya maudhui za kitabu

## SUNA AMBAZO HAZIKUWEKEWA WAKATI MAALUMU




| Maudhui | Ukurasa |
|---|---|
| SUNA ZA KULA. | |
| Suna za kusalimiana, kukutana va vikao | |
| SUNA KATIKA KUVAA NA KUJIPAMBA. | |
| Suna katika kupiga chafia na kwenda miayo. | |
| ◆ **Iliyo bora zaidi kwa mwenye kwenda miayo asinyanyue sauti yake anapopiga miayo.** | |
| Suna nyingine za kila siku. | |
| ◆ Ni Suna kuandika Wasia. | |
| ◆ Kusameheana na upole katika biashara. | |
| ◆ Kuswali Rakaa mbili baada ya kila Udhu. | |
| ◆ Kungojea Swala. | |
| ◆ Mswaki. | |
| ◆ Kujadidisha (kutawadha upya) udhu kwa kila swala. | |
| ◆ Dua | |
| ◆ Kusoma uradi uliopokewa wakati wa kuingia chooni na wakati wa kutoka. | |
| ◆ Kumtaja sana Allah aliyetukuka | |
| ◆ Namna gani walikuwa Maswahaba na Kurani? | |

| Maudhui | Ukurasa |
|---|---|
| ◆ Uradi ni uhai wa nyoyo. | |
| ◆ Allah amehimiza atajwe katika sehemu nyingi. | |
| ◆ Uradi ni aina mbili: Uliowekewa wakati maalumu na Usio-wekewa wakati maalumu. | |
| ◆ Kwa kumtaja Allah mja anakuwa miongoni mwa waliotan-gulia katika kheri. | |

بسم الله الرحمن الرحيم

الحمد لله وحده والصلاة والسلام على من لا نبي بعده، وبعد:

فقد قرأت في هذا المؤلف للشيخ عبد الله بن حمود الفريح (المنح العلية في بيان السنن اليومية) فقد ألفيته مؤلفاً مفيداً جمع على استقصاء السنن اليومية الفعلية والقولية في الليل والنهار، المنفردة والتابعة لغيرها مما ثبت بالدليل فجزاه الله خيراً، ونفع بمؤلفه آمين، وبالله التوفيق.

كتبه

د/ خالد بن علي المشيقح

٧/١١/١٤٣٤هـ

### Utangulizi wa Dkt. Khalid bin Ali Almushaiqih.

Sifa zote njema anazistahiki Allah peke yake. Swala na Salamu ziwe kwa yule ambaye hakuna Mtume mwingine baada yake.

Hakika, nimesoma utunzi wa Sheikh Abdallah bin Hamud Alfareeh **(Vipawa vya Mbinguni katika Kubainisha Suna za Kila Siku)**.

Hakika, nimeuona ni utunzi wenye faida, uliokwenda mbali zaidi katika kukusanya Suna za kila siku za matamshi na za vitendo kwa usiku na mchana, ukiwa wa kipekee na unaofuatia tunzi nyingine za Suna zilizothibiti kwa dalili.

Allah amlipe kheri, na ajaalie utunzi wake uwe wa kunufaisha. Aamin. Allah atie Taufiq.

Dkt. Khalid bin Ali Almushaiqih.

Mhadhiri Katika Chuo Kikuu Cha Qassim na
Mwalimu wa Darsa katika Misikiti Miwili
Mitukufu ya Makkah na Madina.


ادخلوها بسلام آمنين
KING FAHD GATE
TO ROOF

# Utangulizi

Sifa zote njema ni za Allah aliyesema kuwa:

**“Kwa yakini, mna kigezo kizuri kwa Mtume wa Allah kwa mwenye kutaraji (kukutana na) Allah na Siku ya Mwisho na akamdhukuru Allah kwa wingi”**. (Sura Al- ahzaab: 21). Allah ameweka ni sheria kufuata Suna ya Mtume wake, rehema na amani ziwe juu yake. Swala na amani ziwe juu ya mbora zaidi aliyeufahamisha Ummah utii timilifu na kufuata Suna.

Ndugu yangu msomaji, nakuwekea mikononi mwako Suna za Mtume (SAW) za kila siku tokea kuamka kwake hadi kulala kwake, zikiwa zimepangwa kulingana na wakati. Kisha nimezifuatishia kwa Suna nyingine za kila siku zisizofungaman na wakati maalumu.

Kwa neno Suna, nakusudia jambo lenye kupendekezwa na ambalo Sheria imeliamrisha lakini sio kwa kulazimisha, bali ni kwa njia ya kutaka ukamilifu na kuzidisha utii. Kitabu hiki ni muhtasari wa kitabu cha asili ambacho ni **(Vipawa vya Mbinguni katika Kubainisha Suna za Kila Siku)** baada ya kuwa nimeondoa masuala ya kitaaluma na faida zinazohusiana na Suna. Nimefanya muhtasari huu ubaki katika kutaja Suna pamoja na ushahidi wake tu, ikiwa ni kuitikia maoni ya baadhi ya ndugu wanaotaka ufupisho, kuwarahisishia wale ambao hawana wakati wa kutosha au juhudi za kukisoma kitabu cha asili na pia kuzisaidia baadhi ya taasisi za Kidaawa ziweze kukichapisha ili kukifikisha kwa idadi kubwa zaidi ya watu inayowezekana. Sababu iliyonifanya nifuatilie Suna za kila siku za Mtume, Swalla Allahu Alayhi Wasallama, ni kuuweka wazi muongozo wa Mtume (SAW) kama inavyotakikana; muongozo ambao umeharibiwa na Umagharibi. Ukiongezea hapo ni ile hali tunayoishuhudia

sasa ya kutokutekeleza Suna kwa kisingizio kuwa hapati adhabu mwenye kuiacha, jambo linalofanya watu wapitwe na kheri nyingi sana. Na nimekuwa makini katika kubainisha Suna sahihi na za kila siku tu, zikiambatana na ushahidi wake. Namuomba Allah (SWT) Atujaalie tuwe miongoni mwa wenye kufuata muongozo wa Mtume (SAW), wenye kufuata nyayo zake na tufufuliwe tukiwa katika kikundi chake.

Ameandika mhitaji wa msamaha wa Mola wake

Dkt. Abdullah bin Hamuud Alfareeh.

Email: forih@hotmail.com

# Tangulizi



## MAANA YA SUNA

Suna inamaanisha: Kilichopendekezwa.

Sunnah ist somit das, was die Šarīʿa zwar an Handlungen gebot, diese aber nicht als Pflicht auferlegte. Daraus folgt: Für die Umsetzung dieser empfohlenen Handlungen wird man belohnt und für deren Unterlassung nicht bestraft.

### Mifano ya Ari ya Salaf (Wema Waliotangulia) katika kutenda Suna:

1. Imamu Muslim katika kitabu chake cha "Sahiih" amepokea Hadithi ya Nuuman bin Salim akinukuu kwa Amri bin Ausi, Allah Awawie radhi, akisema kwamba, amenisimulia Anbasa bin Abisufiaa, kwa kuesema kuwa: Nimemsikia Ummuhabiba akisema: Nimemsikia Mtume (SAW) akisema: **"Mwenye kuswali rakaa kumi na mbili kwa usiku na mchana (yaani kwa**

**siku moja), atajengewa nyumba peponi kwa (sababu ya) rakaa hizo"**. Hadithi hii imepokelewa na Imamu Muslim, ikiwa na nambari (1727). Na amesema Ummuhabiba: **"Sikuziacha (rakaa hizo) tangu nilipozisikia kwa Mtume (SAW)"**. Na Anbasa amesema: "Sikuziacha (rakaa hizo) tangu nizisikie kwa Ummuhabiba."

Na Amri bin Aus amesema: **"Sikuziacha (rakaa hizo) tangu nizisikie kwa Anbasa"**.

Na Nuuman bin Salim amesema: **"Sikuziacha (rakaa hizo) tangu nizisikie kwa Amri bin Aus"**.

2 2/Hadithi ya Ali, Allah amuwie radhi, : "Kwamba Fatuma alilalamikia hali iliyokuwa ikimsibu katika mkono wake kutokana na jiwe la kusagia nafaka (ili apatiwe mfanyakazi). Na Mtume, SAW alikuwa amepata mateka. Fatuma alikwenda kwa Mtume lakini hakumkuta. Alikutana na Aisha na kumwambia (shida yake). Mtume –SAW- , alipokuja Aisha alimwabia kuhusiana na kuja kwa Fatma. Mtume –SAW- akaja kwetu, hali ya kuwa tulikuwa tumeshajilaza. Tukataka kuinuka, na Mtume –SAW- **akatukataza**, na akakaa kati yetu mpaka nikapata ubaridi wa miguu yake katika kifua change. Kisha Mtume akasema: **"Je, niwafundishe kilicho bora zaidi kuliko kile mlichokiomba? Mnapotaka kulala mtukuzeni Allah kwa kusema Allahu Akbar mara thalathini na nne, na mtakaseni kwa kusema Sub-haanallaah mara thalathini na tatu, na mhimidini kwa kusema Alhamdu Lillaah mara thalathini na tatu. Kufanya hivyo ni bora zaidi kwenu kuliko (kutafuta) mfanyakazi"**. Hadithi hii imepokewa na Bukhaari ikiwa na nambari (3705) na Muslim ikiwa na nambari (2727).

Na katika upokezi mwingine imenukuliwa kwamba, Ali, Allah amuwie radhi, amesema kuwa: "Sikuacha kufanya hayo tangu niyasikie kwa Mtume-SAW-. Aliulizwa: (Hukuacha) Hata katika usiku wa (vita vya) Siffin? Akasema: "Hata katika usiku wa Siffin". Hadithi hii imepokewa na Bukhari namba (5362) na Muslim kwa nambari (2727).

Ijulikanavyo ni kuwa usiku wa Siffin ni usiku uliokuwa n vita. Ali, Allah amuwie radhi, alikuwa kiongozi katika vita hivyo. Pamoja na hali hiyo hakuacha Suna hii.

3 Ibniumar, Allah amuwie radhi, alikuwa anaswalia maiti kisha anaondoka na hamsindikizi kwa kudhani kuwa hiyo ndio Suna kamilifu. Hakuwa akijua fadhila na wema wa kumsindikiza maiti mpaka kuzikwa. Ilipomfikia

Hadithi ya Abuhuraira, Allah amuwie radhi, alijuta kwa kuikosa Suna. Tafakari; alifanya nini?!

Ibniumar, Allah amuwie radhi, alitupa chini ya ardhi kwa hasira changarawe iliyokuwa mkononi mwake kisha akasema: **“Kwa hakika, tumezikosa kwa uzembe Karati nyingi”**. Imepokewa na Bukhari ikiwa na nambari (1324) ,na Muslim ikiwa na nambari (945)

Imamu Annawawi, Allah amrehemu, amesema kuwa: “Ndani ya tukio hilo (la Ibniumar) kunaonekana hali waliyokuwa nayo Swahaba ya kuwa na hamu kubwa ya kufanya ibada pale taarifa inapowafikia na pia kuzijutia ibada zinapowapita hata kama walikuwa hawajui ukubwa wa nafasi yake. Angalia: Alminhaaj (7/15)

## Miongoni mwa faida za kufuata Suna:

Ndugu yangu mpendwa, kufuata Suna kuna faida nyingi. Miongoni mwa faida hizo ni:

1. Kufikia daraja ya kupendwa. Kwa kujiweka karibu na Allah kwa kufanya Suna mja anapata kupendwa na Allah – SWT –.

Ibniqayim, Allah amrehemu, amesema kuwa: “Na Allah hatakupenda isipokuwa tu pale unapokuwa umemfuata kipenzi chake (Mtume) kwa dhahiri na kwa undani, umesadikisha habari zake, umetii amri zake, umeukubali wito wake, umemtanguliza yeye kwa hiari, umeacha sheria za wengine kwa (kutumia) sheria zake, umacha kuwapenda viumbe wengine kwa kumpenda yeye na ukawa umeacha kuwatii wengine kwa kutmii yeye. Kama haitakuwa hivyo, kamwe usisumbuke. Rudi utakako ukatafute nuru, kwani huna kitu chochote”. Angalia kitabu cha Madarijussaalikiin (3/37).

2. Mja kupata daraja ya kuwa pamoja na Allah (SWT), kwa sababu hiyo Allah humuwezesha mja kufanya mambo ya kheri. Hakitoki kitu katika viungo vyake ila kile kinachomridhisha Allah (SWT), kwa sababu mja anapopata kupendwa na Allah hupata kuwa pamoja naye.

3. Kujibiwa dua kunakoambatana na kupata kupendwa. Mwenye kujiweka karibu na Allah kwa kufanya Suna atapata kupendwa, na mwenye kupata kupendwa atapata kukubaliwa dua yake.

### Ushahidi wa faida hizi tatu ni:

Hadithi ya Abuhuraira, Allah amuwie radhi, aliyesema kwamba, Mtume wa Allah amesema kuwa: “Hakika Allah Amesema: **Atakayemfanyia uadui walii wangu (kipenzi change), kwa yakini kabisa nimemtangazia vita, Na mja wangu kwa kitu chochote ninachokipenda zaidi ya vile nilivyomfaradhishia. Na mja wangu ataendelea kujiweka karibu nami kwa kufanya mambo ya Suna mpaka ninakuwa nampenda. Nikimpenda, ninakuwa masikio yake ambayo anasikia kwayo, na macho yake ambayo anaona kwayo, na mkono wake ambao anashika kwao, na mguu wake anaotembelea, Na akiniomba ninampa, na akiniomba kinga ninamlinda. Na sijapatapo kusita juu ya kitu ninachotaka kukifanya kama kusita kwangu yuu ya nafsi ya muumini; hapendi kufa, nami sipendi kumuudhi”**. Hadithi hii imepokewa na Bukhari ikiwa na nambari (6502).

4. Kuziba upungufu unaopatikana katika kutekeleza Faradhi. Suna huziba yale mapungufu yanayotokea katika (kutenda) Faradhi.

**Ushahidi wa hili ni:**

Hadithi ya Abuhuraira, Allah amuwie radhi, aliyesema kuwa, nilimsikia Mtume - SAW- akisema kwamba: **“Hakika, kitu cha kwanza mja atakachohesabiwa kwacho katika amali zake siku ya Kiyama ni Swala. Swala ikiwa itakuwa iko sawa atakuwa amefaulu na kuokoka. Na swala ikiwa imeharibika atakuwa amepata hasara. Na kama kimepungua kitu chochote katika faradhi zake, Allah atasema: Angalieni: Je, mja wangu ana chochote katika Suna? Kwa Suna hiyo kitakamilishwa kile kilichopungua katika faradhi. Na amali zake zote zilizosalia zitakuwa mfano wa hivyo”**. Hadithi hii imepokewa na Ahmad ikiwa na nambari: (9494) na Abudaudi ikiwa na nambari (864) na Tirmidhi ikiwa na nambari (413). Ameihakiki Albani (Swahih Aljami 1/405)





# SUNA ZA NYAKATI MAALUMU

Kwa kusema Suna za nyakati maalumu tunakusudia zile Suna ambazo zimefungamana na nyakati maalumu usiku na mchana. Ni Suna zinazopendekezwa kufanya katika nyakati maalumu. Nimezigawanya katika nyakati saba. Kabla ya Alfajiri, wakati wa Alfajiri, wakati wa Dhuhaa, wakati wa Adhuhuri, wakati wa Alasiri, wakati wa Magharibi na wakati wa Isha.

## KWANZA: WAKATI WA KABLA YA ALFAJIRI.




Huu ni wakati wa kwanza kwa kuzingatia kuamka kutoka usingizini. Katika wakati huu yaweza kugawanywa Suna katika mafungu mawili:

### FUNGU LA KWANZA:

Kuamka kutoka usingizini na matendo yanayofuatia hapo na ambayo Mtume SAW alikuwa akifanya:

### 1 Kusafisha mdomo wake kwa kupiga mswaki.



Imenukuliwa kwa Hudhaifa –Allah Amridhie- akisema kuwa: **"Mtume SAW alipokuwa akiamka usiku alikuwa anasugua mdomo wake kwa kutumia mswaki"**. Hadithi hii imepokewa na Bukhari ikiwa na nambari (245) na Muslim ikiwa na nambari (255). Na katika mapokezi mengine ya Muslim imenukuliwa kuwa: **"Mtume SAW alikuwa anapoamka kufanya Tahajudi**

**(kusali sala za usiku) anasafisha mdomo wake kwa kutumia mswaki"**. Hadithi hii ameipokea Muslim ikiwa na nambari (255). Kusafisha: ni kusugua meno kwa upana kwa kutumia mswaki.

### 2 Anasoma Uradi ulionukuliwa wakati wa kuamuka kutoka usingizini.

Huu ni ule Uradi uliokuja katika Sahih Bukhari kupitia Hadithi ya Hudhaifa, Allah Amridhie, aliyenukuliwa kusema kuwa: "Mtume SAW alikuwa anapotaka kulala anasema: "Kwa jina lako Ewe Mola Wangu ninakufa na ninakuwa hai". Na anapoamka kutoka usingizini anasema: "Sifa njema ni za Allah Ambaye ametupa uhai baada ya kutufisha na kwake yeye tu ndiko tutakapokusanywa". Hadithi hii imepokewa na Bukhari ikiwa na nambari (6324) na Muslim kutoka Hadithi ya Albaraa, Allah amridhie, ambayo imepokewa na Muslim ikiwa na nambari (2711).

### 3 Anapangusa usingizi usoni mwake.

### 4 Na anaangalia mbinguni.

### 5 Na anasoma aya kumi za mwisho katika Sura Aal- imran.

Na Suna hizi tatu zimekuja katika Hadithi ya Ibniabass, Allah amridhie yeye na baba yake, Hadithi ambayo imepokewa na Bukhari na Muslim kwamba **"Yeye (Ibniabbas) alilala siku moja kwa Maimuna mke wa Mtume -SAW- naye ni mama yake mkubwa/mdogo. Nikalala kwa kujiegemeza kwenye mto kwa upana wake, na Mtume –SAW- akalala yeye na mkewe kwa kujiegemeza kwenye mto kwa urefu wake. Mtume akalala mpaka katikati ya usiku, au kabla yake kidogo au baada yake kidogo, Mtume aliamka akaketi akifuta usingizi usoni mwake kwa kutumia mkono wake. Kisha akasoma aya kumi za mwisho katika Sura Aal-imran, Kisha akainuka akachukua kiriba cha maji kilichokuwa kimetundikwa akatawadha vizuri kwa maji yaliyokuwemo humo. Kisha akaanza kuswali"**. Hadthi hii imepokewa na Bukhari ikiwa na nambari (183) na Muslim ikiwa na nambari (763).

Na katika mapokezi ya Imamu Muslim yakiwa na nambari (256) imenukuliwa kwamba: **"Na Mtume wa Allah –SAW- akasimama wakati wa mwisho wa usiku, kisha akatoka akaangalia mbinguni, kisha akasoma aya hii iliopo mwisho wa Sura Aal-imran.**

{إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالأَرْضِ وَاخْتِلاَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لآيَاتٍ لِّأُوْلِي الألْبَابِ ...} [آل عمران190 ]

**Kwa hakika, katika umbo la mbingu na ardhi na kupishana kwa usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili**.... (Sura Aal-imran: 190).

- akiwa anapangusa usingizi usoni mwake kwa kutumia mkono wake". Anapangusa macho yake kwa kutumia mkono wake ili apanguse athari ya usingizi.

Na katika mapokezi ya Imamu Muslim kuna ubainifu wa anachokisoma mwenye kutaka kufuata Suna hii. Ataanza kusoma kwanzia kauli ya Allah aliyetukuka: **"Kwa hakika katika umbo la mbingu na ardhi na kupishana kwa usiku na mchana..."** mpaka mwisho wa Sura Aal-imran.

### 6 ANAOSHA MIKONO YAKE MARA TATU.

Ni kutokana na Hadithi ya Abuhuraira –Allah amridhie- aliyenukuu kwamba, Mtume SAW amesema: **"Mmoja wenu anapoamka kutoka katika usingizi wake asiingize mkono wake katika chombo mpaka auoshe mara tatu, kwa sababu hajui mahali mkono wake ulipolala"**. Hadithi hii imepokewa na Bukhari ikiwa na namba (162) na Muslim ikiwa na namba (278).

### 7 ASUKUTUE MDOMO NA PUA KWA KUTUMIA MAJI MARA TATU.

Ni kutokana na Hadithi ya Abuhuraira –Allah amridhie- akinukuu kwamba, Mtume SAW amesema: "Mmoja wenu anapoinuka kutoka usingizini mwake asukutue pua mara tatu, kwa sababu shetani analala ndani ya tundu za pua yake". Hadithi hii imepokewa na Bukhari ikiwa na nambari (3295).

### 8 KISHA ANATAWADHA.


Hii ni kutokana na Hadithi ya Ibniabass –Allah amridhie yeye na baba yake- iliyo tangulia pale Mtume SAW alipotaka kuswali, alisimama akendea kuchukua kiriba kilichokuwa kimetundikwa na akatawadha kwa maji yaliyokuwemo humo.

## MIONGONI MWA SUNA ZA UDHU.



Na hapa katika Udhu, tutasimama kubainisha Suna kadhaa za Udhu kwa kifupi na kwa idadi fulani, na sio kwa kutoa ufafanuzi na kuzitaja zote, kwa sababu zinajulikana. Sisi tunazikumbushia tu kwa madhumuni ya kutimiza Suna.

### 1 KUPIGA MSWAKI.



Hilo ni kabla kuanza kutawadha, au kabla ya kusukutua. Hapa ndipo sehemu ya pili ambapo ni Suna kupiga mswaki, na sehemu ya kwanza imeshatangulia kutajwa. Ni Suna kwa anayetaka kutawadha apige mswaki, kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira – Allah amridhie- aliyenukuu kwamba, Mtume SAW amesema kuwa: **"Lau nisingeona kuwa itakuwa mashaka (uzito) kwa Umma wangu ningewaamrisha kupiga mswaki wakati wa kila Udhu"**.
Hadithi hii imepokewa na Ahmad ikiwa na nambari (9928.) Pia imepokewa na Ibnikhuzaima na kutaja kuwa ni sahihi (1/73/140). Pia ameipokea Hakim (245/1) na Bukhari kwa Taaliq (kutotajwa kwa baadhi ya wapokezi) kwa lugha ya Jazmi (lugha ya kusisitiza usahihi wa Hadithi) katika mlango wa: "(Kutumia) Mswaki wa mti mbichi na mkavu kwa mwenye kufunga".

Na kutokana na Hadith ya Aisha –Allah amridhie- aliyesema kuwa: **“Tulikuwa tunamtayarishia (Mtume) mswaki wake na maji yake ya kujitwaharishia. Allah anampa ujumbe anaotaka kumpa usiku. Anapiga mswaki na anatawadha na anaswali”**. Hadithi hii imepokewa na Muslim ikiwa na nambari (746).

## 2 KUSEMA BISMILLAHI.

Kutokana na Hadithi ya Abuhuraira- Allah amridhie- iliyohusishwa na Mtume amesema kuwa: **“Hana Udhu yule ambaye hajataja jina la Allah”**. Hadithi hii imepokewa na Ahmad ikiwa na nambari (11371), Abudaud ikiwa na nambari (101) na Ibnimaja ikiwa na nambari (397).

## 3 KUOSHA VIGANJA VYA MIKONO MARA TATU.



Kutokana na Hadithi ya Uthman- Allah Amridhie- katika kuelezea namna ya Udhu wa Mtume SAW. Katika maelezo hayo kuna **“(Mtume) Aliagiza aletewe chombo cha kutawadhia na akatawadha. Aliosha viganja vyake viwili mara tatu…”**. Kisha (Uthman) akasema: **“Nilimuona Mtume –SAW- akitawadha kama hivi nilivyotawadha”**. Hadithi hii ameipokea Bukhari ikiwa na nambari (164) na Muslim kwa nambari (226).

## 4 KUANZA UPANDE WA KULIA KATIKA KUOSHA MIKONO NA MIGUU.



Kutokana na Hadithi ya Aisha –Allah amridhie- aliyenukuliwa kusema kuwa: **“Mtume- SAW- alikuwa anapenda sana kutumia upande wa kulia katika kuvaa viatu vyake, kuchana nywele zake na kujitwaharisha kwake na katika mambo yake yote”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1680) na Muslim kwa nambari (268).

## 5 KUANZA KWA KUSUKUTUA NA KUVUTA MAJI PUANI.

Kwa Hadithi ya Uthman –Allah amridhie- katika kuelezea namna ya Udhu wa Mtume SAW kwamba **“Alisukutua na akavuta maji puani, kisha akaosha**

**uso wake mara tatu”**. Hadithi hii imepokewa na Bukhari kwa nambari (199) na Muslim kwa nambari (226). Ikiwa mtu atachelewesha kusukutua na kuvuta maji puani (na kuyafanya hayo) baada ya kuosha uso itafaa.

### 6 KUZIDISHA KATIKA KUSUKUTUA NA KUVUTA MAJI PUANI KWA YULE AMBAYE HAJAFUNGA SAUMU.



Kutokana na Hadithi ya Lukait bin Swabra – Allah amridhie-aliyesimulia kwamba Mtume-SAW-alimwambia kuwa: **‘‘Tawadha vizuri na pitisha vidole kati ya vidole na zidisha katika kuvuta maji kwenye pua isipokuwa unapokuwa umefunga’’**. Hadithi hii imepokewa na Ahmad kwa nambari (17846) na Abudaud kwa nambari (142). Amesema Ibnihajar kuwa: “Hii ni Hadithi sahihi”. Al-iswaba (9/15). Kuzidisha katika kusukutua kumepatikana kutoka katika kauli ya Mtume kwamba **“Tawadha vizuri”**.

### 7 KUSUKUTUA NA KUVUTA MAJI PUANI KWA KUTUMIA KIGANJA KIMOJA.



Kutokana na Hadithi ya Abdallah bin Zaid – Allah amridhie- katika kuelezea namna Mtume alivyokuwa akitawadha na kusema kuwa: **“……. (Mtume) Aliingiza mkono wake kisha akautoa. Alisukutua na kuvuta maji puani kwa kutumia kiganja kimoja. Alifanya hivyo mara tatu”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (192) na Muslim kwa nambari (235).

### 8 KATIKA KUPAKA MAJI KICHWA INAPENDEKEZWA KUFUATA NAMNA AMBAYO NI SUNA.



Namna hiyo ni mtu kuanza katika kupaka maji kichwa chake kwa kuweka mikono yake mbele ya kichwa chake, kisha aipeleke mpaka kichogoni mwake. Kisha airejeshe pale mahali alipoanzia. Mwanamke pia anafanya Suna hii kwa njia hiyo hiyo. Nywele zilizozidi na kuwa nje ya shingo ya mwanamke hazipakwi maji.

**USHAHIDI WA HILI NI:**

Hadithi ya Abdallah bin Zaid - Allah amridhie – katika kuelezea namna Mtume SAW alivyokuwa akitawadha. Katika maelezo hayo kuna maneno haya: **"(Mtume) Alianzia sehemu ya mbele ya kichwa chake kisha akaipeleka (mikono yake) mpaka kichogoni mwake. Kisha akairudisha mpaka pahali alipoanzia"**. Imepokewa na Bukhaari kwa nambari (185) na Muslim kwa nambari (235).

## 9 KUOSHA VIUNGO MARA TATU.

Mara ya kwanza ni wajibu. Ama mara ya pili na ya tatu ni Suna. Haitakiwi kuzidisha zaidi ya mara tatu.


**USHAHIDI WA HILI NI:**

Hadithi ya Ibniabbas –Allah amridhie yeye na baba yake - iliyothibitishwa na Bukhari -Allah amrehemu- **"Kwamba Mtume –SAW-alitawadha mara moja mara moja''**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (157). Na imethibiti kwa Bukhari pia ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abdallah bin Zaid –Allah amridhie- **"Kwamba Mtume- SAW-alitawadha mara mbili mara mbili"**. Imepokewa na Bukhaari kwa nambari (158). Pia imethibiti katika Sahih Bukharin a Sahih Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Uthmaan –Allah amridhie- **"Kwamba Mtume –SAW- alitawadha mara tatu tatu"**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (159). Kwa hivyo, ni bora kubadilisha saa nyingine. Mara atawadhe mara moja moja, wakati mwingine mara mbili mbili, wakati mwingine mara tatu tatu, na mara nyingine apishanishe idadi. Kwa mfano: aoshe uso mara tatu, mikono mara mbili mbili, na miguu mara moja moja, kama ilivyo katika Sahih Bukhari na Sahih Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abdallah bin Zaid- Allah amridhie- katika mapokezi mengine. Angalia: Zaadul Maad (1/192). Lakini, jambo la aghlabu zaidi ni mtu afanye kwa ukamilifu mara tatu tatu, kwa sababu huo ndio muongozo wa Mtume –SAW-.

## 10 DUA ILIYOTHIBITI BAADA YA UDHU.

Imenukuliwa kwa Umar –Allah amridhie- akisema kuwa, amesema Mtume wa Allah–SAW- kwamba: **"Hakuna yeyote kati yenu anayetawadha akautimiza vilivyo Udhuu wake, kisha akasema: "Nashuhudia ya kwamba hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu, na kwamba Muhammad ni Mja Wa Allah na Mtume Wake, (Ash-hadu Allaa ilaaha illa-llaah, Wa-ash-hadu Anna Muhammadan Abdullaahi Warasuuluhu) isipokuwa atafunguliwa milango minane ya pepo aingie kupitia mlango wowote autakao"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (234).

Au Dua iliyokuja katika Hadithi ya Abusaid–Allah amridhie- ikihusishwa na Mtume kwamba **“Mwenye kutawadha kisha akamaliza Udhu wake na akasema: Sub-hanakallahumma Wabihamdik, Ash-hadu Allaa Ilaaha Illaa Anta, Astaghfiruka Wa-atuubu Ilayika, (Utukufu na sifa njema zote ni zako. Nashuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa kwa haki ila wewe tu. Naomba msamaha wako na natubu kwako), Allah hupiga muhuri na kuwekwa lakiri,** kisha ikanyanyuliwa na kuwekwa chini ya Arshi na haitavunjwa lakiri hiyo mpaka siku ya Kiyama”. Imepokeleawa na Nasai katika Matendo ya Usiku na Mchana. (Ukurasa 147). Pia ameipokea Hakim (1/752) na Ibnihajar – Allah amrehemu-amesema kuwa orodha ya wapokezi wake ni sahihi. Angalia Nataa-ijul-afkaar, (1/246). Ameendelea kubainisha kuwa, kama sio sahihi kuihusisha kwa Mtume, basi imehusishwa kwa Swahaba. Hilo halina tatizo, kwa sababu jambo hilo linachukua hukumu ya kuhusishwa kwa Mtume, kwakuwa ni miongoni mwa mambo ambayo rai ya mtu haina nafasi katika mambo hayo. .



**<u>Sehemu Ya Pili:</u> Kisimamo cha usiku na Witiri. Humo kuna ibada nyingi ambazo ni katika uongozo wa Mtume –SAW-:**

1 **Ni katika Suna mtu kuswali Swala ya usiku katika wakati wake ulio bora zaidi.**

- Ikiulizwa: Ni upi wakati bora zaidi wa swala ya usiku?

Jawabu ni hili: Inajulikana kuwa wakati wa Swala ya Witiri unaanza baada ya Swala ya Isha mpaka kuchomoza kwa Alfajiri. Kwa hivyo, mahali pa swala ya Witiri ni muda uliopo baina ya Swala ya Isha na ya Alfajiri.

**USHAHIDI WA HILI NI:**

Hadithi ya Aisha- Allah amridhie- aliyenukuliwa kusema kuwa: “Mtume wa Allah- SAW-alikuwa akiswali rakaa kumi na moja katika muda uliopo baina ya kumaliza Swala ya Isha mpaka Alfajiri, akitoa Salamu kati ya kila raka mbili. Na anafanya Witiri kwa (kuswali) rakaa moja.” Imepokewa na Bukhaari kwa nambari (2031) na Muslim kwa nambari (7736).

### AMA WAKATI BORA ZAIDI WA SWALA YA USIKU NI: THELUTHI YA USIKU BAADA YA NUSU YAKE.

Kinachokusudiwa: Ni kwamba mwanadamu anagawanya usiku nusu nusu. Anasimama na kuswali katika theluthi ya nusu ya pili ya usiku na mwisho wa usiku analala. Yaani anasimama na kuswali katika sudusi (1/6) ya nne na ya tano kisha analala katika sudusi ya sita.

**Ushahidi wa hili ni:** Hadithi ya Abdallah bin Amri – Allah amridhie yeye na baba yake- aliyenukuliwa kusema kwamba, Mtume wa Allah– SAW-amesema kuwa: "Hakika Swaumu inayopendwa sana na Allah ni Swaumu ya (Mtume) Daudi –AS- na Swala inayopendwa sana na Allah ni Swala ya (Mtume) Daudi –AS-. Alikuwa akilala nusu ya usiku, na anainuka (na kuswali) theluthi yake, na analala sudusi yake. Na alikuwa akifunga siku moja na anafungua siku (ya pili). Imepokelewa na Bukhari namba (3420).

### KAMA MTU AKITAKA KUTEKELEZA SUNA HII, ANAUHESABU VIPI USIKU WAKE?

Anahesabu wakati kutoka kuzama kwa jua mpaka kuchomoza kwa alfajiri. Kisha anaugawanya usiku huo vipande sita. Vipande vitatu vya kwanza ndio nusu ya kwanza ya usiku. Anasimama baada yake. Hii ikiwa na maana kwamba anasimama katika sudusi ya nne na ya tano, kwa sababu hii inazingatiwa kuwa ni theluthi. Kisha analala katika sudusi ya mwisho ambayo ndio sudusi ya sita. Kwa sababu hii Aisha –Allah- amesema kuwa: **"Haukumfikia Mtume- SAW- wakati wa Sahar (Usiku wa Manani) akiwa kwangu isipokuwa alikuwa amelala."** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1133) na Muslim kwa nambari (742).

Na kwa njia hii, Mwislamu anakuwa katika wakati bora sana wa kuswali usiku, kama ilivyokuja katika Hadithi iliyotangulia kutajwa ya Abdallah bin Amri- Allah amridhie yeye na baba yake.

### UFUPI WA MANENO NI KWAMBA: UBORA KATIKA WAKATI WA KISIMAMO CHA USIKU UKO KATIKA DARAJA TATU:

**Daraja ya kwanza:** Ni mtu alale nusu ya kwanza ya usiku, kisha ainuke theluthi yake, kisha alale sudusi yake, kama ilivyotangulia kuelezwa.

**Ushahidi wa hili ni:** Hadithi ya Abdalla bin Amri bin Al-aas –Allah amridhie yeye na baba yake- ambayo imetangulia kutajwa hivi punde.

**Daraja ya pili:** Ni mtu aamke katika theluthi ya mwisho ya usiku.

**Ushahidi wa haya ni:**

Hadithi ya Abuhuraira –Allah amridhie- kwamba Mtume –SAW- amesema kuwa: **“Mola wetu aliyetukuka na kutakasika anashuka kila usiku hadi mbingu ya chini kabisa, pale inapobaki theluthi ya mwisho ya usiku. Anasema: Ni nani anayeniita nimwitikie? Na ni nani anayeniomba nimpe? Na ni nani anayeniomba msamaha nimsamehe”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1145) na Muslim kwa nambari (758). Na pia kuna Hadithi ya Jabir- Allah amridhie- na itakuja.

Mtu akiogopa kuwa atashindwa kuamka mwishoni mwa usiku, basi aswali mwanzo wake au katika wakati wowote ambao utakuwa mwepesi kwake. Na hii ndio daraja ya tatu.

**Daraja ya Tatu:** Mtu anaswali wakati wa mwanzo wa usiku, au katika sehemu ya usiku ambayo ni nyepesi kwake.

**Ushahidi wa hilo ni:**

Hadithi ya Jabir –Allah amridhie- aliyesema kuwa, amesema Mtume wa Allah - SAW- kwamba: **“Atakayechelea kutoamka mwisho wa usiku, basi aswali Witiri mwanzo wake. Na atakayetaraji kuamka mwisho wake basi aswali Witiri mwisho wa usiku, kwa sababu Swala ya mwisho wa usiku ni yenye kushuhudiwa, na hiyo ni bora zaidi”**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (755).

Na vilevile unachukuliwa juu ya hili Wasia wa Mtume -SAW- kwa 1)Abudhari (imepokewa na Nasai katika Sunan Kub’ra (2712) na Albani ameisahihisha (Aswahiihatu (2166). na Wasika wa Mtume kwa 2)Abudrdaa (ameipokea Ahmad kwa kwa nambari (27481), na Abudaudi kwa kwa nambari (1433) na Albani ameisahihisha (Swahiih Abudaud nambari 5/177) na Wasia wa Mtume kwa 3)Abuhuraira –Allah amridhie- ameipokea Muslim kwa nambari (737). Kila mmoja (katika Swahaba hao) amenukuliwa akisema kuwa: **“Ameniusia Kipenzi changu (Mtume) mambo matatu”**, na akataja katika hayo: **“Na (Aliniusia) niswali Witiri kabla sijalala”**.

### 2 SUNA NI KUSWALI RAKAA KUMI NA MOJA.

Na huu ndio ukamilifu zaidi, kwa mujibu wa Hadithi ya Bi Aisha –Allah amridhie- aliyenukuliwa kusema kuwa: **“Mtume- SAW-hakuwa akiswali zaidi ya Rakaa kumi na moja wakati wa Ramadhani wala wakati mwingine.** Ameipokea Bukhari kwa nambari (1147) na Muslim kwa nambari (738).


Imepokewa kwamba Mtume –SAW- aliswali rakaa kumi na tatu. Imepokewa na Imamu Muslim katika Swahihi yake kutoka katika Hadithi ya Aisha-Allah amridhie-.

Na hii ni katika mlango wa namna tafauti za kutekeleza Swala ya Witiri. Iliyokuwa Aghlabu katika Witiri za Mtume –SAW- ni kwamba alikuwa akiswali Witiri rakaa kumi na moja. Na mara nyingine alikuwa akiswali rakaa kumi na tatu. Na kwa namna hii tunapata muwafaka wa kuziweka pamoja Hadithi zilizopokewa (kuhusu suala hili).

### 3 Ni katika Suna kuanza Swala ya usiku kwa Rakaa mbili nyepesi.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Aisha –Allah amridhie- aliyesema kuwa: **“Mtume wa Allah –SAW- anaposimama usiku ili aswali alikuwa anaanza swala yake kwa rakaa mbili nyepesi”.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (767).

### 4 Ni katika Suna mtu kusoma dua za kuanzia swala zilizothibiti katika Swala ya usiku. Miongoni mwa dua hizo ni hizi:



1. Hadithi ya Aisha –Allah amridhie- iliyokuja katika Swahihi Muslim akinukuliwa kusema kuwa: **“Mtume- SAW- anaposwali usiku anafungua swala yake kwa kusoma: Allaahumma Rabba Jibraa-iil wa Miikaa-iil wa Israafiil. Faatwiras-samaawaati wal-ardhwi. Aalimal ghaybi wash-shahaadah. Anta Tahkmu bayna ibaadika fiimaa kaanuu fiihi yakhtalifuun. Ihdinii limakhtulifa fiihi minalhaqqi Bi-idhnika. Innaka Tahdii Mantashaa-u ilaa Swiraatwim-mustaqiim. (Ee Allah, Mola wa Jibrili na Mikaili na Israfili, Muumba wa mbingu na ardhi, Mjuzi wa ghaibu (yasiyo onekana kwa macho)**

**na dhahiri, Wewe Utahukumu baina ya waja wako katika ambayo walikuwa wakihitilafiana. Niongoze mimi kwenye haki katika yale ambayo (watu) wamehitilafiana kwa idhini yako. Hakika, wewe unamuongoza umtakae kwenye njia ilio nyooka)**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (770).

2. Hadithi ya Ibniabbas –Allah amridhie yeye na baba yake- iliyokuja katika Swahih Bukhari na Swahih Muslim) aliyenukuliwa kusema kuwa: "Mtume- SAW- anapofanya Tahajudi usiku alikuwa anasema: "Allaahumma Lakalhamdu. Anta Nuurussamaawaati Wal-ardhi. Walakalamdu. Anta Qayyimussamaawaati Wal-ardhi. Walakalhamdu. Anta Rabbussamaawaati Wal-ardhi Waman Fiihinna. Antalhaqqu. Waqaulukalhaqqu. Waliqaa-ukalhaqqu. Waljannatu Haqqun. Wannaaru Haqqun. Wannabiyyuuna Haqqun. Wassaa'tu Haqqun. Allahumma Laka Aslamtu. Wabika Aamantu. Wa-alaika Tawakkaltu. Wa-ilaika Anabtu. Wabika Khaaswamtu. Wa-ilaika Haakamtu. Faghfir Lii Maaqaddamtu, Wamaa Akh-khartu, Wamaa Asrartu, Wamaa A'alantu. Anta Ilaahii. Laa Ilaaha Illaa Anta". **(Ewe Allah, ni zako wewe tu sifa njema. Wewe ndiye nuru ya mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake. Na ni zako wewe tu sifa njema. Wewe ndiye Mwenye kuzisimamia mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake. Na ni zako wewe tu sifa njema. Wewe ni Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake. Na sifa njema ni zako wewe tu. Wewe ni kweli, na ahadi yako ni ya kweli, na neno lako ni la kweli, na kukutana nawe ni kweli, na Pepo ni kweli, na Moto ni kweli, na Mitume ni kweli na Kiyama ni kweli. Ewe Mola wangu, kwako tu nimejisalimisha, na wewe tu nimekuamini, na wewe tu nimekutegemea, na kwa sababu yako tu nimegombana, na sheria zako tu nimezifuata. Nisamehe nilyokwishayafanya na nitakayoyafanya na niliyoyafanya kwa siri na niliyoyafanya dhahiri. Wewe ndiye Mola wangu. Hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa wewe tu).** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (7499) na Muslim kwa nambari (768).

**5. Ni katika Suna kurefusha kisimamo chake, rukuu yake na sujudi yake. Nguzo zote za vitendo vya Swala viwe vinakaribiana kuwa sawa.**

**6. Alete Suna zilizopokewa katika kisomo chake. Miongoni mwa Suna hizo ni hizi:**

1. Asome taratibu. Makusudio yake ni kuwa, mtu asiwe mwenye kwenda mbio katika kisomo.

2 Akate kisomo chake aya baada ya aya. Maksudio ni kwamba: Mtu asiwe mwenye kuunganisha aya mbili au tatu bila kusimama. Bali awe anasimama katika kila aya.

3 Akipita katika aya ya Tasbihi analeta Tasbihi (Sub-haanallah), na akipita katika aya ya maombi anaomba, na akipita katika aya ya kuomba kinga anaomba kinga (kwa Allah) amlinde.

Na ushahidi wa hayo yaliyotangulia ni:

Hadithi ya Hudhaifa- Allah amridhie- aliyenukuliwa kuesema kuwa: “Niliswali na Mtume –SAW-usiku mmoja. Alianza kusoma Sura Albaqara nikasema: Atarukuu akifika aya ya mia moja. Kisha akapita, nikasema: Ataswali kwayo katika rakaa moja, na akapita. Nikasema: Atarukuu kwayo. Kisha akaanza (kusoma) Sura Annisaa na akaisoma (yote). Kisha akaanza (kusoma) Sura Aal-imrani na akaisoma (yote) kwa utulivu. Akipita kwenye aya ambayo ndani yake ina kusabihi anasabihi, na akipita kwenye aya ya kuomba anaomba, na akipita kwenye aya ya kuomba kinga anaomba kinga (kwa Allah). Kisha akarukuu akawa anasema: **“Sub-haana Rabbiyal-adhwiim”.** Kurukuu kwake kulikuwa kama kusimama kwake. Kasha akasema: **“Samia-llaahu Liman Hamidah”**, **(Allah amemsikia mwenye kumhimidi).** Kisha akasimama sana, kukaribia vile alivyorukuu. Kisha akasujudu na kusema: **“Subhaana Rabiiyal A’alaa” (Ametakasika Mola wangu Aliye Juu)**. Kusujudu kwake kulikuwa kunakaribia kusimama kwake. Ameipokea Muslim kwa nambari (772).

Pia hayo ni kwa mujibu wa Hadithi ya Ummusalama –Allah amridhie- aliyoipokea Imam Ahmad –Allah amrehemu- katika kitabu chake cha Musnad, kwamba “(Ummu Salama) Aliulizwa kuhusu kisomo cha Mtume –SAW- akasema: Alikuwa akikata kisomo chake aya aya. (Bismillahirrahmaanirrahiim* Alhamdulillaahi Rabbil-aalamiin* Arrahmaanirrahiim* Maaliki Yaumiddiin)”. Imepokewa na Imam Ahmad (26583). Amesema Daarqutni kuwa (118): “Isnadi (Orodha ya wapokeaji wa Hadithi hii) ni sahihi na wote ni waaminifu”. Pia Imam Nawawi amesema kuwa ni sahihi (Almajmuu 3/333).

## 7 NI KATIKA SUNA KUTOA SALAMU KATIKA KILA RAKAA MBILI.

Imenukuliwa kwa Ibniumar –Allah amridhie yeye na baba yake- kwamba amesema kuwa: “Mtu mmoja alisimama na kusema: Ewe Mtume wa Allah, Swala ya usiku inaswaliwaje? Mtume wa Allah–SAW-akasema: **Swala ya usiku ni rakaa mbili mbili. Na ukiogopa Alfajiri (kukaribia kuchomoza) basi**

**swali Witiri rakaa moja".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (990) na Muslim kwa nambari (749).

Makusudio ya "rakaa mbili mbili" ni kwamba mtu anaswali rakaa mbili kisha anatoa salamu baada ya rakaa mbili hizo, na haswali rakaa nne kwa pamoja.



## 8 NI KATIKA SUNA KUSOMA SURA MAALUMU KATIKA RAKAA TATU ZA MWISHO.

Katika Rakaa ya kwanza anasoma: (Sabbihisma Rabbikal-aalaa) na katika Rakaa ya pili anasoma (Qul Yaa Ayyuhal Kafiruun) na katika Rakaa ya tatuanasoma (Qul Huwallaahu Ahad) tu.

Ushahidi wa hayo ni:

Hadithi ya Ubayya bin Kaab- Allah amridhie-akinukuliwa kusema kuwa: **"Mtume wa Allah –SAW-alikuwa akiswali Witiri kwa kusoma Sabbihisma Rabbikal-aalaa, na Qul Yaa Ayyuhalkaafiruun, na Qul Huwallaahu Ahad".** Imepokewa na Abudaudi kwa nambari (1423) na Annasai kwa nambari (1733) na Ibnimaja kwa nambari (1117). Imam Nawawi (Alkhulaaswa (1/556) na Albaaniy (Sahiih Anassai 1/273) wamesema kuwa ni Hadithi sahihi.

## 9 NI KATIKA SUNA WAKATI MWINGINE MTU KULETA KUNUTI KATIKA WITIRI YAKE.

Na makusudio yake hapa ni: Dua. Kunuti hiyo inafanyika katika Rakaa ya tatu ambayo mtu anasoma ndani yake Suratul Ikhlaasw.

Na Kunuti katika Witiri ni katika Suna wakati mwingine kuifanya, kwa sababu ya kuthibiti kwake kunukuliwa kwa baadhi ya Swahaba– Allah awawie radhi. Pia ni Suna kuiacha wakati mwingine. Sheikhul Islaam Ibnitaymia -Allah amrehemu- amelichagua



hili (la kuacha kukunuti). Jambo bora zaidi ni kwamba kuacha Kunuti iwe ni kwingi zaidi kuliko kuileta.

### SUALA: JE, YAFAA KUINUA MIKONO KATIKA KUNUTI YA WITIRI?

**Iliyo sahihi ni kwamba:** Mtu ananyanyua mikono. Wanazuoni wengi - Allah awarehemu - wamesema hivyo, kwa sababu ya kuthibiti kunukuliwa hilo kwa Ibniumar –Allah amridhie yeye na baba yake-, kama ilivyo kwa Baihaki ambaye amesema kuwa ni sahihi.

Baihaki –Allah amrehemu- amesema kuwa **"Hakika, idadi (kadhaa) ya Swahaba –Allah awawie radhi- waliinua mikono yao katika Kunuti"**. Angalia: Assunan Alkubraa (2/211).

### **Suala:** Kwa kitu gani mtu anaanza Kunuti yake katika Witiri?

Kauli yenye nguvu – na Allah ndiye mjuzi zaidi - ni kwamba, anaanza kwa kumhimidi Allah na kumsifu, kisha anamswalia Mtume-SAW-. Kisha anaomba dua, kwa sababu hii iko karibu zaidi kujibiwa.

**Ushahidi wa hilo ni:**

Hadithi ya Fudhala bin Ubaid – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa: "Mtume–SAW-alimsikia mtu mmoja akiomba dua katika swala yake hali ya kuwa hakumswalia Mtume-SAW-, Mtume-SAW-akasema: "Huyu ameharakisha. Kisha alimuita na kumwambia yeye na wengine kwamba: **"Mmoja wenu anaposwali, aanze kwa kumhimidi Allah na kumsifu, kisha aniswalie na aombe akitakacho baada ya hapo"**. Imepokewa na Tirmidhi kwa namba (3477), na akasema: Hii ni Hadithi nzuri na sahihi.

Na Ibniqayyim – Allah amrehemu – amesema kuwa: "Kinachopendekezwa katika dua ni mwenye kuomba aanze kwa kumhimidi Allah na kumsifu kwa shida yake, kisha aombe shida yake, kama ilivyo katika Hadithi ya Fudhala bin Ubaid. Angalia: Alwaabilus-swayyib (Ukurasa wa110).


### **SUALA: JE, MTU ANAFUTA USO WAKE KWA MIKONO YAKE BAADA YA DUA YA KUNUTI?**

**Lililo sahihi ni kwamba**: Sio Suna kupangusa uso baada ya kumaliza dua, kwa sababu ya kukosekana kwa hoja sahihi juu ya jambo hilo.

Imamu Malik - Allah amrehemu - aliulizwa kuhusu mtu anayefuta au kupangusa uso wake kwa mikono yake wakati wa kuomba dua, alilikanusha hilo na kusema “Silijui (hilo)”. Angalia kitabu cha Witri cha Maruuzi (Ukurasa wa 237).

Sheikh wa Uilamu Ibnitaimia – Allah amrehemu – amesema kuwa: “Ama mtu kupangusa uso wake kwa mikono yake hakuna isipokuwa Hadithi moja au mbili ambazo hoja haziwezi kusimama kama hoja”. Angalia: Fatawa (22/519).

### 10 DUA KATIKA THELUTHI YA MWISHO YA USIKU



Miongoni mwa Suna ambazo zinasisitizwa katika wakati wa mwisho wa usiku ni Dua. Mtu ikiwa ataomba dua katika Kunuti yake mwisho wa usiku inamtosha. Na kama hakuomba dua, ni katika Suna kuomba dua katika wakati huu, kwa sababu ni wakati ambao uwezekano wa kujibiwa dua unasisitizwa sana. Katika wakati huu Allah - SW- huteremka kuja katika mbingu ya karibu kwa namna anayostahili. Imekuja katika Sahihi Bukhaari na Sahihi Muslim kwamba Mtume wa Allah amesema kuwa: “**Mola wetu aliyetukuka na kutakasika anashuka kila usiku hadi mbingu ya chini pale inapobaki thuluthi ya mwisho ya usiku na kusema: “Ni nani anayeniomba nimwitikie? Ni nani anayeniomba nimpe? Ni nani anayeniomba msamaha nimsamehe?**”. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1145) na Muslim kwa nambari (758).

### 11 Ni Suna mtu anapotoa Salamu katika Witiri yake aseme: “Sub-haanal-malikil-qudduus” (Utukufu ni wa Mfalme Aliyetukuka) mara tatu. Anyanyue sauti yake katika mara ya tatu.

**Ushahidi wa hili ni:**

Hadithi ya Ubayi bin Kaab – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa: **“Mtume -SAW- alikuwa akisoma katika Witiri (Sabbihisma Rabbikal-aa’laa) na (Qul Yaa Ayyuhalkaafiruun) na (Qul Huwallaahu Ahadu). Na anapotoa Salamu anasema: “Sub-hanalmalikil-qudduus mara tatu”.** Imepokewa na Annasai kwa nambari (1702). Imam Annawawiy na Albaani wamesema kuwa ni sahihi, kama ilivyotangulia kutajwa hivi punde. Na katika Hadithi ya Abdulrahman bin Abzaa –Allah amridhie – imenukuliwa kwamba: **“Na**

**anyanyue sauti yake akisema (Sub-haanalmlmalikill-qudduus) katika mara ya tatu”**. Imepokewa na Ahmad kwa nambari (15354), na ameipokea Annasai kwa nambari (1734), na Albaniy amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Tahqiiq Mishkaatul Maswaabiih 1/398).

## 12 NI SUNA MTU KUAMSHA FAMILIA YAKE KWA AJILI YA KISIMAMO CHA USIKU.

Ni Suna kwa mume kumuamsha mkewe kwa ajili ya swala ya usiku, na halikadhalika mke ikiwa atasimama kwa ajili ya kusali usiku ni Suna kumuamsha mumewe na watu wengine wa familia yake kwa ajili ya hilo. Hii ni katika mlango wa kusaidiana katika kheri.

Ushahidi wa hilo ni:

Hadithi ya Aisha – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa**: “Mtume – SAW - alikuwa anaswali swala yake yote usiku na mimi nikiwa kati yake na Kibla. Na anapotaka kuswali Witiri, ananiamsha nami ninaswali Witiri”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (512) na Muslim kwa nambari (512).

Amenukuliwa Ummualama – Allah amridhie – akisema kuwa: “Mtume –SAW- aliamka na kusema: **“Sub-haanallah (Ametakasika Allah)! Ni hazina gani zimeteremushwa? Na ni fitina gani zimeteremshwa? Ni nani wa kuwaamsha wenye nyumba -anakusudia wake zake - ili waswali? Inawezekana mwanamke aliyevaa nguo duniani akawa uchi akhera”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6218).

## 13 NI KATIKA SUNA KWA MWENYE KUSIMAMA USIKU AFANYE KILICHO RAFIKI KWAKE ILI ASIJE AKAATHIRI UNYENYEKEVU WAKE.

**- Ikiwa atapata uchovu (wa kusimama) ataswali akiwa ameketi.**

Kwa mujibu wa Hadithi ya Anas – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa: **“Mtume wa Allah - SAW- aliingia msikitini na kukuta kamba imefungwa kati ya nguzo mbili. Akasema: “Ni nini hii?, Swahaba wakasema: Ni (kamba) ya Zainabu. Anaswali. Akiona uvivu au akichoka hujishikilia kwayo. Mtume akasema: “Ifungueni. Mmoja wenu aswali kwa uchangamfu wake. Na akiona uvivu au akichoka basi aketi”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1150) na Muslim kwa nambari (784).

**- Na akishikwa na usingizi alale ili aamke akiwa mchangamfu, na aswali baada ya hapo.**

Kwa mujibu wa Hadithi ya Aisha – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume -SAW-amesema kwamba "**Anaposinzia mmoja wenu wakati anaswali, alale mpaka usingizi umwishe, kwa sababu mmoja wenu anaposwali akiwa anasinzia, anaweza akawa anaomba maghufirah kumbe anajitukana mwenyewe**". Imepokewa na Bukhari kwa nambari (212), na Muslim kwa nambari (786).

**Na ni hivyo hivyo mtu akihisi usingizi na mfano wake wakati anasoma Kur'ani usiku. Ni Suna alale ili apate nguvu.**

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kwamba, Mtume wa Allah amesema kuwa: **"Anapoamka mmoja wenu usiku ikawa Kur'ani imemshinda kusoma kwa ulimi wake, ikawa hajui asemacho, basi alale".** Imepokewa na Bukhari (787).

### 14 Suna kwa yule aliyepitikiwa na kisimamo cha usiku ni kuswali mchana kwa Shufwa (bila ya Witiri).

Ikiwa ni katika ada yake kuswali Witiri kwa rakaa tatu, lakini akalala ikampita Witiri hiyo au akawa mngonjwa na hivyo akashindwa kuswali, basi ataiswali Witiri hiyo mchana rakaa nne. Na ikiwa ni katika ada yake kuswali Witiri rakaa tano, na akalala Witiri ikampita au akawa mgonjwa, ataswali Witiri hiyo mchana rakaa sita. Mtume –SAW- alikuwa akifanya hivyo, na kwa sababu ilikuwa ni katika ada yake –SAW- kuswali Witiri rakaa kumi na moja. Aisha –Allah amridhie – akimuelezea Mtume –SAW- anasema kuwa: **"Na Mtume alikuwa usingizi unapomshinda au ugonjwa unapomzidia na kushindwa kuswali usiku, anaswali mchana rakaa kumi na mbili"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (746).



## PILI: WAKATI WA ALFAJIRI



Kuna ibada mbalimbali ambazo ni katika mwongozo wa Mtume –SAW-:

### Adhana. Ndani yake kuna Suna nyingi:

#### 1 Kufuatisha anavyosema Muadhini.

Ni Suna kwa anayesikia Adhana aseme mfano wa vile anavyosema Muadhini, isipokuwa katika mara mbili za tamko la: **"Hayya Alas-swalaa"** na **"Hayya Alal-falaah".** Hapo atasema: **"Laa Hawla Walaa Quwwata Illaa Billaah".**

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abdallah bin Amri bin Al-aasw – Allah amridhie yeye na baba yake – aaliyenukuliwa kusema kuwa, alimsikia Mtume –SAW- akisema: **"Mnapomsikia Muadhini semeni mfano wa vile anavyosema"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (384). Pia Suna hii ya kufuatisha anavyosema Muadhini imethibiti kwa mujibu wa Hadithi ya Umar bin Alkhattwaab –Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume –SAW- amesema kwamba: **"Muadhini anaposema Allahu Akbar, Allahu Akbar, na mmoja wenu akasema: Allahu Akbar Allahu Akbaru. Kisha (Muadhini) akisema: Ash-hadu Allaa Ilaaha Illallaah, na (mmoja wenu naye) akasema: Ash-hadu Allaa Ilaaha Illallaah". Kisha (Muadhini) akisema: "Ash-hadu**

**Anna Muhammadan Rasuulullaah", (Mmoja wenu naye) akasema: "Ash-hadu Anna Muhammadan Rasuulullaah". Kisha (Muadhini) akisema: "Hayya Alas-swalaa" (Mmoja wenu naye) akasema: "Laa Hawla Walaa Quwwata Illaa Billaah". Kisha (Muadhini) akisema: "Hayya Alal-falaah", (Mmoja wenu naye) akasema: "Laa Hawla Walaa Quwwata Illaa Billaah". Kisha (Muadhini) akisema: "Allahu Akbar Allahu Akbar" (Mmoja wenu naye) akasema: "Allahu Akbar, Allahu Akbar". Kisha (Muadhini) akisema: Laa Ilaaha Illallaah, (Mmoja wenu naye) Akasema: 'Laa Ilaaha Illa Allah' kutoka ndani ya moyo wake ataingia peponi".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (385).

Wakati wa kufuatisha anavyosema Muadhini kwa Swala ya Alfajiri, mwenye kufuatisha Adhana atasema vile asemavyo Muadhini**: "Asswalaatu Khairun Minan-nauum".**

## 2 Uradi huu unasomwa baada ya Shahada mbili.

Baada ya Muadhini kusema: **"Ash-hadu Anna Muhammadan Rasuulullah"** ya mara ya pili, ni Suna kusoma ule uradi uliokuja katika Hadithi ya Saad – Allah amridhie – akimnukuu Mtume –SAW- kwamba amesema kuwa: **"Mwenye kusema anaposikia Muadhini: Ash-hadu Allaa Ilaaha Illallaah Wahdahuu Laa Shariika Lah. Wa-anna Muhammadan Abduhu Warasuuluh, Radhwiitu Billaahi Rabban, Wabi-muhammadin Rasuulaa, Wabil-islaami Diinaa" yakiwa na maana: (Nashuhudia ya kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah Peke Yake, hana mshirika, na kwamba Muhammad ni Mja wake na Mtume wake. Nimeridhia Allah kuwa Mola wangu, na Muhammad kuwa Mtume), atasemehewa dhambi zake".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (386).

## 3 KUMSWALIA MTUME –SAW- BAADA YA ADHAANA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abdallah Ibniamri – Allah amridhie yeye na baba yake – akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema kwamba: **"Mkisikia Muadhini semeni kama anavyosema, kisha niswalieni. Atakayeniswalia mara moja Allah atamswalia mara kumi. Kisha niombeeni kwa Allah nipate Wasila (cheo, daraja). Hiyo ni hadhi peponi haistahiki kupewa isipokuwa mja miongoni mwa waja wa Allah, na nataraji mimi niwe (mja) huyo. Atakayeniombea Wasila, uombezi wangu utakuwa halali kwake (atapata uombezi wangu".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (384).

Na namna bora zaidi katika namna za kumswalia Mtume ni: "Swala Ibrahimia": **Allaahumma Swalli Alaa Muhammad, Wa-alaa Aali Muhammad, Kamaa Swallayta Alaa Ibraahiim Wa-alaa Aali Ibraahiim.....".**

### 4 KUSOMA DUA ILIYOTHIBITI BAADA YA ADHANA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Jabir – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema kwamba: **"Mwenye kusema pindi anaposikia Adhana: "Allaahuma Rabba Haadhihid-daawati-taamma, Wasswalaatilqaa-ima, Aati Muhammadan Alwasiila Walfadhiila, Wab-ath-hu Maqaaman Mahmuudan Alladhii Wa-adtahu", (Ewe Allah, Bwana wa ulingano (wito) huu uliotimia, na swala iliyo simama, mpe Muhammad Wasila na fadhila, na mfikishe daraja yenye kusifiwa, ambayo umemuahidi, utakuwa halali kwake Uombezi wangu Siku ya Kiyama".** Hadithi imepokewa na Bukhari ikiwa na nambari (614).

### 5 DUA BAADA YA ADHANA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abdallah bin Amri – Allah amridhie yeye na baba yake - **: "Kwamba mtu mmoja alisema: Ewe Mtume wa Allah, hakika Waadhiini wanatushinda kwa fadhila. Mtume – SAW – akasema: "Sema kama (Waadhini) wanavyosema, na ukimaliza omba utapewa".** Imepokewa na Abudaud kwa nambari (524). Ibnihajar (Nataa-ijul-afkaar 1/367) pia Albaani (Sahiihulkalimit-twayyib, ukurasa 73) wametaja kuwa ni Hadithi Hasan.



Pia kwa mujibu wa Hadithi ya Anas – Allah amridhie – aliyenukuu kwamba, Mtume – SAW – amesema kuwa: **"Dua kati ya Adhana na Iqama hairejeshwi (haikataliwi)"**. Hadithi hii imepokewa na Annasai kwa nambari (9895) na Ibnikhuzaima (2/221/425) ameitaja kuwa ni sahihi (1/221/425).

## SUNA YA ALFAJIRI, NA NDANI YAKE KUNA SUNA NYINGI:

Suna za Alfajiri ni Suna za mwanzo zilizopangiwa muda maalumu ambazo mja anazifanya katika siku yake. Ndani yake kuna Suna mbalimbali. Kabla hatujazielezea, hatuna budi kubainisha baadhi ya yanayohusu Suna zilizopangiwa muda maalumu. Suna zilizopangiwa muda maalumu: Ni Suna


za kudumu zinazoambatana na Swala za Faradhi. Ni Rakaa kumi na mbili.

Imenukuliwa kwa Ummuhabiba – Allah amridhie – akisema, nimemsikia Mtume wa Allah – SAW – akisema kwamba: “**Atakayeswali Rakaa kumi na mbili katika siku atajengewa nyumba peponi**”. Imepokewa na Muslim kwa nambari (728) na imepokewa pia na Tirmidhi na akaongeza kusema: **“Rakaa nne kabla ya Adhuhuri, na Rakaa mbili baada yake, na Rakaa mbili baada ya Magharibi, na Rakaa mbili baada ya Ishaa, na Rakaa mbili kabla ya Swala ya Alfajiri**”. Imepokewa na Tirmidhi kwa nambari (415) na akasema “Ni Hadithi Hasan, Sahihi”.

**Jambo bora ni kuswali Suna zenye mpangilio wa muda maalumu nyumbani.**

Imenukuliwa kwa Zaid bin Thabit – Allah amridhie -: kwamba, Mtume –SAW- amesema kuwa: **“Enyi watu, swalini majumbani mwenu kwa sababu Swala bora kabisa ya mtu ni nyumbani kwake isipokuwa Swala ya fardhi”**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (7290), na Muslim kwa nambari (781).

### SUNA ZENYE KUPANGIWA MUDA MAALUMU ZILIZOSISITIZWA SANA.



Suna yenye kupangiwa muda maalumu iliyosisitizwa sana ni Suna ya Alfajiri.

Ushahidi wa hilo ni huu ufuatao:

1. Hadithi ya Aisha – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa: **“Mtume hakuwa na Swala yoyote ya Suna ambayo alikuwa akiijali sana kuliko Rakaa mbili kabla ya Swala ya Asubuhi”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1196) na Muslim kwa nambari (724).
2. Hadithi ya Aisha – Allah amridhie - akimnukuu Mtume – SAW – kwamba amesema kuwa: **“Rakaa mbili za Alfajiri ni bora kuliko dunia na vilivyomo ndani yake**”. Imepokewa na Muslim kwa nambari (725).

### Suna ya Alfajiri in mambo kadhaa maalumu:

* **Kwanza:** Imethibiti kisheria kuziswali katika safari na katika hali isiyokuwa ya safari, kama ilivyopokewa katika Sahihi Bukhari na Sahihi

Muslim. Ama Suna nyingine zilizopangiwa muda maalumu, ni Suna kuziacha katika safari, kama Rakaa za Suna za Adhuhuri, Magharibi na Ishaa.

* **Pili:** Thawabu zake ni bora kuliko dunia na vilivyomo ndani yake, kama ilivyotangulia kuelezwa.
* **Tatu:** Ni Suna kuziswali kwa wepesi, na ushahidi wa hilo umetangulia kuelezwa.

Na pia ushahidi wa hilo ni Hadithi ya Aisha – Allah amridhie – ambaye imenukuliwa kuwa, alikuwa anasema kwamba: "**Mtume –SAW- alikuwa anaswali Rakaa mbili za (Suna) ya Alfajiri, anaziswali kwa wepesi mpaka nikawa nasema: Hivi amesoma ndani yake Ummulqur-aan (Suratulfaatiha) au hakusoma?.** Ameipokea Bukhari kwa nambari (1171) na Muslim kwa nambari (724).

Lakini ni sharti kwamba: Wepesi huo usiwe unaharibu mambo ya lazima, au kupelekea kudonoadonoa swala yake, akaingia katika makatazo.

* **Nne:** Katika Suna ya Alfajiri ni Suna kusoma (**Qul Yaa Ayyuhal Kaafiruun**) katika Rakaa ya kwanza baada ya Sura Alfaatiha, na katika Rakaa ya pili ni Suna kusoma (**Qul Huwallaahu Ahad**) kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhurara katika mapokezi ya Muslim.

  Au katika Rakaa ya kwanza baada ya Sura Alfaatiha asome: (**Quuluu Aamannaa Billahi Wamaa Unzila Ilaynaa Wamaa Unzila Ilaa Ibraahiima Wa-Ismaaila Wa-Is-haaqa Wa Yaaquuba, Wal-Asbaatw, Wamaa Uutiya Muusaa Wa-Isaa, Wamaa Uutiyannabiyyuuna Mirrabbihim, Laa Nufarriqu Bayna Ahadin Minhum, Wanahnu Lahuu Muslimuun**", **(Semeni: "Tumemwamini Allah na yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwa Ibrahm na Ismail na Is-haak na Yakubu na Asbaat na aliyopewa Musa na Isa na waliyopewa Manabii kutoka kwa Mola wao. Hatutofautishi baina ya mmoja yeyote miongoni mwao, na sisi ni wenyekujisalimisha kwake tu".** (Sura Albaqara: 136).

Na katika ya pili asome: **"Qul Yaa Ahlalkitaab, Taalaw Ilaa Kalimatin Sawaa-in Baynanaa Wabaynakum, Anlaa Na'abuda Illallaah, Walaa Nush-rika Bihii Shay-an, Walaa Yattakhidha Ba'adhunaa Arbaaban Min Duunillaah. Fa-in Tawallaw Faquulush-haduu Bi-annaa Muslimuun", (Sema: Enyi Watu wa Kitabu, njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu, kwamba tusiabudu isipokuwa Allah tu, na wala tusikishirikishe naye kitu**

**chochote, na wala baadhi yetu wasiwafanye wengine Miungu badala ya Allaah. Wakikengeuka, waambieni: Shuhudieni kwamba sisi ni Waislamu".** (Sura Aal-imran: 52), kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniabbas katika mapokezi ya Muslim. Hii ni katika Suna ambazo zimepokewa kwa namna mbalimbali. Wakati mwingine anafanya hii, na mara nyingine anafanya ile.

* **Tano**: Ni suna kujilaza kwa ubavu wa kulia baada ya Suna a Alfajiri.

Na ushahidi wa hili ni:

Hadithi ya Aisha – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa **"Mtume – SAW - akishaswali Rakaa mbili za kabla ya (swala ya) Alfajiri alikuwa anajilaza kwa ubavu wake wa kulia".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1160) na Muslim kwa nambari (736).

## Kwenda Msikitini. Kuna Suna kadhaa:

Kwa kuwa Swala ya Alfajiri ndio swala ya kwanza katika siku ambayo mja anakwenda msikitini, kwenda huku kuna mambo mengi ambayo ni suna mtu ayafanye:

### 1 Ni Suna kwenda mapema msikitini.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhurara –Allah amridhie- akinukuliwa kusema kuwa, Mtume –SAW- amesema kwamba: **"Lau watu wangelijua (fadhila) za kuwahi mapema msikitini wangeshindania (katika kuwahi msikitini)".** Ameipokea Bukhari kwa nambari (615) na Muslim kwa nambari (437).

Kuwahi: Ni kwenda mapema kwa ajili ya Swala.

### 2 Mtu atoke nyumbani kwake akiwa Twahara, ili hatua zake anazotembea ziandikwe.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira –Allah amridhie- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW-amesema kwamba: **"Mtu kuswali kwa Jamaa huzidi kuswali kwake nyumbani kwake, kuswali kwake sokoni kwake kwa daraja ishirini na ushei. Hiyo ni kwa sababu, mmoja wao anapotawadha vizuri kisha akenda msikitini, hakuna lililomuinua isipokuwa**



**Swala tu, hakusudii isipokuwa Swala tu, basi (atakuwa) hapigi hatua isipokuwa atapandishwa daraja kwa hatua hiyo na ataondolewa dhambi kwa hatua hiyo mpaka aingie msikitini. Akishaingia msikitini, ataendelea kuwa katika Swala madamu Swala ndio iliyomzuia (kubaki humo msikitini). Na Malaika humuombea rehema mmoja wenu madamu yupo katika mahali pake aliposwali; wanaomba: Ewe Mola wetu, mrehemu. Ewe Mola wetu, msamehe. Ewe Mola wetu, mkubalie toba yake, (Hali inaendelea kuwa hivyo) madamu hajaudhi humo (msikitini) au kupatwa na Hadathi (kutengukwa na Udhu)".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (649).

### 3 Mtu atoke kwenda kuswali kwa utulivu na upole.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira – Allah amridhie – akimnukuu Mtume- SAW- kwamba amesema: **"Mkisikia Ikama, tembeeni kwenda kuswali mkilazimika kuwa katika utulivu na upole, na msifanye haraka. Mtakacho kiwahi swalini, na kitachowapiteni kitimizeni"**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (636) na Muslim kwa nambari (602).

Imamu Nawawiy, Allah amrehemu, amesema kuwa: **"Upole maana yake ni kuwa mtaratibu katika kutenda na kujiepusha kuchezacheza. Utulivu ni katika muonekano, kama kuinamisha macho (kwa kutoangalia haramu) na kupunguza sauti (wakati wa kuzungumza) na kutogeukageuka".** Sharhu Sahih Muslim, Hadithi nambari (602), Mlango wa kupendekezwa kwa kwenda kuswali kwa utulivu na upole na kukatazwa kuiendea swala kwa kukimbia.

### 4 Kutanguliza mguu wa kulia wakati wa kuingia msikitini, na kutanguliza mguu wa kushoto wakati wa kutoka.




Kwa mujibu wa Hadithi ya Anas – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa: **"Ni katika Suna unapoingia msikitini uanze kwa mguu wako wa kulia, na unapotoka uanze kwa mguu wako wa kushoto".** Imepokewa na Hakim (1/388) na kusema kuwa ni sahihi kwa sharti ya Muslim.

### 5 Wakati wa kuingia msikitini na wakati wa kutoka alete Uradi ambao umepokewa.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhamiid, au Abu-usaid akinukuliwa kusema kuwa, Mtume – SAW – amesema kwamba: **"Mmoja wenu anapoingia**

**msikitini, aseme: Allaahumma Iftah Lii Ab-waaba Rahmatik (Ewe Mola wangu, nifungulie milango ya rehema zako), na anapotoka aseme: Allaahumma Innii As-Aluka Min Fadhwlik", (Ewe Mola wangu, ninakuomba fadhila zako"** Imepokewa na Muslim kwa nambari (713).

### 6 Aswali rakaa mbili za Tahiyyatulmasjid (kusalamia msikiti).



Na hii ni mtu anapokuja msikitini mapema. Ni suna kwake asikae mpaka aswali Rakaa mbili, kwa mujibu wa Hadithi ya Abukatada – Allah amuwie radhi – akinukuliwa kusema kuwa, Mtume – SAW – amesema kwamba **"Mmoja wenu anapoingia Msikitini, asiketi mpaka aswali Rakaa mbili"**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1163).

Na Suna ya Kabliya (sala ya Suna iliyopangiwa muda wa kabla ya sala ya faradhi) inatosheleza Tahiyyatul Masjid ikiwa Swala hiyo (ya Faradhi) ina Suna ya Kabliya, kama vile Swala ya Alfajiri na Adhuhuri, au Suna ya Dhuha ikiwa mtu ataingia msikitini wakati wa Dhuha, au Swala ya Witiri ikiwa mtu ataiswali msikitini, au swala ya faradhi. Hii ni kwa sababu, lengo la Tahiyyatul Masjid ni kuwa mtu asikae hadi aswali, kwa sababu katika kufanya hivyo kuna kuiimarisha misikiti kwa kuswali, ili mtu asije akawa anaingia misikitini na kutoka bila ya kuswali.

### 7 Ni Suna kwa wanaume kuwahi Safu ya kwanza, kwa Sababu ndio Safu bora zaidi. Na kwa wanawake Safu bora zaidi ni ya mwisho.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume – SAW – amesema kwamba: **"Safu bora zaidi ya wanaume ni Safu ya kwanza**, **na Safu mbaya zaidi ni Safu ya mwisho.** Na **Safu bora zaidi ya wanawake ni Safu ya mwisho, na Safu mbaya zaidi ya wanawake ni (Safu yao) ya kwanza"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (440). Maana ya Bora zaidi ni kwamba: Ina thawabu na fadhila nyingi sana. Na maana ya mbaya zaidi ni kwamba: Ina thawabu na fadhila chache sana.

Na Hadithi inalenga ni pale wanaume na wanawake watakaposwali pamoja; yaani kwa Jamaa, na hakuna kizuizi kati yao kama vile ukuta na mfano wake. Hapo, itakuwa safu bora ya wanawake ni safu ya mwisho, kwa sababu itakuwa ndio sitara zaidi kwao wasionekane na wanaume. Ama pale penye kizuizui kati ya safu za wanaume na wanawake, kama vile ukuta

na mfano wake au kama ilivyo katika misikiti yetu mingi siku hizi ambapo wanawake wametengewa eneo maalumu lenye kujitegemea, katika hali hii safu bora zaidi ya wanawake ni safu ya kwanza, kwa sababu ya kukosekana kwa sababu ya kuwa karibu na wanaume. Hukumu huzunguka kufuata sababu yake kwa kuwepo na kwa kukosekana. Pia ni kwa sababu ya kuwepo kwa Hadithi kadhaa za jumla zinzoelezea ubora wa safu ya kwanza. Baadhi ya Hadithi hizo ni hizi zifuatazo:

Hadithi ya Abuhuraira – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema kwamba: **“Lau kama watu wangejua (faida, fadhila na mema) yaliyomo kwenye Adhana na safu ya kwanza, kisha wasipate (njia ya kupata nafasi ya kuwa katika safu ya kwanza) ila kwa kupiga kura, wangepiga kura. Na lau kama wangejua (faida, fadhila na mema) yaliyomo katika kwenda msikitini mapema, wangelishindania. Na lau kama wangelijua (faida, fadhila na mema) yaliyomo ndani ya Swala ya Alfajiri na Swala ya Isha wangeliziendea japo kwa kutambaa”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (615) na Muslim kwa nambari (437).

### 8 Ni Suna kwa Maamuma kuwa karibu na Imamu wake.

Iliyo bora kwa maamuma katika kusimama safu kwa ajili ya swala ni safu ya kwanza kama ilivyotangulia. Kisha awe na hamu ya kuwa karibu na imamu. Kuwa karibu zaidi (na imamu) kutoka upande wa kulia au wa kushoto ndio bora zaidi.

Na ushahidi wa hilo ni:

Hadithi ya Abdallah bin Masoud – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah-SAW-amesema kwamba: **“Na wawe karibu yangu (wasimame karibu na mimi) miongoni mwenu wale wenye balehe na kupevuka akili”.** Ameipokea Abudaud kwa nambari (674) na Tirmidhiy kwa nambari (228). Kauli ya Mtume kwamba: **“wawe karibu yangu”** ni hoja kwamba kuwa karibu na imamu ni jambo linalo takikana kwa upande wowote utakaokuwa.

## Suna za swala:



Kutokuiendea Kwako Swala Ya Jamaa Msikitini Kunakunyima Fadhila Nyingi, Hata Hatua Zako Kuuendea Msikiti Zinakunyanyulia Daraja Mbele Ya Allah Na Kukufutia Makosa

### Swala ina Suna nyingi. Katika hizo tunataja hizi zifuatazo:

### 1 Sutra (Sitara): Na ina suna zifuatayo:

### 1 Ni Suna kuweka Sutra (Kizuizi):

Sutra ni Suna kwa imamu na anayeswali peke yake. Ama maamuma Sutra ya imamu ndio Sutra yake. Kuweka Sutra ni Suna.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abusaid Alkhudhriy –Allah amridhie- iliyohusishwa na Mtume. Ndani ya Hadithi hiyo mna kauli kwamba: **"Anaposwali mmoja wenu ikawa ameweka kitu cha kumkinga dhidi ya watu….."**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (509) na Muslim kwa nambari (505). Hadithi zinazoelezea hoja ya kwamba Sutra ni Suna ni mingi. Mtume alifanya Sutra kitanda, ukuta, kisiki, mbao, mkuki, bakora, mnyama na vingine mbali na hivyo.

Kuweka Sutra ni takwa la sheria (ikiwa mtu anaswali) katika majengo au sehemu ya wazi, safarini au sio safarini. Pia ni sawa amechelea mtu kukatiza (mbele yake) au hakuchelea mtu kukatiza. Hii ni kwa sababu Hadithi hazikutofautisha kati ya kuswali ndani ya majengo au katika sehemu ya wazi,

na pia ni kwa sababu Mtume-SAW- alikuwa akiweka Sutra katika safari zake na ukazi wake, kama ilivyo katika Hadithi ya Abujuhaifa – Allah amridhie - iliyopokewa na Bukhari (501) na Muslim (503).

### 2 Ni suna kuwa karibu na Sutra.



Mtu anaposogelea Sutra, Suna ni kwamba kati ya sehemu yake ya kusujudu na kati ya Sutra pawe na eneo la kiasi cha kuweza kupita mbuzi.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Sahli bin Saad Alsaaidiy-Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kwamba: **"Ilikuwa kati ya mahali anaposwali Mtume -SAW- na ukuta nafasi ya kupita mbuzi."** Ameipokea Bukhari kwa nambari (496) na Muslim (508). Makusudio ya mahali pa kuswalia ni: sehemu ambayo Mtume - SAW- alikuwa akisujudu. Imekuja nukuu kwa Ahmad na Abudaud kwamba kati ya Mtume na kati ya Sutra ilikuwa ni dhiraa tatu. Nukuu hii imepokewa na Ahmad kwa nambari (6231) na Abudaud kwa nambari (2024). Albaaniy amesema kuwa ni sahihi (Swahiih Abudaud 6/263), na chimbuko lake liko Bukhari kwa nambari (506). Hii ni kwa kuzingatia kwamba, mtu pindi anaposimama kwa ajili ya kuswali masafa yawe hivyo kati yake na kati ya Sutra.

### 3 Ni suna kumzuia mwenye kupita mbele ya mtu anayeswali.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Abusaid – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW-amesema kwamba: **"Mmoja wenu akiswali mbele kukawa na kitu kinachomsitiri (kinachomkinga) dhidi ya watu wengine, na mtu akataka kupita mbele yake, basi amzuie. Akikataa, apigane naye, kwa sababu huyo ni shetani"**. Ameipokea Muslim kwa nambari (505).

Ama ikiwa mwenye kupita mbele ya mwenye kuswali ni mwanamke au mbwa mweusi au punda, ni wajibu kumzuia katika kauli iliyo sahihi, kwa sababu hao wanakata (wanabatilisha) swala, kama ilivyokuja katika Hadithi ya Abudhari – Allah amridhie -, tofauti na vitu vingine ambavyo sio mwanamke, mbwa mweusi na punda. Hivyo

havibatilishi Swala. Imepokewa na Muslim kwa nambari (510), na Shekhe wetu Ibniuthaimiin, Allah amrehemu, amechagua kauli hii

### 4 Ni suna kupiga mswaki kwa kila swala.



Na hii ndio sehemu ya tatu katika sehemu ambazo inasisitizwa kupiga mswaki.

Na ushahidi wa hilo ni:

Hadithi ya Abuhuraira – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah–SAW- amesema kwamba: **“Lau kama si kuuonea uzito umma wangu, basi ningeliwaamuru kupiga mswaki katika kila swala”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (887).

## 2 Wakati wa kusimama kwa ajili ya Swala inasuniwa kufanya yafuatayo:

### 1 Kunyanyua mikono wakati wa kuleta Takbira ya kuanza Swala.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniumar – Allah amridhie yeye na baba yake – aliyenukuliwa kusema kwamba: **“Mtume wa Allah –SAW- alikuwa akinyanyua mikono yake kufikia usawa wa mabega yake anapoanza kuswali, na anapoleta Takbira kwa ajili ya kurukuu, na anapoinua kichwa chake kutoka katika rukuu, alikuwa akiinyanyua mikono yake pia. Na anasema: “Samiallaahu Liman Hamidah, Rabbanaa Walakal Hamdu”, (Allah anamsikia mwenye kumhimidi. Ewe Mola wetu, sifa zote njema ni zako), na alikuwa hafanyi hivyo katika kusujudu”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (735) na Muslim kwa nambari (390).

Ibnihubaira - Allah amrehemu – amesema kuwa: “Na (wanazuoni) wamekubaliana kuwa, kunyanyua mikono wakati wa kupiga Takbira ya kuanza Swala ni Suna na sio wajibu”. Angalia: Al-ifswaah (1/123).

Sehemu Za Kunyanyua Mikono Ambazo Nususwi Zimethibiti Ndani Yake Ni Sehemu Nne

**Wakati Wa Takbira Ya Kuhirimia Swala**

**Wakati Wa Kurukuu**

**Wakati Wa Kunyanyuka Kutoka Katika Kurukuu**

Sehemu Hizi Tatu Zimethibiti Katika Sahihi Mbili (Bukhaar na Muslim) Kutoka Katika Hadithi Ya Ibn 'Umar Allah Amridhie Kama Ilivyotangulia, Na Sehemu Ya Nne Ni:

**Wakati Wa Kusimama Kutoka Katika Attahiyyatu Ya Kwanza**

Na Hii Imethibiti Vilevile Kutoka Kwa Ibn 'Umar Allah Amridhie Katika Sahihi Bukhaar

### 2 Ni Suna wakati wa kunyanyua mikono vidole viwe vimenyooka.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhurara – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa, "Mtume–SAW-alikuwa anaposimama kwa kuswali ananyanyua mikono yake". Imepokewa na Ahmad kwa nambari (8875) na Abudaud kwa nambari (753) na Tirmidhi kwa nambari (240), na Albaniy ameitaja kuwa ni sahihi (Swahiih Abii 3/341).

### 3 Ni Suna kunyanyua mikono kufike hadi katika sehemu iliyosuniwa.





Zimekuja Hadithi kwa njia mbili, zilizonukuliwa kwa Mtume –SAW- katika kuweka mpaka wa kunyanyua mikono miwili. Imekuja kwamba, kunyanyua mikono ni hadi mkabala na mabega, kama ilivyo katika Swahihi Bukhari na Swahihi Muslim ikinukuliwa kwa Ibniumar – Allah amridhie yeye na baba yake – na ambayo imepokewa na Bukhari kwa nambari (735) na Muslim kwa nambari (390). Pia imekuja kwamba, kunyanyua mikono ni hadi mkabala wa kingo za masikio; yaani mkabala sehemu za juu za masikio. Hayo yapo kwa Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Malik bin Huwairith – Allah amridhie – ambayo ameipokea Muslim (391). Mwenye kuswali anatakiwa mara afanye namna hii na mara nyingine afanye namna ile.

## 4 BAADA YA TAKBIRA YA KUANZA SWALA NI SUNA KWA MWENYE KUSWALI AWEKE MKONO WAKE WA KULIA JUU YA MKONO WA KUSHOTO.

Na hii ni kwa maafikiano ya wanazuoni, kama alivyonukuu Ibnihubaira - Allah amrehemu - . Angalia: Al-ifswaah (1/124).

## 5 NI SUNA ASHIKE MKONO WA KUSHOTO KWA MKONO WAKE WA KULIA.





**Namna ya Kwanza:** Aweke mkono wake wa kulia juu ya mkono wake wa kushoto. Hii ni kutokana na Hadithi ya Wail bin Hujri – Allah amridhie – ambaye amenukuliwa kusema kuwa: **"Nilimuona Mtume wa Allah –SAW- alipokuwa amesimama katika Swala, alishika mkono wake wa kushoto kwa mkono wake wa kulia ukiwa juu".** Imepokewa na Abudaud kwa nambari (755), na Annasai kwa nambari (888), na Albaniy ameitaja kuwa ni sahihi.

**Namna ya Pili:** Ni kuweka mkono wake wa kulia juu ya dhiraa ya kushoto. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Sahli bin Saad – Allah amridhie – aliyenukuliwa kusema kuwa: **"Watu walikuwa wakiamrishwa mtu kuweka mkono wa kulia juu ya dhiraa yake ya kushoto katika Swala"**. Imepokewa na Bukhari kwa namba (740).

Atakuwa mara akiweka juu ya mkono na mara nyingine anaweka juu ya dhiraa, ili awe amefanya namna zote katika kuteleza Suna.

## 6 NI SUNA KUSEMA DUA YA KUFUNGUA (SWALA).

Dua ya kufungua Swala ina matamko ya namna mbalimbali. Inapendekezwa mtu kutumia matamko tafauti tafauti. Mata atumie matamko haya, na mara nyingine atumie matamko yale. Miongoni mwa matamko yaliyothibiti ni haya:

1. **"Sub-haanakallaahumma Wabihamdika. Tabaarakasmuka, Wataalaa Jadduka, Walaa Ilaaha Ghairuka"**. (**Kutakasika ni kwako Eee Mola wangu, na sifa njema zote ni zako. Limetukuka jina lako na uko juu utukufu wako na hapana mwengine badala yako apasae kuabudiwa**). Ameipokea Ahmad kwa nambari (11473), na Abudaud kwa nambari (776), na Tirmidhi (243) na Annasai (900) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abusaid – Allah amridhie -. Hadithi hii ndani yake kuna maneno (yaani kuna walakini juu ya usahihi wake), isipokuwa ina njia nyingi ambazo inapata nguvu kwa njia hizo. Na Ibnihajar ameichukulia kuwa ni Hadithi Hasan. (Nataa-ijul Afkaar 1/412).

2. **"Alhamdulillaah Hamdan Kathiiran Twayyiban Mubaarakan Fiih"**. (Sifa njema ni za Allah, sifa nyingi, nzuri na zenye Baraka). Na katika kuelezea fadhila za tamko hili, amesema Mtume –SAW- kuwa: **Nimewaona Malaika kumi na mbili wakishindana nani atakayelipeleka (tamko hili) juu (mbinguni)"**. Imepokewa na Muslim (600) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Anas.

3. **"Allaahumma Baa-id Baynii Wabayna Khatwaayaaya Kamaa Baa-adta Baynal-Mashriqi Wal-Maghrib. Allaahumma Naqqinii Min Khatwaayaaya Kamaa Yunaqqath-thawbul Abyadhwu Minad-Danasi. Allaahumma-Ghsilinii Min Khatwaayaaya Bil-Maa-i Wath-thalji Walbarad". (Ewe Mola wangu, niweke mbali na makosa yangu kama ulivyoweka mbali baina ya Mashariki na Magharibi. Ewe Mola wangu, nisafishe makosa yangu kama vile nguo nyeupe inavyosafishwa isiwe na uchafu. Ewe Mola wangu, nisafishe makosa yangu kwa maji na theluji na barafu)".** Imepokewa na Bukhari (744) na Muslim (598) katika Hadithi ya Abuhuraira.

4. **“Allahu Akbar Kabiiran, Walhamdulillaahi Kathiiran, Wasub-haanallaahi Buk-ratan Wa-aswiilan”. (Allah ni Mkubwa, Na sifa njema ni za Allah kwa wingi. Ametakasika Allah asubuhi na jioni)**. Na katika kuelezea fadhila za tamko hili, Mtume – SAW – amesema kuwa: **“Nimeyashangaa maneno haya! Milango ya mbinguni imefunguliwa kwa ajili yake”.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (601), ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Ibniumar – Allah amridhie yeye na baba yake-.

## 7 KUOMBA KINGA DHIDI YA SHETANI (ISTIADHA)

Istiadha ni Suna, na inasuniwa kuleta aina mbalimbali za matamshi ya Isitiadha. Mara analeta aina hii na mara nyingine analeta aina ile. Katika matamshi yaliyopokewa ni:

1. **“Auudhu Billaahi Minash-shaytwaanirrajiim”, (Najilinda kwa Allah dhidi ya shetani aliyelaaniwa**).

Na hii ndio namna ambayo wanachuoni wengi - Allah awarehemu – wameichagua, kwa kuzingatia kauli ya Allah isemayo kuwa: (**Unaposoma Qur’ani, basi (kwanza) omba kinga kwa Allah dhidi ya shetani aliyelaaniwa)**. (Sura Annahli: 98).

2. **Auudhu Billaahis-samiiul-aliim. Minash-haitwaanir-rajiim. (Najikinga kwa Allah Mwenye kusikia, Mwenye kujua dhidi ya shetani aliyelaaniwa).**

Kutokana na kauli ya Allah aliyetukuka: “**Na ka utakupata ushawishi wowote kutoka kwa shetani, basi omba kinga kwa Allah. Hakika, yeye ndiye Mwenye kusikia (yote), Mjuzi (wa yote**)”. (Sura (Haamiym) Fus-swilat: 36).

## 8 BASMALA (Kusema BISMILLAAHI).

Ni katika Suna alete Basmala baada ya Isitiadha na kusema: **“Bismillaahir-rahmnaanir-rahiim”,** kwa mujibu wa Hadithi ya Nuaimu Almujammir – Allah amridhie – akinukuliwa kusema kuwa: **“Niliswali nyuma ya Abuhuraira – Allah amridhie – akasoma: “Bismillaahir-Rahmaanir-Rahiim”, kisha akasoma Mama wa Kur’ani (Sura Alfaatihah)…na ndani ya hadithi hiyo kuna maneno: “Ninaapa kwa (Allah) Ambaye roho yangu iko mkononi mwake kwamba, Swala yangu inafanana sana na ile ya Mtume wa Allah kuliko yeyote miongoni mwenu”**. Imepokewa na Nasai kwa nambari (906), na pia Ibnihuzaima ambaye amesema kuwa ni sahihi (1/251). Amesema Darukutni kuwa: “Hii ni Hadithi sahihi, na wapokezi wake wote ni waaminifu”. Assunan 2/46.

Aidha kinachoitoa isiwe wajibu ni kwamba, Mtume wa Allah – SAW - hakumfundisha Basmala (Bismillaahi) yule mtu aliyekosea katika Swala yake. Alimuelekeza tu asome Kifunguzi cha Kitabu yaani (Sura Alfaatiha), kama ilivyo katika Hadithi ya Abuhuraira – Allah amridhie - ambayo imepokewa na Bukhari (757) na Muslim (397).

## 9 KUSEMA "AAMIIN" PAMOJA NA IMAMU.

Na hiyo ni pindi imamu anaposoma Sura Alfaatiha kwa sauti ya wazi katika Swala ambayo imamu anasoma kwa sauti ya wazi (Jahria). Ni katika Suna maamuma aitikie "Aamiin", pindi imamu anaposema "Aamiin", kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira –RAA- aliyenukuliwa kusema kwamba, Mtume –SAW-amesema kuwa: **"Imamu anaposema "Aamiin" na nyinyi semeni "Aamiin, kwa sababu yule ambaye "Aamiin" yake itawafikiana (itaendana pamoja) na "Aamiin" ya Malaika, atasamehewa dhambi zake zilizotangulia".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (780) na Muslim kwa nambari (410).

## 10 KUSOMA SURA BAADA SURA ALFAATIHA.

Kusoma sura hiyo ni Suna katika Rakaa mbili; ya kwanza na ya pili. Hiyo ndio kauli ya wanachuoni wengi - Allah awarehemu - , na ni kwa mujibu wa Hadithi ya Abukatada-RAA - ambaye amesema kuwa: **"Mtume – SAW - katika Rakaa mbili za mwanzo za Swala ya Adhuhuri, alikuwa anasoma Sura Alfaatiha na sura mbili (nyingine). Alikuwa anarefusha (kusoma) katika Rakaa ya kwanza na anafupisha (kusoma) katika Rakaa ya pili".** Imepokewa na Bukhari (759) na Muslim (451).

Ama Maamuma katika Swala ya kusoma kwa sauti ya wazi (Jaharia), hasomi sura baada ya Alfaatiha, bali anatakiwa kumsikiliza imamu wake.

Ibnikudama - Allah amrehemu- amesema kuwa **"Hatujui kuwepo kwa kutofautiana baina ya wanazuoni juu ya kwamba, ni suna kusoma sura baada ya Sura Alfaatiha katika Rakaa mbili za mwanzo katika kila Swala".** Angalia: Almugh-nii (1/568)..

3 **WAKATI WA KURUKUU NI SUNA KUFANYA YAFUATAYO:**

### 1 Ni Suna mtu kuweka mikono juu ya magoti, kama mwenye kuyashika na vidole kuviachanisha.



Hii ni kutokana na Hadithi ya Abuhumaid – RAA - amesema: **"Mimi nilikuwa mwenye kuhifadhi zaidi Swala ya Mtume –SAW- kuliko nyinyi. Nilimuona Mtume apigapo Takbira anaweka mikono yake mkabala wa mabega yake. Na aliporukuu aliweka mikono yake kwenye magoti, na aliinamisha mgongo wake…".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (828). Na Katika Hadithi ya Abumasoud – Allah amridhie – imekuja kwamba: **"Na (Mtume) aliachanisha baina ya vidole vyake kwenye magoti yake".** Ameipokea Ahmad kwa nambari (17081), Abudaud kwa nambari (863) na Nasai kwa nambari (1038) kwa orodha nzuri ya wapokezi. Hadithi hii ina ushahidi kwenye Hadithi ya Wail bin Hajar iliyopokewa na Ibnikhuzaima (594).

### 2 Ni Suna kwa mwenye kurukuu kunyoosha sawasawa mgongo wake.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhumaid As-saidiy –RAA- kwamba, Mtume wa Allah –SAW-: **"Aliporukuu aliweka vyema mikono yake kwenye magoti yake, na aliinamisha mgongo wake".** Ameipokea Bukhaari (828), Maana ya **"Aliinamisha mgongo wake"**: ni kwamba, aliuinamisha mgongo ukiwa umenyooka bila ya kuufanya umepinda kama upinde. Hakuwa akiuinua sana wala kuuinamisha sana, kwa mujibu wa Hadithi ya Aisha – Allah amridhie iliopo kwa Muslim. Ndani ya Hadithi hiyo imenukuliwa kwamba Aisha, katika kuelezea Rukuu ya Mtume-SAW-, amesema kuwa:

**"Na (Mtume) aliporukuuu alikuwa hainui kichwa chake wala hakiinamishi, lakini alikiweka baina ya hali hizo".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (498).

Maana ya **"hainui kichwa"**: ni kwamba hakuwa akikiinua kikawa juu. Na maana ya **"hakiinamishi"** ni kwamba hakuwa akikiinamisha sana.



### 3 Wakati wa kurukuu, ni Suna kwa mwenye kuswali kutenganisha viwiko vya mikono yake visiguse mbavu zake.

Yaani: Mikono yake asiigusihe kwenye mbavu zake, kwa mujibu wa Hadithi ya Abumasoud –RAA- iliyotangulia, na ambayo ndani yake kuna nukuu kwamba: **"Kisha (Mtume) akarukuu na akaweka mbali mikono yake (isigusane na mbavu zake) na akaweka mikono yake juu ya magoti yake na akatenganisha baina ya vidole vyake"**, na akaendelea kusema: **"Hivi ndivyo nilivyomuona Mtume – SAW - akiswali"**. Imepokewa na Ahmad kwa nambari (17081), Abudaud kwa nambari (863) na Nasai kwa nambari (1038). Angalia: Haashiya (2).

Na **(Kutenganisha mikono isiguse mbavu)** ni kujitanua, lakini kwa sharti kwamba hili halitamkera mtu aliye karibu yake, kwa sababu haitakikani kwa mwenye kuswali kufanya Suna ambayo kwayo atawakera wenzake wanaoswali.

Kuhusu kutenganisha mikono isiguse mbavu amesema Imam Nawawi – Allah amrehemu - kwamba**: "Sifahamu tofauti kwa mwanazuoni yeyote juu ya kwamba ni suna kutenganisha mikono isiguse mbavu katika hali yoyote (ya kukera au ya kutokera)"**. Tirmidhi amenukuu kwa wanazuoni Suna ya kutenganisha mikono isiguse mbavu katika kurukuu na kusujudu katika hali zote. Angalia: Almajmuu (3/410).

### 4 WAKATI WA KURUKUU NI SUNA ALETE NYIRADI ZILOPOKEWA.

Pamoja na kuleta: "**Sub-haana Rabbiyal-adhwiim",** ni Suna kwa mwenye kurukuu alete nyiradi nyingine ambazo zimepokewa katika Rukuu. Na miongoni mwa nyiradi zilizothibiti ni hizi zifuatazo:

1. **"Sub-haanakallaahumma Rabbanaa Wabihamdik, Allaahummaghfirlii", (Kutakasika ni kwako, Ewe Mola wangu, na sifa njema zote ni zako. Ewe Mola wangu, nisamehe".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (794) na Muslim (484) kutoka katika Hadithi ya Aisha, Allah amridhie.

2. **"Subbuuh. Qudduus. Rabbul Malaa-ikati warruuh", (Mwingi wa kutakaswa, Mtakatifu, Mola wa Malaika na Jibrili).** Imepokewa na Muslim kwa nambari (487) kutoka katika Hadithi ya Aisha –RAA-.

3. **"Allaahuma, Laka Rakaatu, Wabika Aamantu, Walaka Aslamtu, Khasha-a Laka Sam-ii Wabaswarii, Wamukh-khii, Wa-adhmii, Wa-aswabii", (Ewe Allah, kwa ajili yako tu nimerukuu, na wewe tu nimekuamini, na kwako tu nimejisalimisha. Usikivu wangu umenyenyekea wako, na uoni wangu na ubongo wangu, na mfupa wangu, na mishipa yangu).** Imepokewa na Muslim kwa nambari (771).

4. **"Sub-haana Dhil Jabaruuti, wal Malakuuti, wal Kibriyaa, wal-adhama", (Ametakasika Mwenye Utawala wa kufanya atakalo, na Ufalme, na Ukubwa, na Utukufu).** Ameipokea Ahmad kwa nambari (23411), na Abudud kwa nambari (873) na Nasai kwa nambari (1050) kutoka katika Hadithi ya Auf bin Maalik-RAA-, na Albaani amesema kuwa ni sahihi (Swahiih Abudaud 4/27).

## 4 KUINUKA KUTOKA KATIKA RUKUU. NDANI YAKE KUNA SUNA NYINGI.

### 1 Kurefusha nguzo Hii.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Thabit Albunani akimnukuu Anas –RAA- kwamba amesema kuwa: **"Hakika, mimi siwezi kuacha kukuswalisheni kama nilivyomuona Mtume –SAW- akituswalisha".** Akasema: **"Anas –RAA-alikuwa anafanya kitu ambacho sikuoneni nyinyi mkikifanya. Ainuapo kichwa chake kutoka katika kurukuu alikuwa anasimama wima mpaka msemaji anaweza kusema kuwa, labda amesahau. Na ainuapo kichwa chake kutoka katika kusujudu anakaa mpaka msemaji anaweza kusema kuwa, labda amesahau".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (821) na Muslim kwa nambari (472).

### 2 Kuleta aina tofauti za matamshi ya "Rabbanaa, Walakal-hamdu" kati ya matamshi yafuatayo:

1. **"Allaahumma Rabbanaa walakal-hamdu", (Ewe Allah Mola wetu, na ni zako wewe tu sifa njema).** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (795) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira- RAA-.

2. "**Allaahumma Rabbanaa Lakal Hamdu", (Ewe Allah Mola wetu, ni zako wewe tu sifa njema)**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (796) na Muslim kwa nambari (404) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhraira –RAA-.

3. **"Rabbanaa walakal Hamdu", (Ewe Mola wetu, na ni zako wewe tu sifa njema).** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (799) na Muslim kwa nambari (411) ikiwa ni sehemu ya Hadith ya Aisha –RAA-.

4. **"Rabbanaa Lakalhamdu", (Ewe Mola wetu, ni zako wewe tu sifa njema).** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (722) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira –RAA-.

Ni Suna mara alete aina hii na mara nyingine alete aina nyingine.

### 3 Baada ya kunyanyuka kutoka katika Rukuu, ni suna kuleta nyiradi zilizothibiti.

Na miongoni mwa nyiradi ambazo sheria imeziweka baada ya kuinuka kutoka katika Rukuu ni hizi zifuatazo:

1. **"Rabbanaa Lakalhamdu, Mil-ussamaawaati Wal-ardhi, Wamil-u Maashi-ita Min Shai-in Baadu, Ahluth-thanaa-i Walmajdi, Ahaqqu Maaqaalal-bdu, Wakullunaa Laka Abdu, Allaahumma Laa Maania Limaa Aatwaita, Walaa Muutwiya Limaa Manaata. Wala Yan-fau Dhaljaddi Minkaljaddu", (Ewe Allah Mola wetu, ni zako wewe tu sifa njema, ujazo wa mbingu na ardhi, na ujazo wa chochote ulichotaka (kuumba) baadaye. Ewe Mwenye kustahiki sifa na utukufu. La kweli kabisa alilolisema mja, na sisi sote kwako ni waja, ni kwamba: Hakuna wa kuzuia ulichotoa, na hakuna wa kutoa ulichozuia. Na wala mali haziwezi kumnufaisha tajiri kwako).** Imepokewa na Muslim kwa nambari (477), na Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abusaid-RAA.

2. **"Alhamdulillahi, Hamdan Kathiiran, Twayyiban, Mubaarakan Fiihi", (Sifa njema ni za Allah, sifa nyingi, nzuri, zenye Baraka).** Amesema Mtume-SAW- juu ya matamshi haya kwamba: **"Nimewaona Malaika kumi na mbili wakishindana nani atakayeiyapeleka juu".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (600) na Bukhari kwa nambari (799).


3. **"Allahumma, Twah-hirnii, Bith-thalji, Walbaradi, Walmaa-ilbaarid, Allahumma, Twah-hirnii, Minadh-dhunuubi, Walkhatwaayaa,**

**Kamaa Yunaqqath-thaubul Abyadhu, Minal Wasakh'', (Ewe Allah Mola wangu, Nisafishe kwa theluji na barafu aa maji baridi. Ewe Allah Mola wangu, Nisafishe niondokane na madhambi na makosa kama vile inavyotakaswa nguo nyeupe iondokane na uchafu).** Imepokewa na Muslim kwa nambari (476).

Na Muislamu akileta nyiradi hizi ataweza kurefusha nguzo hii.

### 5 Kusujudu. Ndani yake kuna Suna yyingi:

**1 Es ist Sunnah, zwischen den Armen und der Körperseite sowie zwischen den Oberschenkeln und dem Bauch einen Abstand zu halten, während man sich niederwirft.**



**Ni Suna kwa mwenye kusujudu kuepusha sehemu ya juu ya mikono yake (kutokea kiwiko mpaka kwenye bega) isiguse mbavu zake. Pia aepushe tumbo lake lisiguse mapaja yake.**

Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Abdallah bin Buhaina-RAA-: **"Kwamba Mtume wa Allah–SAW- pindi akiswali alikuwa anatenganisha kati ya mikono yake mpaka unaonekana weupe wa makwapa yake"**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (390) na Muslim kwa nambari (495). Suna hii pia imethibiti kwa mujibu wa Hadithi ya Maimuna – RAA - aliyenukuliwa kusema kuwa **"Mtume – SAW - alikuwa anaposujudu, kama ndama wa mbuzi au kondoo angetaka kupita kati ya mikono yake angepita"**. Ameipokea Muslim kwa nambari (496). Katika (Hadithi) hii kuna kuonesha uzidishaji wa kiwango katika kutanua mikono. Ilivyo Suna ni kutanua kati ya mikono, madamu katika kufanya hivyo hakuna maudhi kwa aliye pembeni yake, kama ilivyotangulia kuelezwa katika suala la kujitanua katika kurukuu.

Na ni katika Suna pia anaposujudu mwenye kuswali kutenganisha mapaja yake asiyakutanishe pamoja. Na pia asiliegemeze tumbo lake kwenye mapaja yake. Lakini aliweke tumbo lake mbali na mapaja yake, kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhumai –RAA- inayoelezea namna ya swala ya Mtume – SAW- : **"Na akisujudu anatenganisha kati ya maja yake, bila ya kuligusisha tumbo lake na sehemu yoyote ya mapaja yake"**. Imepokewa na Abudaud

kwa nambari (735). Kufanya hao ni Suna kwa maafikiano ya wanazuoni kama Imamu Shaukani na wengine walivyonukuu.

Imamu Shaukani - Allah amrehemu - amesema kuwa: "Na Hadithi inaonesha kuwa ni sheria ya kuachanisha kati ya mapaja katika kusujudu, na kuinua tumbo lisigusane na mapaja. Na hakuna tofauti za Wanazuoni juu ya hilo. Angalia: Nailul Autwaar (2/257).

### 2 Ni Suna kwa mwenye kusujudu aelekeze Kibla ncha za vidole vyake vya miguu.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhumaid – RAA - akinukuliwa kusema kuwa: **"Hakika mimi ndiye niliyehifadhi sana swala ya Mtume – SAW- kuliko nyinyi nyote"** na ndani ya Hadithi hiyo amesema Abuhumaid kuwa: **"Pindi (Mtume) aliposujudu aliweka mikono yake bila ya kuilaza wala kuishikanisha, na alielekeza Kibla ncha za vidole vya miguu yake".** Ameipokea Bukhari kwa nambari (828).

Ama vidole vya mikono wakati wa kusujudu Suna ni kwamba, viwe vimeshikana, na mikono yake aielekeze Kibla, kwa mujibu wa nukuu iliyothibiti kunukuliwa kwa Ibniumar – Allah amuwie radhi yeye na baba yake - katika kitabu cha Muwat-twai cha Imamu Malik. (Angalia: Muwattwai). Pia nukuu hiyo ipo katika kitabu cha Muswannaf cha Ibnu-abii Shayba akimnukuu Hafs bin Aaswim – RAA – kwamba amesema: **"Ni katika Suna katika swala mtu kukunja viganja vyake, na kuviweka pamoja vidole vyake na kuvielekeze Kibla".** Angalia kitabu cha "Muswannaf" cha Ibnu-abii Shayba (1/236). Aidha suala hili lina ushahidi kutoka katika Hadithi ya Waa-il bin Hujri aliyenukuliwa kusema kuwa **"Mtume –SAW- alipokuwa akisujudu aliweka pamoja vidole vyake".** Ameihakiki Haithami (Maj-mauz-zawaaid 2/135).

### 3 Ni Suna kuleta nyiradi zilizopokewa katika kusujud.

Pamoja na kuleta **"Sub-haana Rabbiyal Aalaa"**, (**Ametakasika Mola wangu aliyejuu**), ni Suna kwa mwenye kusujudu kuleta nyiradi nyingine ambazo zimenukuliwa wakati wa kusujudu. Miongoni mwa hizo ni:

1. **"Subhaanakallahumma, Rabbanaa Wabihamdika, Allaahummagh-fir-lii", (Kutakasika ni kwako ewe Allah Mola wetu, na sifa njema**

**zote ni zako. Ewe Allah Mola wangu, nisamehe**). Ameipokea Bukhari kwa nambari (794) na Muslim kwa nambari (484) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Aisha –RAA-.

2. **"Subbuuh, Qudduus, Rabbul Malaa-ikati Warruuh", (Mwingi wa kutakaswa, Mtakatifu, Mola wa Malaika na Jibrili).** Ameipokea Muslim kwa nambari (487) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Aisha-RAA-.

3. **"Allaahumma, Laka Sajadtu, Wabika Aamantu, Walaka Aslamtu, Sajada Waj-hii, Lilladhii Khalaqahuu Waswawwarahuu, Wa Shaqqa Sam-ahuu, Wabaswarahu.Tabaarakallaahu Ahsanulkhaaliqiin", (Ewe Allah Mola wangu, nimekusujudia wewe tu, na nimekuamini wewe tu, na nimejisalimisha kwako tu. Uso wangu umemsujudia aliyeuumba na akautia sura na akauwekea masikio yake na macho yake. Ametukuka Allah Mbora wa waumbaji).** Ameipokea Muslim (771) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Ali- RAA-.

4. "**Allahummagh-fir Lii Dhambii Kullahu, Diqqahuu Wajillahu, Wa-awwaluhuu Wa-aakhirahuu, Wa-alaaniyatahu Wasirrahu", (Ewe Allah Nisamehe dhambi zangu zote, ndogo na kubwa, za mwanzo na za mwisho, za dhahiri na za siri).** Ameipokea Muslim kwa nambari (483) katika Hadithi ya Abuhuraira. –RAA-.

5. **"Allahumma A'uudhu Biridhwaaka Min Sakhatika, Wabimua'afaatika Min 'Uquubatika, Wa-a'udhu Bika Minka, Laa Uh-swii Thanaa-an 'Alayka, Anta Kamaa Athnaita 'Aalaa Nafsika", (Ewe Allah, hakika mimi najilinda kwa radhi zako dhidi ya hasira zako, na kwa msamaha wako dhidi ya adhabu yako, na najilinda kwako unihifadhi. Mimi siwezi kuzikariri sifa zako zote. Wewe ni kama ulivyojisifu mwenyewe**). Hii ni sehemu kutoka katika Hadithi ya Aisha –RAA-. Ni suna mtu alete nyiradi hizi katika kusujudu kwake kadiri atakavyoweza, na alete tofauti tofauti. Na ni jambo linalojulikana kwamba iliyo wajibu katika Rukuu ni kusema "**Sub-haana Rabbiyal 'Adhwiim**", (**Ametakasika Mola wangu aliye Mtukufu)** mara moja, na inayozidi ni Suna. Na vile vile katika kusujudu, iliyo wajibu ni kusema **"Sub-haana Rabbiyal A'alaa"**, (**Ametakasika Mola wangu aliye juu**), mara moja. Ama mara ya pili na ya tatu hizo ni Suna.



### 4 Ni Suna kuomba sana Dua katika kusujudu.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniabas – RAA – iliyopo kwa Muslim: **“Na Ama (katika) kusujudu, jitahidini katika kuomba, kwa sababu ni yakini kuwa mtajibiwa”**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (479).

## 6 Miongoni mwa Suna katika kuketi kati ya Sijida mbili.



### 1 Ni katika Suna kwa mwenye kuswali atandaze mguu wake wa kushoto na kuukalia, na asimamishe (unyayo wa mguu wake) wa kulia.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhumaid Assaaidiy –RAA- iliyohusishwa na Mtume. Ndani yake kuna: **“….(Mtume) Alipoketi katika rakaa mbili, alikalia mguu wake wa kushoto na kusimamisha wa kulia”.** Ameipokea Bukhari kwa nambari (828).

### 2 Kurefusha nguzo hii.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Thabit Albunani – RAA - ambayo imetangulia.

### 3 Ni Suna kwa mwenye kutaka kusimama kwenda Rakaa yoyote; ya pili au ya nne, akae kidogo kabla hajasimama.

Na mkao huu unaitwa **“Jilsatul-Istiraaha”** (**Kikao Cha Kupumzika**), na hakina uradi maalumu.

Na kuthibiti kwa mkao huu kumekuja katika Hadithi tatu. Miongoni mwa Hadithi hizo ni hizi zifuatazo:

Hadithi ya Malik bin Alhuwairith – RAA – aliyenukuliwa kusema kwamba: **“Alimuona Mtume akiswali. Alipokuwa katika Rakaa za Swala yake ya Witiri, hakusimama wima hadi alipokaa chini sawasawa”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (823). Na Malik bin Alhuwairith – RAA - ndiye aliyenakili maneno ya Mtume –SAW – yasemayo kwamba: **“Swalini kama mlivyoniona nikiswali”**. Ameipokea Bukhari (631).

Kuna kutofautiana (baina ya wanazuoni) juu ya Suna ya (**Kikao Cha Kupumzika**). Iliyo sawa ni kwamba, kikao hicho kwa jumla ni Suna, kwa

mujibu wa Hadithi ya Malik – RAA -. Na miononi mwa wanazuoni walioipa nguvu kauli kwamba kikao hicho, kwa jumla, ni Suna ni Nawawiy, Shaukaniy, Ibnibaz, Albaniy – Allah awarehemu - na Kamati ya Kukudumu ya Utafiti wa Kielimu a Fat-wa. (Angalia: Fat-wa na Makala Mbalimbali 11/99) na Fat-wa za Kamati Ya Kudumu (6/445-446).

Imamu Nawawiy – Allah amrehemu – amesema kuwa: **"Na hii ndio sawa ambayo zimethibiti ndani yake Hadithi sahihi".** Angalia: Almajmuui (3/441).

## 7 MIONGONI MWA SUNA KATIKA TASHAHUDI (ATTAHIYYAATU).

### 1 Ni Suna mwenye kuswali atandaze mguu wake wa kushoto, na asimamishe mguu wa kulia.



Na hii namna anaifanya mwenye kuswali baada ya kuwa anaswali rakaa ya pili pamoja na rukuu yake, na sijida yake na kisimamo chake, na kuketi kwake; ni sawa sawa kwamba yupo katika kuswali swala ya rakaa nne au tatu au mbili. Rakaa yeyote ya pili katika kuketi katika Tashahudi yake kikao kinakuwa katika namna hii, kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhumaid Assaaidy – RAA – iliyohusishwa na Mtume. Ndani ya Hadithi hiyo kuna (nukuu hii): **"… (Mtume) Alipoketi katika Rakaa mbili alikalia mguu wake wa kushoto na kuusimamisha wima (mguu) wa kulia"**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (828). Na pia ni kwa mujibu wa Hadithi ya Aisha – RAA – aliyenukuliwa kusema kuwa: **"..Na (Mtume) katika kila Rakaa mbili alikuwa akisoma At-Tahiyyaatu, na alikuwa akitandaza mguu wake wa kushoto na kuusimamisha wa kulia".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (498).

Ama Tashahudi ya mwisho katika swala yenye Rakaa nne, na tatu utakuja ubainifu wa namna yake.

### 2 Suna ni kufanya sampuli tofauti tofauti katika kuweka mikono wakati wa Tashahudi.

Uwekaji wa viganja wakati wa Tashahudi una namna mbili:

**Ya Kwanza:** Ni kuweke mikono juu ya mapaja.

**Namna Ya Pili:** Ni kuweka mikono juu ya magoti, na hilo ni kwa (kiganja cha) mkono wake wa kushoto kulifinika goti lake la kushoto. Ama mkono wa

kulia atatoa ishara kwa mkono huo kama itakavyokuja ubainifu wake. Ama mkono wa kushoto ni wenye kukunjuliwa wakati wote.





Kwa mujibu wa Hadithi ya Umar –RAA – aliyenukuliw kusema kuwa: **"Alikuwa (Mtume – SAW -) anapoketi katika swala anaweka kiganja chake cha kulia juu ya paja lake la kulia, na anakunja vidole vyake vyote, na anaashiria kwa kidole chake cha shahada, na anaweka kiganja chake cha kushoto kwenye paja lake la kushoto".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (580). Na katika mapokezi mengine kuna nukuu kwamba: **"Anashikanisha kiganja chake cha kushoto na goti lake (la kushoto)".** Ameipokea Muslim kwa namba (579).

**3 Suna ni kufanya sampuli tafauti katika namna za kuweka vidole wakati wa Tashahudi.**





Uwekaji vidole wakati wa Tashahudi una namna mbili:

**Namna ya Kwanza:** Ni mtu akunje vidole vyote vya kiganja chake cha kulia, na atoe ishara kwa kidole chake cha shahada, na mkono wa kushoto unakuwa umekunjuliwa.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniumar – RAA - iliyotangulia: **"...alikunja vidole vyake vyote na aliashiria kwa kidole chake ambacho kinafuatia kidole Gumba...".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (580).

**Namna ya Pili:** Atengeneze kwa nambari hamsini na tatu (kwa Kiarabu) kwa kukunja kidole cha mwisho na kinachofuata, na afanye duara kwa kukutanisha dole gumba na kidole cha kati, na aashirie kwa kidole cha shahada. Ama mkono wa kushoto vidole viwe vimekunjuliwa.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniumar –RAA- iliyotangulia katika riwaya isemayo kuwa: **"Alikuwa (Mtume –SAW-) anapoketi katika Tashahudi anaweka mkono wake wa kushoto juu ya goti lake la kushoto, na anaweka mkono wake wa kulia juu ya goti lake la kulia, na anakunja kwa nambari hamsini na tatu (kwa Kiarabu), na anaashiria kwa kidole cha shahada".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (850).

### 4 Suna ni mwenye kuswali alete aina tofauti tofauti za matamshi ya Tashahudi.

Asome matamshi haya mara hii, na mara nyingine asome matamshi mengine. Miongoni mwa matamshi yaliyopokewa ni haya yafuatayo:

1. "At-Tahiyyaatu Lillaah. Wasw-Swalawaatu, Watw-Twayyibaatu. As-Salaamu 'Alayka Ayyuhan-Nabiyyu Wa-Rahmatullaahi Wa Barakaatuh. As-Salaamu 'Alaynaa Wa 'Alaa 'Ibaadi-Llaahi-Sw-Swaalihiin. Ash-Hadu An-Laa Ilaaha Illallaah, Wa-Ash-Hadu Anna Muhammadan 'Abduhuu Wa Rasuuluh". **(Maamkizi mema ni ya Allaah, na Swala na maneno mema yote. Amani iwe juu yako Ewe Mtume na Rehema za Allah na Baraka Zake. Amani iwe juu yetu na juu ya waja wema wa Allah, Ninashuhudia (ninakiri) kwamba hapana mwabudiwa wa haki isipokuwa Allah tu, na ninashuhudia kwamba Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake)**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1202), na Muslim kwa nambari (402) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Ibnimasoud- RAA-.
2. **"At-Tahiyyaatul Mubaarakaatu, Asw-Swalawaatu, Atw-Twayyibaatu Lillaah. As-Salaamu 'Alayka Ayyuhan-Nabiyyu..." (Maamkizi yenye baraka na Swala njema ni ya Allah. Amani iwe juu yako Ewe Mtume...).** Ameipokea Muslim kwa nambari (403) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Ibniabbas –RAA-. Kisha anakamilisha kama ilivyotangulia kuelezwa.

3. **"At-Tahiyyaatul Attwaypbaatu, Atw-Twayyibaatu Asw-Swalawaatu, lillaah. As-Salaamu 'Alayka Ayyuhan-Nabiyyu ...", (Maamkizi mema, Swala ni ya Allah, Amani iwe juu yako Ewe Mtume .....").** Ameipokea Muslim kwa nambari (404) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abumousa-RAA-. Kisha anakamilisha kama ilivyotangulia kuelezwa..

## 5 Suna ni mwenye kuswali akae katika Tashahudi ya mwisho mkao wa Tawaruki (kukalia tako) katika Swala zenye Rakaa tatu na nne.

Kusudio lake ni mtu akalie tako lake katika Tashahudi ya mwisho, iwapo swala ni yenye rakaa tatu au nne. Anakalia tako lake la kushoto. Na Tawaruki imethibiti kwa njia zaidi ya moja. Kwa hivyo, inapendekezwa kukaa Tawaruki kwa sampuli tofauti tofauti.:

Miongoni mwa aina za Tawaruki zilizopokewa ni:



1. Atandaze chini mguu wake wa kushoto na kuutoa utokeze upande wa kulia, na asimamishe mguu wa kulia na kuyaweka makalio yake ardhini.

Aina hii ameipokea Bukhari - Allah amrehemu (828) – akimnukuu Abuhumaid Assaaidiy.



2. Kutandaza chini miguu yake yote, na kuitoa itokeze upande wa kulia, na anaweka makalio yake ardhini.

Aina hii ameipokea Abudaud kwa nambari (731), Ibnuhibbaan kwa nambari (1867) na Baihaqiy (2/128), ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhumaid Assaaidiy-RAA-, na Shekh Albaaniy- Allah amrehemu amesema kuwa nukuu hizo ni sahihi. Tunamuomba Allah awarehemu wote.

Na ijulikane kuwa, mkao wa Tawaruki, katika kauli iliyo sahihi, sio kwamba ni katika kila Tashahudi ya mwisho. Lakini ni katika Tashahudi ya mwisho katika swala zenye Rakaa tatu na nne tu, na sio swala zenye Rakaa mbili.

### 6 Suna ni mwenye kuswali alete sampuli tofauti tofauti za matamshi ya kuswalia Mtume – SAW -.

Yamepokewa matamshi mbalimbali ya kumswalia Mtume –SAW-. Suna ni kuleta sampuli tofauti tofauti kati ya matamshi hayo. Na miongoni mwa yaliyopokewa ni:

1. **"Allaahumma Swalli 'Alaa Muhammad, Wa 'Alaa Aali Muhammad, Kamaa Swallayta 'Alaa Ibraahiym, Wa Alaa Aali Ibraahiim, Innaka Hamiidun Majiid. Allaahumma Baarik 'Alaa Muhammad Wa 'Alaa Aali Muhammad, Kamaa Baarakta 'Alaa Ibraahiym, Wa Alaa Aali Ibraahiim, Innaka Hamiydun Majiyd".,** (**Ewe Allah Mola wangu, mswalie Muhammad na familia ya Muhammad, kama ulivyomswalia Ibrahimu na familia ya Ibrahimu. Hakika, wewe ni mhimidiwa, mtukufu. Ewe Allah Mola wangu, mbariki Muhammad na familia ya Muhammad, kama ulivyombariki Ibrahimu na famila ya Ibrahimu. Ulimwenguni Kote, Hakika, Wewe ni Mhimidiwa, Mtukufu**). Imepokewa na Bukhari (3370) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Kaabi bin Ujra, Allah amuwiye radhi.

2. **"Allaahumma Swalli 'Alaa Muhammad, Wa 'Alaa Aali Muhammad, Kamaa Swallayta 'Alaa Aali Ibraahiym. Wa Baarik 'Alaa Muhammad, Wa 'Alaa Aali Muhammad, Kamaa Baarakta 'Alaa Aali Ibraahiym, Fil- 'Aalamiyn, Innaka Hamiydun Majiyd", (Ewe Allah! Mswalie Muhammad na familia ya Muhammad, Kama Ulivyoswalia familia ya Ibrahimu. Na mbariki Muhammad na familia ya Muhammad kama Ulivyobariki familia ya Ibrahimu katika walimwenguni. Hakika, Wewe ni Mhimidiwa, Mtukufu".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (405) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abumasoud Al-answaariy-RAA-.

3. **"Allaahumma Swalli 'Alaa Muhammad, Wa 'Alaa Azwaajihii, Wadhur-riyyatihii, Kamaa Swallayta 'Alaa Aali Ibraahiym. Wabaarik 'Alaa Muhammad Wa 'Alaa Azwaajihii, Wadhur-riyyatihi, Kamaa Baarakta 'Alaa Aali Ibraahiym, Innaka Hamiydun Majiyd", (Ewe Allah! Mswalie Muhammad na wake zake, Na kizazi chake, kama ulivyoswalia familia ya Ibrahimu, Na mbariki Muhammad na wake zake, na kizazi chake, Kama ulivyoibariki familia ya Ibrahimu. Hakika, Wewe ni Mhimidiwa, Mtukufu".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (3369) na Muslim kwa nambari (407) ikiwa ni sehemu ya Hdithi ya Abuhumaid Assaidiy- RAA-.

## 7 Ni Suna Mmwenye kuswali aombe kinga kwa Allah dhidi ya vitu vine kabla hajatoa Salamu.

Na hiyo ndio kauli ya wanazuoni wengi, Allah awarehemu, kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira –RAA- aliyenukuliwa kusema kwamba, Mtume –SAW- amesema kuwa: **"Mmoja wenu anapomaliza Tashahud ya mwisho, aombe kinga kwa Allah dhidi ya mambo manne. Adhabu ya Jahanamu na adhabu ya kaburini, na dhidi ya mitihani ya uhai na mauti, na dhidi ya uovu wa Masia Laghai). "Allaahumma Innii A'uwdhubika Min 'Adhaabi Jahannam, Wamin 'Adhaabil Qabri, Wamin Fitnatil-mahyaa Walmamaati, Wamin Sharri Fitnatil-Masiyhid-dajjaal", (Ewe Allah, naomba kinga kwako dhidi ya adhabu ya Jahanamu na adhabu ya kaburini, na dhidi ya mitihani ya uhai na mauti, na dhidi ya uovu wa Masia Laghai).** Imepokewa na Muslim kwa nambari (588) na Bukhari kwa nambari (832).

Kuna dua nyingine katika Suna zilizopokewa. Ni Suna kwa mwenye kuswali azilete dua hizo kwa namna tofauti tofauti, kabla hajatoa Salamu. Na miongoni mwa dua zilizothibiti ni hizi zifuatazo:

1. **"Allaahumma Innii A'udhu Bika Minal Ma-thami Walmagh-rami", (Ewe Allah, hakika mimi naomba kinga unilinde dhidi ya dhambi na madeni).** Ameipokea Bukhari kwa nambari (832) na Muslim kwa nambari (589).
2. **"Allaahumma Inniy As-Alukal-Janna, Wa A'uwdhu Bika Minan-Naar". (Ewe Allah, hakika mimi nakuomba Pepo na nakuomba unikinge dhidi ya moto).** Imepokewa na Abudaudi kwa nambari (792) na Shekh Albaniy amesema kuwa ni sahihi (Swahih Abudaud 3/377).
3. **"Allaahumma Inniy Dhwalamtu Nafsiy Dhwulman Kathiyra, Walaa Yaghfirudh-Dhunuuba Illaa Anta. Faghfirliy Maghfiratan-Min 'Indika, Warhamniy Innaka Antal-Ghafuurur-Rahiym". (Ewe Allah, Hakika nimedhulumu nafsi yangu dhuluma nyingi, wala hakuna wa kusamehe dhambi isipokuwa wewe tu. Basi, nighufirie maghfirah kutoka kwako, na nirehemu. Hakika, wewe ni Mwingi wa kughufiria, Mwenye kurehemu).** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6326) na Muslim kwa nambari (2705).
4. **"Allaahumma A'inniy 'Alaa Dhikrika, Wa Shukrika, Wa Husni 'Ibaadatika". (Ewe Allaah, nisaidie juu ya kukutaja, na kukushukuru, na kukuabudu kwa uzuri".** Imepokewa na Ahmad kwa nambari (22119), Abudud kwa nambari (1522) na Nasai kwa nambari (1304). Na Shekh Albaaniy amesema kuwa ni sahihi (Sahiihul Jaami'u 2/1320).

5 **"Allahumma Innii A'udhu Bika Minal Bukhli, Wa-auudhu Bika Minal Jubni, Wa-auudhu Bika An- Uradda Ilaa Ardhalil-umri, Wa-auudhu Bika Min Fitnatid-dun-yaa, Wa Auudhu Bika Min Adhaabilqabri", (Ewe Allah, naomba kinga kwako dhidi ya ubahili, na naomba kinga kwako dhidi ya woga, na naomba kinga kwako dhidi ya kurudishwa kwenye umri dhalili, na naomba kinga kwako dhidi ya mtihani wa dunia na naomba kinga kwako dhidi ya adhabu ya kaburini).** Ameipokea Bukhari kwa nambari (6370).

6 **"Allahuma Haasibnii Hisaaban Yasiiraa", (Ewe Mola wangu, nihesabu mimi hesabu nyepesi).** Ameipokea Ahmad kwa nambari (24215), na Shekh Albaaniy amesema kuwa ni sahihi. (Tahqiiqu Mishakaatilmaswaabiih 3/1544).

Kisha anatoa Salamu akigeuka katika kutoa kwake Salamu. Kugeuka kwake katika Swala ni Suna, na kuzidisha kiwango katika kugeuka ni Suna pia, kwa sababu Mtume – SAW -alikuwa anageuka mpaka mtu aliye nyuma yake anaona weupe wa shavu lake –SAW-. Imenukuliwa kwa Saad bin Abiwaqqaas – RAA – kwamba, amesema kuwa: **"Nilikuwa namuona Mtume wa Allah – SAW - akitoa Salamu kuliani mwake na kushotoni kwake, mpaka naona weupe wa shavu lake"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari: (582).

## 8 NYIRADI AMBAZO SHERIA IMEZIWEKA BAADA YA KUTOA SALAMU KATIKA SWALA ZA FARADHI NI SUNA.

Imam Nawawiy - Allah amrehemu – amesema kuwa: **"Wanazuoni wote wameafikiana juu ya kwamba nyiradi baada ya Swala ni jambo la kupendekezwa".** Angalia: Al-adhkaar (Ukurasa 66).

Na inapendekezwa kuzisoma nyiradi hizi kwa sauti ya juu, kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniabbass – RAA – aliyenukuliwa kusema kwamba: **"Kusoma uradi kwa sauti ya juu wakati watu wanapomaliza kuswali swala ya faradhi ni jambo lilikuwako wakati wa Mtume – SAW -".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (841) na Muslim kwa nambari (583).

### -Na nyiradi zenyewe ni hizi:

1 Amuombe Allah msamaha kwa kusema "**Astaghfiru Allaah"** mara tatu. Kisha aseme: **"Allahumma Antassalaam, Waminkassalaam, Tabaarakta Yaa Dhaljalaali Wal-ikraam". (Ewe Allah, wewe ndiye amani, na amani hutoka kwako. Umebarikika ewe Mwenye utukufu na ukarimu).** Imepokewa na Muslim (591) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Thauban – RAA –.

2 **"Laa Ilaaha Illallaah. Wahdahuu Laa Shariika Lah. Lahulmulku, Walahulhamdu. Wahuwa 'Alaa Kullishay-in Qadiir. Laa Hawla Walaa Quwwata Illaa Billaah. Laa Ilaaha Illallaah. Walaa Naabudu Illaa Iyyaah. Lahunniima. Walahulfadh-lu. Walahuth-thanaa-ulhasan. Laa Ilaaha Illallaah. Mukhliswiina Lahuddiin. Walaw Karihalkafiruun". (Hakuna apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah tu, Peke Yake, hana mshirika. Ni wake yeye tu ufalme, na ni zake yeye tu sifa njema, na Yeye ni Muweza wa kila kitu. Hakuna uwezo (wa kuacha dhambi) wala nguvu (ya kufanya ibada) isipokuwa kwa (msaada wa) Allah tu. Hakuna apasae kuabudiwa isipokuwa Allah tu, na hatuabudu ila Yeye tu. Ni zake yeye tu neema, na ni zake yeye tu fadhila, na ni zake yeye tu sifa nzuri. Hakuna apasae kuabudiwa isipokuwa Allah tu, tukimtakasia yeye tu dini, japo makafiri watachukia**). Ameipokea Muslim (596).

3 **"Laa Ilaaha Illaallaah. Wahdahuu Laa Sharikka Lah. Lahul-Mulku. Walahul-hamdu. Wahuwa 'Alaa Kulli Shay-in Qadiir. Allaahumma Laa Maani'a Limaa A'twayta, Wa Laa Mu'twiya Limaa Manaata, Walaa Yanfa'u Dhal-Jaddi Minkal-Jaddu", (Hapana Mwabudiwa wa haki Ila Allah, Peke Yake, Hana Mshirika. Ufalme ni wake yeye tu, na kuhimidiwa ni kwake yeye tu, Naye ni Muweza wa kila kitu. Ewe Allah, hakuna wa kuzuia ulichokitoa, na wala hakuna wa kutoa ulichokizuia, na wala mwenye utajiri hatamnufaisha utajiri (wake) kwako).** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (844) na Muslim kwa nambari (593).

4 **Kisha Aseme Tasbihi Iliyonukuliwa, nayo ina matamshi mengi:**

**La kwanza:** {**Sub-haana Allaah** mara (33), **Alhamdulillaah** mara (33), **Allahu Akbar** mara (33) kisha anatimiza mara ya mia na: **Laa ilaaha illallah, Wahdahuu Laa Shariika Lah, Lahulmulku, Walahulhamdu. Wahuwa 'Alaa Kullishay-in Qadiir}.**



Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira -RAA- akinukuliwa kuwa, amesema Mtume wa Allah –SAW- kwamba: **"Atakayesabihi (Sub-haana Allaah) kila baada ya Swala mara thalathini na tatu, na akahimidi (AlhamduliLLaah) mara thalathini na tatu, na akaleta Takbira (Allaahu Akbar) mara thalathini na tatu, kwa kukamilisha mara ya mia kwa kusema: "Laa ilaaha illallaah, Wahdahuu laa shariika Lah, Lahul-Mulku, walahulhamdu wahuwa 'alaa**

**kullishay-in Qadiir" [Hapana mwabudiwa wa haki ila Allah tu, Peke yake, Hana mshirika, ufalme wote ni wake yeye tu, na Himdi zote ni zake yeye tu, Naye ni Muweza wa kila kitu] atasamehewa makosa yake japo ni (mengi) mfano wa povu la bahari"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (597).

**La Pili:** {**Sub-haanallah mara (33), Alhamdulillah mara (33),** Allahu Akbar mara (34)}, kwa mujibu wa Hadithi ya Kaabi bin Ujrah – RAA – aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume –SAW- amesema kwamba: **"Ni vifuatishi (ambavyo) hatoki patupu mwenye kuvisema baada ya kila swala ya faradhi: Tasbihi (Sub-haanallah) thalathini na tatu,**

Na Tahamidi (Alhamdu lillaah) thalathini na tatu na Takbira (Allaahu Akbar) thalathini na nne". Imepokewa na Muslim (596).

**La tatu: {Sub-haanallah mara (25), Alhamdulillaah mara (25), Allaahu Akbar mara (25), Laa ilaaha illallaah mara (25)}.**

Na tamshi hili limepokewa na Tirmidhiy kwa nambari (3413) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abdallah bin Zaid –RAA-, na Shekh Albaaniy amesema kuwa ni sahihi (Tahqiiq Mishkaatul Maswaabiih 1/ 307).

**La Nne: {Sub-haana Allah, mara (10), Alhamdu lillaah mara (10), Allaahu Akbar mara (10)}.**

Na tamshi hili limepokewa na Tirmidhiy kwa nambari (3410) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abdallah bin Amri –RAA-, na Shekh Albaaniy amesema kuwa ni sahihi (Tahqiiq Mishkaatul Maswaabiih 2/743).

Na imetangulia kutajwa kanuni katika ibada ambazo zimekuja kwa njia tafauti tafauti kwamba, hufanywa mara kwa namna hii na mara nyingine kwa namna ile.

Na Suna ni kuwa Tasbihi (uradi) ifanywe kwa vidole, kwa mujibu wa Hadithi aliyoipokea Imam Ahmad na Tirmidhiy kwamba, Mtume –SAW-amesema kuwa: "**Leteni Tasbihi (uradi) na hesabuni kwa vidole, kwa sababu vidole vitaulizwa na vitatakiwa kutamka**". Imepokewa na Ahmad kwa nambari (27089), na Tirmidhiy kwa nambari (3486), na Shekh Albaaniy amesema kuwa ni Hadithi Hasan.

### 5 Kusoma Aya Kursiy.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abu-umama- RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume –SAW- amesema kwamba: "**Mwenye kusoma Aya Kursiy mwisho wa kila Swala ya faradhi, hakuna kitakachomzuia kuingia Peponi isipokuwa mauti tu**". Imepokewa na Nasaiy katika Assunan Alkubraa kwa

nambari (9928). Wanachuoni wafuatao wamesema kuwa ni Hadithi sahihi: Almundhiriy katika kitabu chake cha Attarghiib Wattarhiibu kwa nambari (2373), Ibnuabdilhadi (Almuharrir 1/198) na Ibnulqayyim (Zaadulmaad 1/303).


6 **Kusoma Muawidhataini:** {Qul A'uudhu Birabbilfalaq} na {Qul A'uudhu Birabbinnaas}.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Utba bin Amir –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa: **"Aliniamrisha Mtume wa Allah-SAW- kusoma Muawidhati baada ya kila Swala."** Ameipokea Abudud kwa nambari (1525). Amesema Shekh Albaniy kuwa: **"Nasema: Isnadi yake (Orodha ya wapokezi wake) ni sahihi".** Pia Ibnuhiban na Ibnukhuzaima wamesema kuwa ni Hadithi sahihi (Sahiih Abiidaauud (5/254).

Hizi ni katika Suna za swala ambazo inapendekezwa kwa mwenye kuswali kuzileta. Bado tuko katika wakati wa Alfajiri. Tumeeleza hayo yaliyopita kutokana na kuhitaji kwetu kuyatumia katika kila sehemu ya swala. Allah ndiye Mjuzi zaidi.


## 9 NI KATIKA SUNA MTU KUKETI BAADA YA SWALA YA ALFAJIRI KATIKA SEHEMU ALIPOSWALI MPAKA JUA LICHOMOZE.

Imenukuliwa kwa Jabir bin Samura –RAA- kwamba: **"Mtume – SAW - pindi akimaliza kuswali Alfajiri alikuwa akiketi kwenye sehemu yake aliposwali mpaka jua lichomoze vizuri".** Ameipokea Muslim kwa nambari (670). Jua kuchomoza vizuri ni liinuke juu.



◆ Amesema Mtume-SAW-: "Watu Saba Allah Atawafunika Katika Kivuli Chake, Siku Ambayo Hakutokuwa Na Kivuli Ila Kivuli Chake...(Na Akataja Miongoni Mwao).. Mwanamme Ambaye Moyo Wake Umesehelea [Au Umeambatana] Katika Misikiti"

## Nyiradi za Asubuhi.



Wakati wa nyiradi za asubuhi unaanza kutokea kuchomoza kwa alfajiri. Muadhini anapoadhini kwa ajili ya swala ya alfajiri, unaanza wakati wa nyiradi za asubuhi. Hakuna shaka kwamba nyiradi ni kinga madhubuti kwa mja hapa duniani na ni hazina yake kubwa akhera.

### Nyiradi za asubuhi na jioni ni:

1. **Mwenye kusema: "Laa ilaaha illallaah, Wahdahuu laa shariyka Lah, Lahul-mulku, walahul-hamdu, wahuwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr", (Hapana mwabudiwa wa haki ila Allah tu, Peke Yake, Hana mshirika. Ni wake yeye tu ufalme, na ni zake yeye tu Himdi, na Yeye ni Muweza wa kila kitu" Atakayesema hayo mara kumi anapoamka ataandikiwa mema mia moja, na atafutiwa maovu mia moja, na atapata thawabu sawa na za kumwacha huru mtumwa, na atapewa kinga kwayo kwa mchana huo hadi jioni. Na atakayesema hayo wakati wa jioni atapata mfano wa hivyo''.** Ameipokea Ahmad kwa nambari (8719), na Shekh Ibnibaz, Allah amrehemu, amesema kuwa Isnadi yake (Orodha ya wapokezi wake) ni nzuri.

2 **"Amsaynaa wa-amsal-mulku lillaah, walhamdu lillaah. Laa ilaaha illa-llaah, Wahdahuu laa shariyka Lah. Allahumma Innii as-aluka min khayri haadhihil-layla, wakhayri maa fiihaa. Wa-auudhu bika Min-sharrihaa washarri maa fiihaa. Allaahumma innii a'uudhu bika minalkasali, walharami, wasuu-ilkibar, wafitnatid-dun-yaa, wa-adhaabilqabri.** (**Tupo jioni na ufalme ni wa Allah, na himdi ni za Allah Peke yake, hana mshirika. Ewe Mola wangu, nakuomba kheri zilizomo katika usiku wa leo na kheri za vilivyomo humo. Na ninakuomba kinga dhidi ya shari yake na shari ya vilivyomo humo. Ewe Mola wangu, naomba kinga kwako dhidi ya uvivu, na ukongwe na uzee mbaya, na mtihani wa dunia na adhabu ya kaburini".** Na anapoamka asubuhi aseme kama hivyo: **"Asbahnaa wa-asbahal-mulku lillaah, walhamdu lillaah. Laa ilaaha illa-llaah, Wahdahuu laa shariyka Lah. Allahumma Innii as-aluka min khayri haadhalyaum, wakhayri maa baadahuu. Wa-auudhu bika Min-sharrihii Min-sharri maa fii Haadhalyaum Washarrimaa baadah. Allaahumma innii a'uudhu bika minalkasali, walharami, wasuu-ilkibar, wafitnatid-dun-yaa, wa-adhaabilqabri.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2723).

3 Bwana wa Istighfari (Maneno yenye uzito mkubwa katika kumuomba Allah msamaha): **"Allahumma Anta Rabbii, Laa Ilaaha illaaa Anta, Khalaqtanii Wa-Anaa 'Abduka, WaAnaa 'Alaa 'Ahdika Wawa'adika Mastata'tu, A'udhu Bika Min-Sharri Maa Swana'atu, Abu'u Laka Bini'imatika Alayya, Wa-abuu-u Laka Bidhanbii, Fagh'fir Lii Fa-innahuu Laa Yaghfirudh-dhhunuuba illaa Anta". (**Bwana wa Istighfari ni kusema: **"Ewe Allaah, Wewe ni Mola wangu, hakuna wa kustahiki kuabudiwa ila wewe tu. Umeniumba, na mimi ni mja Wako. Nami niko katika ahadi yako na agano lako kiasi cha uwezo wangu. Naomba kinga kwako dhidi ya ubaya wa niliyoyafanya. Nakiri neema zako kwangu, na nakiri kukukosea, basi naomba unisamehe, kwa sababu hakuna wa kusamehe dhambi ila wewe tu.** Amesema Mtume kuwa**: (Atakayesema maneno haya mchana akiwa na yakini nayo, na akafa mchana wake huo kabla ya kuingia jioni, basi atakuwa miongoni mwa watu wa Peponi. Na atakayesema maneno haya usiku akiwa na yakini nayo na akafa kabla hajafika asubuhi, basi yeye ni miongoni mwa watu wa Peponi)".** Ameipokea Bukhaari, kwa nambari (6306).

4 Anapopambazukiwa mmoja wenu aseme: **"Allahumma Bika Aswbahnaa, Wabika Amsaynaa, Wabika Nahyaa, Wabika Namuut, Waileyikan-nushuur",** (**Ewe Allah, kwa sababu yako tumeingia katika asubuhi, na kwa ajili yako tuliingia jioni, na kwa sababu**

**yako tumekuwa hai, na kwa sababu yako tutakufa, na kwako tu tutafufuliwa**). Na ikifika jioni aseme: **"Allahumma Bika Amsaynaa, Wabika Aswbahnaa Wabika Nahyaa Wabika Namuut, Wailayikal Maswiir",** (**Ewe Allah, kwa sababu yako tumefika jioni, na kwa sababu yako tumefika asubuhi, na kwa sababu yako tuko hai na kwa sababu yako tutakufa na marejeo ni kwako tu).** Amepokea Hadithi hii Abudaud kwa nambari (5068), Tirmidhiy kwa nambari (3391), Nasaai kwa nambari (9836) {Assunanul Kubraa}, Ibnimaja kwa nambari (3868). Shekh Ibnibaz - Allah amrehemu - amesema kuwa orodha (Isnadi) ya wapokezi wake ni sahihi.

5 **"Allahumma, Faatwirassamaawaati Wal-ardhwi, 'Aalimalghaybi Wash-shahaada, Laa ilaaha illaa An'ta, Rabba Kulli Shay-in Wamaliikah, A'uudhu Bika Min-sharri Nafsii, Wamin-sharri Shaitwaani Wa Shirkihii, Wa-an-aqtarifa 'Alaa Nafsii Suu-an, au Ajurrahuu ilaa Muslim",** (**Ewe Allaah, Mjuzi wa Ghaibu (mambo yasiyo onekana kwa macho) na yanayo onekana, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila wewe tu, Mola wa kila kitu na Mmiliki wake. Nakuomba kinga dhidi uovu wangu mwenyewe na uovu wa shetani na shirki yake na kujichumia uovu mimi mwenyewe au kumfanyia ubaya Muislamu**). Amesema Mtume –SAW-: **"Yaseme hayo asubuhi na jioni, na unapolala".** Imepokewa na Imam Ahmad kwa nambari (6597), Abudaud kwa nambari (5079), Tirmidhiy kwa nambari (3529), Nasaai kwa nambari (7699). Shekh Ibnibaz - Allah amrehemu - amesema kuwa orodha (Isnadi) ya wapokezi wake ni sahihi

6 **"Hakuna mja yeyote anayesema mara tatu kila siku asubuhi na kila siku usiku: "Bismillahilladhii Laa Yadhurru Ma'asmihii Shay-un Fil-ardhwi Walaa Fissamaa-i Wahuwassamiiul 'Aliimu**", **(Kwa Jina La Allah ambaye hakuna chochote kinachodhuru pamoja na jina lake si ardhini wala mbinguni. Na yeye ni Mwenye kusikia, Mjuzi**), **isipokuwa kwamba hakuna chochote kitakachomdhuru".** Hadithi hii ameipokea Imamu Ahmad kwa nambari (10179), Imamu Ibnimaja kwa nambari (3869). Shekh Ibnibaz - Allah amrehema kuwa, amesema Tirmidhiy kwamba **"Ni Hadithi sahihi"** na ni hivyo alivyosema - Allahu amrehemu.

7 **"Hakuna mja yeyote Muisilamu ambaye husema mara tatu pindi anapopambazukiwa na pindi anapofikiwa na jioni: "Radhiitu billaahi Rabban, Wabil-islaami Diinan, Wabimuhammaddin – Swallallaahu**

**'Alayi Wasallama Nabiyyan**" (**Nimeridhia kuwa Allah ndiye Mola, na Uislamu ndio dini, na Muhammad SAW ndiye Mtume**), **ila inakuwa haki kwa Allah kumuridhisha mja huyo Siku ya Qiyama".** Ameipokea Imaam Ahmad kwa nambari (18967), Tirmidhiy kwa nambari (3389) na Ibnimaja kwa nambari (3870). Shekh Ibnibaz - Allah amrehemu - amesema kuwa orodha (Isnadi) ya wapokezi wake ni Hasan (inakubalika).

8 **"Allaahumma inniy as-alukal'aafiyah fid-dun-yaa wal-aakhirah. Allaahumma inni as-alukal'afwa wal'aafiyata fii Diiniy wadun-yaaya, wa-ahliy, wamaaliy. Allaahumma-stur 'awraatiy, wa-aamin rau'aatiy. Allaahumma-hfadhwniy min bayni-yadayya, wamin-khalfiy, wa'an-yamiyniy, wa'an-shimaaliy, wamin-fawqiy, wa-a'uuwdhu bi'adhwamatika an-ughtaala min-tahtiy", (Ewe Allaah, hakika nakuomba uzima (utimamu) duniani na Akhera. Ewe Allah, hakika nakuomba msamaha na utimamu katika Dini yangu na dunia yangu, na familia yangu, na mali yangu. Ewe Allah, nisitiri aibu zangu na itulize hofu yangu. Ewe Allah, nihifadhi mbele yangu na nyuma yangu na kulia kwangu na kushoto kwangu na juu yangu. Na naomba kinga kwa utukufu wako nisivamiwe {na adui, maafa, majanga au misiba}).** Ameipokea Imamu Ahmad kwa nambari (4785), Abudaudi kwa nambari (5074), Nasai kwa nambari (10401) na Ibnimaja kwa nambari (3871). Imam Hakim amesema kuwa ni Hadithi sahihi.

9 **"A'uudhu Bikalimaatillaahit-taam-maati Min-Sharri Maakhalaq"**, **(Naomba hifadhi kwa maneno ya Allah yaliyotimia anilinde dhidi ya shari ya alivyoviumba**). Ameipokea Ahmad kwa nambari (7898), na Tirmidhiy kwa nambari (3437) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira – RAA -. Shekh Ibnibaz amesema kuwa Isnadi (orodha) ya wapokezi wake ni Hasan (inakubalika), Allah amrehemu.

10 "Mtume – SAW - akipambazukiwa alikuwa anasema: **"Aswbahnaa 'Alaa Fitwratil-islaam, Wakalimatil-ikhlaasw, Wadiini Nabiyyinaa Muhammadin – Swallaallahu 'Alayhi Wasallam -, Wamillati Abiinaa Ibraahim, Haniifan, Wamaa Kaana Minalmushrikiin," (Tumeingia asubuhi tukiwa katika maumbile ya Kiislamu na neno la ikhlasi na dini ya Mtume wetu Muhammad Swalla Allahu 'Alayi Wasallam, na mila (dini) ya baba yetu Ibrahimu iliyo sawa na hakuwa miongoni mwa mwenye kumshirikisha Allah).** Imepokewa na Ahmad kwa nambari (15367, 21144). Na akifikiwa na jioni anasema: **"Amsaynaa 'Alaa Fitwratil Islaami…".** Shekh Ibnibaz - Allah amrehemu - amesema kuwa ni Hadithi sahihi.

Yote yaliyotangulia kutajwa yako katika kitabu cha Sheikh Ibnibaz - Allah amrehemu - kinachoitwa (Tuh'fatul-akhyaar Bibayaanijumlatin-naafia Mimmaa Warada Filkitaabi Was-sun-na Minal-ad-i'yati Wal-adhkaar), Fasili ya "Nyiradi za Asubuhi na Jioni".

11 **"Yaa Hayyu Yaa Qayyuum, Birahamtika Astaghiith, Aslih-lii Sha-'nii Kullah, Walaa Takilnii ilaa Nafsii Twarfat 'Ain", (Ewe Uliye hai, Uliyesimama kwa dhati yako, kwa rehema zako ninakuomba msaada. Nitengenezee mambo yangu yote, wala Usiniachie mambo yangu mwenyewe (pasi na kunisaidia) hata kwa muda (mdogo kama muda) wa kupepesa jicho).** Imepokewa na Nasai kwa nambari (10405) na Bazaar (2/282). Ibnihajar na Albaniy wamesema kuwa ni Hadithi Hasan. (Angalia: Nataaijul Afkaar, ukurasa 177, na Silsilatul Ahaadiithisswahiiha 1/449).

12 **"Hasbiyallaahu, Laa ilaaha illa huwa, 'Alayhi Tawakkaltu Wahuwa Rabbul 'Arshil 'Adhwiim. Mwenye kuyasema mara saba, Allah atamtosheleza na (kumuondolea) jambo linalomhuzunisha", (Allah tu ananitosha. Hakuna apasaye kuabudiwa ila Yeye tu. Yeye nimemtegemea, na Yeye ni Mola wa Arshi Tukufu).** Ameipokea Abudaud kwa nambari (5081) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abudardai – RAA -. Kauli yenye nguvu zaidi ni kwamba Hadithi hii ni "Mawquuf" (Imeishia kuhusishwa na Swahaba tu). Wapokezi wake ni waaminifu, na ina hukumu ya kuhusishwa na Mtume, kama alivyosema Shekh Albaaniy. (Angalia: Silsila 11/449).

## TATU: WAKATI WA DHUHA.



Wakati wa Dhuha ni Suna Mja aswali Swala ya Dhuha.

### Na ushahidi wake ni:

1. Hadithi ya Abuhuraira – RAA – amesema aliyenukuliwa kusema kuwa: **“Ameniusia rafiki yangu (Swallallaahu ‘alayhi wasallam) mambo matatu: kufunga swaumu siku tatu katika kila mwezi, rakaa mbili za Dhuhaa na niswali Witiri kabla ya kulala”.** Na pia Mtume – SAW -alimuusia mambo hayo Abudardai – RAA – (Muslim 722). na Abudhari – RAA – (Nasai – Assunan Alkubraa). Shekh Albani amesema kuwa Hadithi hii ni sahihi.

2. Hadithi ya Abudhari – RAA - akimnukuu Mtume –SAW- kwamba, amesema kuwa: **“Panapopambazuka, inakuwepo sadaka katika kila kiungo cha mmoja wenu. Kila Tasbihi (Sub-haanallaah = Ametakasika Allah) ni Sadaka, na kila Tahmidi (Alhamdu Lillaah = Sifa njema ni za Allah) ni sadaka, na kila Tahalili (Laa ilaaha illallaah = Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu) ni sadaka, na kila Takbira (Allaahu Akbar = Allah ni Mkubwa zaidi) ni sadaka,**

**na kuamrisha mema ni sadaka, na kukataza maovu ni sadaka. Na yote hayo yanatoshelezwa na rakaa mbili anazoswali mtu wakati wa Dhuha".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (720).

Viungo**:** Ni sehemu ya mwili iliyojigawa.

Na umekuja ufafanuzi katika Sahihi Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Aisha – RAA – kwamba kila mwanadamu ameumbwa akiwa na viungo mia tatu na sitini, na kwamba mwenye kuleta idadi hii ya sadaka, atakuwa anatembea siku hiyo akiwa ameepushwa na moto wa Jahanamu.

## Wakati wake:

Wakati wa swala ya Dhuha unaanza pale jua linapoinuka kwa kadiri ya kiwango cha mkuki; kwa maana ya baada ya kutoka wakati uliokatazwa kuswali.

Na unakwisha: Muda mfupi kabla ya wakati wa Zawali (jua kupinduka kuacha usawa wa kati); kwa maana kabla ya kuingia wakati wa swala ya Adhuhuri kwa takribani dakika kumi.

Na hoja ya hili ni Hadithi ya Amri bin Absa – RAA -: "**Swali swala ya asubuhi, kisha acha kuswali wakati jua linachomoza mpaka liinuke... Kisha swali, kwa sababu swala hiyo inashuhudiwa na inahudhuriwa, mpaka kivuli kitoshane na mkuki. Kisha acha kuswali wakati huo, kwa sababu wakati huo Jahanamu huwa inakokwa (inakolezwa)".** Ameipokea Muslim kwa nambari (832).

## Wakati wake bora zaidi:

Ni katika wakati wake wa mwisho ambao ni pale kwato za ndama wa Ngamia zinapo ungua kwa jua kuwa kalili.

Na hoja yake ni Hadithi ya Zaid bin Arqam – RAA - pindi kwato za ndama wa ngamia zinapo ungua kwa sababu ya jua kuwa kali na kuchoma, kwamba Mtume – SAW – amesema (kuwa huo ndio muda wa): **Swala ya wenye kutii".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (748).

Ibnibaz - Allah amrehemu - amesema kuwa: "Maana ya kuchomo: ni wakati joto la jua linapozidi. Na Ndama: Ni watoto wa ngamia. Swala hii ni katika zile swala ambazo kuziswali mwisho wa wakati ni bora zaidi. Angalia (Fataawaa Islaamiyya 1/515).

### Idadi ya Rakaa zake:

Uchache wa swala ya Dhuha ni Rakaa mbili, kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira – RAA – iliopo katika Sahiih mbili (Sahiih Bukhaariy na Sahiih Mulim) akinukuliwa kusema kuwa: **“Aliniusia rafiki yangu mambo matatu”** na akataja katika hayo **“na rakaa mbili za Dhuha”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1981), na Muslim kwa nambari (721).

Ama wingi wa swala ya Dhuha, lililo sahihi ni kwamba haina ukomo wa wingi wake, tofauti na wale walioiwekea ukomo wa rakaa nane. Kwa hiyo, mtu ana hiyari ya kuzidisha zaidi ya rakaa nane hadi kiasi ambacho Allah – SWT – atakachomuwezesha, kwa mujibu wa Hadithi ya Aisha – RAA – aliyenukuliwa kusema kuwa: **“Mtume – SAW - alikuwa anaswali Dhuha rakaa nne na anazidisha mpaka Allah atakavyo”.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (719).



Kutokana Na Utukufu Wa Swala Ya Adhuhaa Ulikuwa Wasiya Wa Mtume-SAW- Kwa Maswahaba Wake

## NNE: WAKATI WA ADHUHURI.



Ndani yake kuna mambo mengi:

### Jambo la Kwanza: Swala za Suna za Kabla na za Baada.

Imetangulia katika maelezo juu ya Suna za Ratibu (swala za suna zilizowekewa muda maalumu) kwamba sheria imeweka Suna kuswali rakaa nne kabla ya Adhuhuri, na rakaa mbili baada ya Adhuhuri, kama inavyolitolea ushahidi hilo Hadithi ya Aisha, Ummuhabiba na Ibniumar, Allah awawie radhi wote.

### Jambo la Pili: Ni katika Suna kurefusha Rakaa ya kwanza ya Swala ya Adhuhuri.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abusaid Alkhudriy – RAA – aliyenukuliwa kusema kuwa: **"Hakika, ilikuwa swala ya Adhuhuri inakimiwa, kisha mwenye kwenda anakwenda mpaka Baqii na kukidhi haja yake, kisha anatawadha na kurudi na ilhali Mtume – SAW - akiwa bado yupo katika**

**Rakaa ya kwanza, kwa namna alivyokuwa akiirefusha”**. Ameipokea Muslim kwa nambari (454).

Kutokana na hayo, ni katika Suna kwa imamu kurefusha rakaa ya kwanza ya swala ya Adhuhuri, na vilevile mwenye kuswali peke yake, na pia mwanamke katika swala yake ya Adhuhuri. Na hii ni katika Sunnah ambazo zimetoweka (zimekufa). Tunaomba Allah – aliyetukuka - atuwezeshe kutekeleza Suna kwa namna iliyo kamilifu, na kuiwekea maanani.

### Jambo la nne: Wakati wa joto kali. Ni Suna kuchelewesha Swala yua Adhuhri Mpaka joto lipungue.

Na ushahidi wa hilo ni:
Hadithi ya Abuhuraira – RAA - ambayo imehusishwa na Mtume kwamba: **“Jua linapokuwa kali sana ngojeni hadi lipoe ndipo mswali, kwa sababu ukali wa joto unatokana na mtokoto wa Jahanamu”.**

**Kutokota kwa Jahanam:** Ni kuchemka kwake na kusambaa kwa miali na sauti yake. Ameipokea Bukhari kwa nambari (533,534), na Muslim kwa nambari (615).

Shekhe wetu Ibniuthaimini - Allah amrehemu – amesema kuwa: **“Tukikadiria, kwa mfano, kuwa jua katika siku za joto linapinduka saa sita, na Alasiri inakuwa takribani saa kumi na nusu, basi Ibraad (kuliacha joto lipoe) itakuwa hadi takribani saa kumi”**. Angalia: Almumti’u (2/104).

Na Ibradi ni kwa watu wote; anayeswali kwa jamaa na mwenye kuswali peke yake, katika kauli iliyo sahihi. Na hii ndiyo kauli aliyoichagua Shekhe wetu Ibniuthaimini - Allah amrehemu. Kwa kauli hiyo, wanawake pia wanaingia, na maana hiyo, ni Suna kwao kusubiri hadi joto lipoe wakati wa jua kali, kwa mujibu maana jumla ya Hadithi ya Abuhuraira –RAA-.



Amesema Mtume-SAW-: “Swala Ni Nuru”, Ni Nuru Kwako Duniani Na Akhera

## TANO: WAKATI WA ALASIRI.



Yametangulia maelezo juu ya Swala za Sunah za muda maalumu na ufafanuzi wake, na kwamba kabla ya swala ya Alasiri hakuna swala yoyote ya Suna.

Shekhe wa Uislamu Ibnitaimia - Allah amrehemu –amesema kuwa: **"Na ama kabla ya Alasiri, hakuna yeyote aliyesema kuwa Mtume – SAW- alikuwa akiswali kabla ya Alasiri isipokuwa ndani ya kauli hiyo kuna udhaifu, bali makosa".** Angalia: Alfataawa (23/125).

Iliyo sawa ni kwamba - na Allah ndiye anayejua zaidi: - hakuna Suna yoyote iliyopangwa kuswaliwa kabla ya Alasiri.  Suala linabaki wazi. Anayetaka kuswali rakaa mbili au zaidi ya hizo ikiwa ni katika mlango kujikurubisha kwa Allah kusikofungwa, kama vile anavyoswali katika nyakati nyingine zisizokuwa zile nyakati ambazo imekatazwa kuswali, basi anaweza kufanya hivyo. Ama kwamba kuna swala yoyote yenye kufungamanishwa kabla ya Alasir, hapana.

## Nyiradi za asubuhi aa jioni.

Wakati wa nyiradi za asubuhi na jioni unaanza wakati gani?

## Wakati wa nyiradi za asubuhi:

Huanza tangu kuchomoza kwa alfajiri ya kweli ambayo ndio wakati wa swala ya Alfaijri. Muadhini anapoadhini kwa ajili ya swala ya Alfajiri, hapo unakuwa umeanza wakati wa nyiradi za asubuhi. Na hii ndio kauli ya wanachuoni wote, Allah awarehem. Na sio vibaya kuzisoma nyiradi hizo baada ya jua kuchomoza, hasa inapokuwa kuziacha kwake ilikuwa ni kutokana na udhuru, na pia ni kwa sababu muda uliopo baada ya jua kuchomoza unaitwa (Asubuhi), na kwa kufanya hivyo atapata fadhila za uradi na baraka zake. Hii ni bora zaidi kuliko kuziacha kabisa, na kughafilika katika sehemu ya siku yake iliyobaki.

## Wakati wa nyiradi za jioni:

Lililo wazi zaidi – na Allah ndiye ajuae zaidi – ni kwamba: Muda huu unaanza baada ya (swala ya) Alasiri mpaka jua linapotua. Na sio vibaya kuzisoma nyiradi hizo baada ya jua kuzama, hasa inapokuwa kuziacha kwake ilikuwa ni kutokana na udhuru, na pia ni kwa sababu muda uliopo baada ya jua kuzama unaitwa (Jioni), na kwa kufanya hivyo atapata fadhila za uradi na baraka zake. Hii ni bora zaidi kuliko kuziacha kabisa, na kughafilika katika sehemu ya siku yake iliyobaki.

Shekhe wetu Ibniuthaimini - Allah amrehemu – aliulizwa kwamba: “**Ni upi wakati wa nyiradi za jioni? Na ni upi wakati wake bora? Na je, zinalipwa zinaposahauliwa?**

**Jawabu:** Alhamdulillah, jioni ni pana; tangu baada ya swala ya Alasiri mpaka wakati wa Ishaa. Muda wote huu unaitwa (jioni), na ni sawa kama atasoma uradi katika wakati wa mwanzo au wa mwisho, isipokuwa tu ule uradi ambao imethibiti kuhusishwa na wakati wa usiku, kama vile Aya Kursi ambayo mtu anataisoma katika usiku wake. Uradi unaokuwa umefungamanishwa na usiku unasomwa usiku, na uradi uliofungamanishwa na mchana unasomwa mchana. Ama kulipa uradi unaposahau, nataraji kuwa mtu akiusoma atapatiwa ujira juu yake”. Angalia katika Fat-wa za Sheikh Uthaimini katika jarida la Adda’awa, namba (174), la tarehe 07/02/1421AH, Ukurasa (36). Angalia pia: Sherehe yake ya kitabu cha Riyaadhus-swalihiin (2/1533), mlango wa “Nyiradi za asubuhi na jioni”.

## SITA: WAKATI WA MAGHARIBI



**Ndani yake kuna mambo mengi:**

- **Jambo la kwanza: Ni katika Suna kuwazuia watoto (wasitoke majumbani) mwanzo wa magharibi.**

- **Jambo la pili: Ni katika Suna kufunga milango mwanzo wa magharibi, na kutaja jina la Allah –aliyetukuka.**

Na katika kufanya taratibu hizi mbili kuna kinga dhidi ya Mashetani na Majini. Katika kuwazuia watoto (wasitoke nje) mwanzo wa wakati wa magharibi ni kuwalinda dhidi ya mashetani ambao husambaa katika wakati huo, na katika kufunga milango wakati huo na kutaja jina la Allah-aliyetukuka – kuna kinga pia dhidi ya mashetani na majini. Watoto wengi na nyumba nyingi mashetani wamejipenyeza kwao na kuingia katika wakati huu. Ni ukubwa ulioje wa ulinzi wa dini ya Kiislamu kwa watoto wetu na nyumba zetu!



Na hoja ya hili ni:

Hadithi ya Jabir bin Abdallah - RAA – aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume – SAW – amesema kwamba: **“Liingiapo giza la usiku wazuieni watoto wenu kutokatoka (majumbani), kwa sababu mashetani wanasambaa nyakati hizo. Likishapita saa moja ya usiku waacheni. Na fungeni milangeni na tajeni jina la Allah (mnapoifunga), kwa sababu shetani hafungui mlango uliofungwa”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (3304) na Muslim kwa nambari (2012). Giza la usiku ni: Kuingia kwa usiku baada ya jua kuzama.

Kuzuia watoto na kufunga milango mwanzo wa magharibi, ni katika hali ya kupendekezwa. Angalia: Fat-wa za Kamati ya Kudumu (26/317).

**Jambo la tatu:** Kuswali Rakaa mbili kabla ya Magharibi.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abdallah ibn Mughaffal Almuzani – RAA - akimnukuu Mtume – SAW – kwamba, amesema kuwa: **“Swalini kabla ya swala ya Magharibi”**-, na mara ya tatu akasema: “**kwa anayetaka**, kwa kuchelea watu wasiifanye kuwa ni Suna”.  Imepokewa na Bukhari kwa nambari (1183).

**Na vilevile ni suna kuswali Rakaa mbili kati ya kila Adhana na Ikama.**

Ni sawa kwamba hizi Rakaa mbili ni zile za Ratibu (za kabla na za baada), kama suna ya Alfajiri na Adhuhuri au la. Kwa kuswali kwake Suna Ratibu, kwa hakika inatosheleza na hakuna haja ya kuswali Rakaa hizi mbili (za kati ya kila Adhana na Ikama). Mtu kama amekaa msikitini kisha Muadhini akaadhini kwa ajili ya swala ya Alasiri au Ishaa, ni Suna asimame na kuswali Rakaa mbili.

**Na ushahidi wa hili ni:**

Hadithi ya Abdallah bin Mughaffal Almuzani – RAA – aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume – SAW – amesema kwamba: **“Kati ya kila Adhana mbili** (Adhana na Ikama) **kuna Swala”.** Mtume alisema hayo mara tatu. Alisema katika mara ya tatu: **“Kwa anayetaka”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (624) na Muslim (838).

Hakuna shaka kwamba, Rakaa mbili za kabla ya Magharibi au kati ya Adhana na Ikama hazijatiliwa mkazo sana kama zilivyotiliwa mkazo Suna za Ratibu. Kwa hakika, huwa zinaachwa mara nyingine. Ndio akasema Mtume – SAW – katika mara ya tatu kwamba: **“Kwa anayetaka”**; kwa kuchelea watu kuifanya kuwa ni Suna (iliyotiliwa mkazo sana).

**Jambo la nne:** Ni Makuruhu (haipendezi) kulala kabla ya Isha.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abubarza Al-aslami – RAA - aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume **“Alikuwa anapendelea kuchelewesha Isha**. Amesema: **Na alikuwa anachukia kulala kabla ya Isha, na mazungumzo baada yake”.** Ameipokea Bukhari namba (599), na Muslim kwa namba (647).

Na sababu ya kuchukia kulala wakati wa Magharibi; yaani kabla ya Isha ni kwa sababu kulala kwake kunaweza kuwa sababu ya kupitwa na Swala ya Isha.



Tobah Mchana Na Usiku Ni Funguo Kwa Mja Na Ndani Yake Kuna Kusahihisha Mwendo Wake Wa Kumwendea Allah Aliyetukuka, Amesema Mtume-SAW-: “Hakika Allah Anakunjua Mkono Wake Usiku Ili Apokee Tawbah Ya Mkoseaji Mchana. Na Anakunjua Mkono Wake Mchana Ili Apokee Tawbah Ya Mkoseaji Usiku”

## SABA: WAKATI WA ISHA



Kuna mambo mengi:

**Jambo la kwanza: <u>Ni Makuruhu kuzungumza na kukaa (kijiweni au maskani) baada yake.</u>**

Kwa mujibu Hadithi ya Abubarza Al-aslami – RAA –iliyotangulia. Na ndani ya Hadithi hiyo kuna nukuu kwamba: **“Na (Mtume) alikuwa anachukia kulala kabla yake, na mazungumzo baada yake**”. Ikiwa mazungumzo yake yana ulazima, hakuna makuruhu kufanya hivyo.

Na sababu ya kuchukizwa (kulala kabla ya Isha na mazungumze baada yake) - na Allah ndiye Mjuzi zaidi – ni kwamba, atachelewa kulala na kwa hiyo, inahofiwa kuwa anaweza kupitwa na swala ya Asubuhi akaiswali nje ya wa wakati wake au nje ya mwanzo wa wake au kukosa kisimamo cha usiku kwa ambaye ni kawaida yake kufanya hivyo.

**Jambo la pili:** Jambo lililo bora kwa swala ya Isha ni kucheleweshwa, kama katika kufanya hivyo hakuna uzito kwa maamuma.

Na hoja ya hilo ni:

Hadithi ya Aisha –RAA - aliyenukuliwa kusema kuwa: "Mtume – SAW - alikesha usiku mmoja mpaka sehemu kubwa ya usiku ikapita, na mpaka watu msikitini wakawa wamelala. Kisha akatoka, akaswali (swala ya Isha) na kusema **"Hakika, huu ndio wakati wake, lau kama si kuwaonea tabu watu wangu"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (638).

Kwa mujibu wa hayo, iliyo Suna kwa mwanake ni kuchelewesha Ishaa ikiwa, katika kufanya hivyo, hakuna tabu kwake. Ni hivyo hivyo mwanaume pindi anapokuwa hafungamani na swala ya jamaa; mfano akiwa safarini n.k.

**Ni Katika Suna kusoma Sura Ikhlaas kila usiku.**

Imenukuliwa kwa Abbdardai naye akimnukulu Mtume –SAW- kwamba amesema kuwa: **"Je, anashindwa mmoja wenu kusoma theluthi ya Kur'ani katika usiku mmoja? (Swahaba) Wakasema: Anawezaje mtu kusoma theluthi ya Kur'ani? Mtume akasema: "Qul-huallaahu Ahad" inalingana na theluthi ya Kur'ani"**. Imepokewa na Muslim (811) na Bukhari (5015) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abusaid -RAA-.



## SUNA ZA KULALA

### Kulala, na ndani yake kuna Suna nyingi:

### 1 Kufunga milango wakati wa kulala.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Jabiri –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, amesema Mtume wa Allah kwamba –: **“Zimeni taa mnapolala, na mfunge milango, na mfunike mitungi ya maji, na mfunike chakula na vinywaji”.** Imesimuliwa na Bukhari kwa nambari: (5624) na Muslim kwa nambari (2012).

Na sababu ya amri ya kufunga milango: Ni kuzuia mashetani kuingia, kama ilivyotangulia katika Hadithi nyingine ya Jabiri - RAA:

**“Na fungeni milango, na tajeni jina la Allah, kwa sababu mashetani hayafungui mlango uliofungwa.”** Imesimuliwa na Bukhari kwa nambari (5623), na Muslim kwa nambari (2012).

### 2 Kuzima moto kabla ya kulala.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Jabiri –RAA- iliyotangulia. Katika Hadithi hiyo kuna nukuu kwamba: **“Zimeni taa mnapolala”.**

Pia ni kwa mujibu wa Hadithi ya Umar –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, amesema Mtume –SAW- kwamba: **“Msiache moto katika nyumba zenu mnapolala”.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2015).

Na kinafananishwa na moto kitu chochote kinachoweza kuwa sababu ya kuleta moto kwa watu katika nyumba. Inatakiwa ichukuliwe tahadhari, kwa mfano, kwenye vitu ambavyo vinaweza kuleta athari katika vifaa vya umeme kwa kuwepo karibu navyo, na hivyo, ikawa sababu ya moto kuwaka. Hii ni kwakuwa sababu ni moja, na moto ni adui kama alivyosema Mtume –SAW-.


Kwa msingi huu, lau kama mtu aliyelala ataona kuwa yuko salama na moto huu na kwamba hautamdhuru kwa sababu karibu yake hakuna kitu kinachoweza kusababisha kusambaa kwake, hakuna ubaya katika hali hiyo kuuacha moto huo, kwa sababu **“Hukmu inazunguka pamoja na sababu yake kwa kuwepo kwake na kutokuwepo kwake”.**

### 3 KUTAWADHA KABLA YA KULALA.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Baraa bin Aazib - RAA- kwamba, Mtume –SAW- amesema kuwa: **“Utakapofika kitandani mwako [na kutaka kulala] tawadha kama unavyotawadha kwa ajili ya Swala kisha lalia ubavu wako wa kulia kisha sema: “Allaahumma innii, Aslamtu Nafsii ilayka, wawajjahtu waj-hiya ilayka, wafawwadhtu Amrii ilayka, Wa-alja’tu Dhahrii ilayka, Ragh-batan Warahbatan ilayka, Aamantu Bikitaabikalladhii Anzalta, Wa-binabiyyikalladhii Arsalta”, Ewe Allah, nimeisalimisha nafsi yangu kwako, na nimeuelekeza uso wangu kwako, nimeyakabidhi mambo yangu kwako, na nimekutegemea wewe (nisimame) kama mwanadamu anavyotegemea mgongo wake (ili asimame), kwa kutaraji rehema zako na kuogopa adhabu yako. Nimeamini kitabu chako ulichoteremsha na Mtume wako uliyemtuma”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (247) na Muslim kwa nambari (2710).

### 4 KUKUNG’UTA KITANDA (TANDIKO) KABLA YA KUKILALIA.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira –RAA- aliyenukuliwa kuasema kuwa, Mtume –SAW- amesema kwamba: **“Pindi mmoja wenu atakapo elekea kitandani kwake (kwa ajili ya kulala), basi akung`ute kitanda chake kwa kutumia sehemu ya ndani ya ncha ya shuka yake na ataje jina la Allah, kwa sababu hajui nini kilikaa (hapo kitandani) badala yake baada ya yeye kuamka. Kisha asome dua hii: “Bismikallaahumma Wa-dhwaatu Jan-bii…= Kwa jina lako, Ewe Mola wangu, nimeweka ubavu wangu…”.**Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6320) na Muslim kwa nambari (2714).

Sehemu ya ndani ya ncha ya nguo: Ni ile ncha ya nguo ambayo inafuatia mwili.

Kutokana na maelezo yaliyotangulia, inabainika kwamba Suna ni mtu kukung'uta kitanda chake kwa sehemu ya ndani ya ncha ya nguo yake, na kwamba kukung'uta ni mara tatu, na ataje jina la Allah wakati wa kukung'uta.

Jambo bora zaidi ni kwamba kukung'uta kufanyike kwa kutumia sehemu ya ndani ya nguo. Miongoni mwa wanazuoni ambao wamesema mtu akung'ute kwa kitu chochote, na kwamba la muhimu zaidi ni kukung'uta kitanda. Miongoni mwa wanazuoni hao ni Shekh Ibnijabrin - Allah amrehemu – aliposema kuwa: **"Na sio sharti kutumia sehemu ya ndani ya ncha ya nguo. Kama mtu atakung'uta tandiko lote au kama atakung'uta kwa kutumia kitambaa na mfano wa hivyo, kusudio litapatikana".** Angalia: Fat-wa yake kwa nambari (2693).

## 5 KULALIA UBAVU WA KULIA.

## 6 KUWEKA MKONO WAKE WA KULIA CHINI YA SHAVU LA KULIA.



Na ushahidi wa Suna hizi mbili: Ni Hadithi ya Baraa bin Azib – RAA – kwamba, Mtume wa Allah –SAW- amesema kuwa: **"Utakapofika kitandani mwako [na kutaka kulala] tawadha kama unavyotawadha kwa ajili ya Swala, kisha lalia ubavu wako wa kulia, kisha sema: "Allaahumma innii Aslamtu Nafsiy ilayka, Wa Fawwadhwtu Amriy Ilayka, Wa Wajjahtu Waj-Hiya Ilayka, Wa-Alja-Tu Dhwahriy Ilayka, Raghbatan Warahbatan Ilayka, Laa Malja-a Walaa Manjaa Minka illaa ilayka, Aamantu Bikitaabikal-Ladhiy Anzalta WabiNabiyyikal-Lladhiy Arsalta", (Ewe Allaah, Nimeisalimisha nafsi yangu kwako, na nimekuachia wewe mambo yangu, na nimeuelekeza kwako uso wangu, na nimeutegemeza mgongo wangu kwako (Nakutegemea wewe katika kufanikiwa kwangu kama mwili wa mwanadamu unavyoutegemea mgongo katika kusimama kwake), kwa matajarajio (ya kupata rehema zako) na kwa kukuogopa (adhabu yako). Hakuna sehemu ya kukimbilia wala ya kujiokoa ila kwako tu. Nimeamini kitabu chako ulichokiteremsha na Nabii wako uliyemtuma".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (247).

Na Hadithi ya Hudhaifa -RAA- ambaye amenukulikwa kusema kuwa: **"Mtume – SAW – alipokuwa akilala usiku alikuwa anaweka mkono wake chini ya shavu lake."** Imesimuliwa na Bukhari kwa nambari (6314).

## 7 KUSOMA NYIRADI ZA KULALIA.



Kulala kuna nyiradi kutoka katika Qur'ani a Suna.

### 1 KUTOKA KATIKA QUR'AN.

#### 1 Kusoma Aya Kursi

Ni katika Suna kusoma Aaya Kursi wakati wa kulala, kwa sababu ndani yake kuna kinga dhidi ya Shetani mpaka kunapopambazuka.

**Na ushahidi wa** hili ni: Kisa cha Abuhuraira –RAA- na mtu aliyekuwa akiiba Zaka. Amesema Abu Hurara –RAA- kuwa: **"Na Mtume – SAW- akaniambia kuwa: "Amefanya nini mateka wako (uliyemkamata kwa wizi) usiku wa jana?". Nikamwambia: "Alidai kuwa atanifundisha maneno ambayo Allah ataninufaisha kwayo, na kwa hiyo, nikamwachia". Mtume akasema: "Ni yapi maneno hayo?". Nikamwambia: Ameniambia: "Utakapoingia kitandani kwako (kwa ajili ya kulala), soma Aya Kursi (Allaahu Laa ilaaha illaa Huwal-Hayyul-Qayyuum) kuanzia mwanzo wake hadi uikamilishe", na (Mwizi) aliendelea kuniambia kuwa: "(Kwa kusoma Aya hiyo) Utaendelea kuwa katika ulizi wa Allah na kamwe Shetani hatakusogelea mpaka asubuhi". Na (Swahaba) walikuwa na ari sana ya kujali mambo ya kheri. Hapo, Mtume – SAW - akaniambia: "Amekwambia ukweli japokuwa yeye ni muongo, Je, unamjua ewe Abuhurara uliyekuwa ukizungumza naye tangu siku tatu?" Nikamwambia: "Hapana, ewe Mtume wa Allah -SAW-. Mtume akasema: "Huyo ni Shetani".** Imesimuliwa na Bukhari kwa nambari (2311) na ameiunganisha Imamu Nasai katika Assunan Alkubraa kwa nambari (10795).

#### 2 KUSOMA AYA MBILI ZA MWISHO KATIKA SURA BAQARA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abumasoud Al- Answari- RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa: Mtume wa Allah –SAW- amesema: **"Atakayesoma usiku aya hizi mbili za mwisho wa Sura Baqara zitamtosheleza"**. Imesimuliwa na Bukhari kwa nambari (4008) na Muslim kwa nambari (807). Aya mbili za mwisho za Sura Baqara si katika nyiradi za kulalia, katika namna ya umaalumu, lakini ni uradi unaosomwa usiku. Yule ambaye hakuzisoma usiku, na akakumbuka wakati wa kulala kwake, basi azisome wakati huo.

Zimekuwepo tafsiri tafauti za maana ya (**zitamtosheleza**):

Imesemwa kwamba, zitamtosheleza kisimamo cha usiku, na pia imesemwa kwamba, zitamtosheleza na kumkinga dhidi ya Shetani.

Pia imesemwa kuwa zitamtosheleza na kumkinga dhidi ya majanga. Inawezekana kuwa yote hayo yamekesudiwa, kama alivyosema Imamu Nawawi –Allah amrehemu-. Angalia: Sharhun-nawawiy Alaa Muslim, Hadithi namba (808), Mlango juu ya fadhila za Sura Faatiha na aya za mwisho za Surat Baqarah ...).

3. Kusoma Sura Ikhlaas (Qul Huwallaahu Ahad), na Mu'awwidhatain (Qul A'uudhu Birabbilfalaq na Qul 'Auudhu Birabbin-naas), na kupulizia sura zote hizo katika viganja vya mkono, kisha kupangusa mwili mara tatu kwa kutumia viganja hivyo.

**Na ushahidi wa hili ni:**

Hadithi ya Aisha – RAA - aliyenukuliwa kusema kuwa: **"Mtume wa Allah – SAW - alipokuwa anapanda kitandani kila usiku, alikuwa anakusanya viganja vyake, kisha anapulizia humo na kusoma: (Qul Huwallaahu Ahad), na (Qul Auudhu Birabbilfalaq) na (Qul Auudhu Birabbin-naas). Kisha anajipangusa (anajipaka) sehemu anayoweza kuifikia ya mwili wake akianzia kichwani mwake, usoni na sehemu ya mbele ya mwili wake. Alikuwa anafanya hivyo mara tatu".** Imesimuliwa na Bukhari (5017).

**Inapatikana faida kutoka katika Hadithi iliyotangulia** kwamba, Mtume – SAW - alikuwa anaitekeleza Suna hii kila usiku, kwa mujibu wa kauli ya Aisha – RAA - : **"Kila usiku"** na kwamba mwenye kutaka kuitekeleza Suna hii, akusanye pamoja viganja vyake, kisha apulizie ndani yake kwa Sura Ikhlaas (Qul Huwallaahu Ahad), na Mu'awwidhatain (Qul A'uudhu Birabbilfalaq na Qul 'Auudhu Birabbin-naas). Kisha apake sehemu atakayoweza kuifikia ya mwili wake, akianzia kichwani mwake na usoni mwake. Afanye hivyo mara tatu.

### 4. KUSOMA SURA KAAFIRUUN.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Urwa bin Naufal akimnukuu baba yake- RAA – kwamba amesema kuwa, Mtume –SAW - alimwambia Naufal: **"Soma {Qul Yaa Ayyuhal Kaafiruun}. Kisha lala ukimaliza kuisoma, kwa sababu (sura hiyo) ni tangazo la kujitoa kando katika shirki (ukafiri)".** Imepokewa na Ahmad kwa nambari (21934), Abudaud kwa nambari (5055), Tirmidhi kwa nambari (3403), na Shekh Albaani – Allah amrehemu - amesema kuwa ni Hadithi Hasan (inakubalika).

## 2 NA KUNA DUA NYINGI KUTOKA KATIKA SUNA. MIONGONI MWA HIZO NI HIZI:

1. **“Bismikallaahumma Amuutu Wa-ahyaa”**. (**Kwa jinal lako, Ewe Allah, ninakufa na ninakuwa hai**). Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6324), ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Hudhaifa- RAA-.

2. **“Allaahumma, Khalqta Nafsy, Wa-anta Tatawaffaahaa, Laka Mamaatuhaa Wamah-yaahaa, in-ahyaytahaa Fahfadh-haa, Wa-in Amaatahaa Faghfir Lahaa. Allaahumma, innii As-alaukal-aafiya”. (Ewe Allah, wewe umeumba nafsi yangu, na wewe utaiua. Uko kwako tu uhai wake na kifo chake. Ukiipa uhai, ihifadhi. Na ukiifisha (Ukiiua), isamehe. Ewe Allah, nakuomba uzima).** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2712).

3. **“Allaahumma, Rabbas-Samaawaatis-Sab-I, Warabbal-Ardhwi, Warabbal-‘Arshil-‘Adhwiim, Rabbanaa Warabba Kulli Shai-in, Faaliqal-habbi Wan-nnawaa, Wamunzilat-tauraati Wal-injiil, Walfurqaan. A’uwdhu Bika, Min-sharri Kulli Shay-in Anta Aakhidhunbinaaswiyatih. Allaahumma, Antal-Awwalu, Falaysa Qablaka Shay-un, Wa-antal-aakhiru, Falaysa Ba’-Daka Shay-un, Wa-antadhw-Dhwaahiru, Falaysa Fawqaka Shay-un, Wa-antalbaatwinu, Falaysa Duunaka Shay-un. Iqdhwi‘Annad-dayna, Wa-agh-ninaa Minal-faqri”, (Ewe Allah, Mola wa mbingu saba na Mola wa ardhi, na Mola wa Arshi Tukufu, Mola wetu na Mola wa kila kitu, Mpasuaji wa mbegu na kokwa, na Aliyeiteremsha Tawrati na Injili na Qur-ani. Naomba kinga kwako dhidi ya shari ya kila kitu wewe ndiye Mwenye kukidhibiti. Ewe Allah, wewe ndiye wa Mwanzo hakuna kitu kabla yako, na wa Mwisho hakuna kitu baada yako, na Uliye juu hakuna kitu juu yako, na Uliye karibu, hakuna kitu kilicho karibu kuliko wewe. Nilipie madeni na niepushe na ufukara).** Imepokewa na Muslim (2713).

4. **“Bismika Rabbii, Wadha’atu Jan-bii, Wabika Arfauhu, in-amsakta Nafsii Farhamhaa, Wa-in Arsaltahaa Fahfadh’haa Bimaa Tahfadhu Bihii ‘Ibaadakasswaalihiin”**. (**Kwa jina lako Mola wangu, nimeweka ubavu wangu, na kwa sababu yako nitaunyanyua. Ukiichukua roho yangu irehemu, na ukiirudisha ilinde kwa kile unachowalinda nacho waja wako wema.”** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6302) na Muslim kwa nambari (2714).

5. **“Alhamdulillaahilladhii Atw-amanaa Wasaqaanaa, Wakafaanaa Wa-aawaanaa, Fakam Mimman Laa Kaafiya Lah, Walaa Mu’uwiy”**, **(Sifa njema ni za Allah ambaye Ametulisha na ametunywesha, na**

**ametutosheleza, na ametuhifadhi. Ni wangapi ambao hawana wa kuwatosheleza wala wa kuwahifadhi**). Hii ni sehemu ya Hadithi ya Anas-RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa: "Hakika Mtume wa Allah–SAW- anapokwenda kwenye malazi yake alikuwa anasema: "**Alhamdulillaah.....".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2715).



Dhiktri Ni Ngao Imara, Na Ni Sababu Inayoleta Uhai Wa Moyo, Basi Kuwa Miongoni Mwa Wenye Kumdhukuru Allah, Amesema Mtume-SAW-: "Mfano Wa Mwenye Kumdhukuru Allah Na Asiyemdhukuru Allah Ni Mfano Wa Aliye Hai Na Maiti

6. **“Allahumma Qinii ‘Adhaabaka Yawma Tab-athu ‘Ibaadak”,** (**Ewe Allah, nikinge adhabu yako siku utakapofufua waja wako)**. Imepokewa na Ahmad kwa nambari (18660) na Shekh Albaani amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Swahiihuljaami’u 2/869).

7. Kufanya Tasbiih (Sub-haanallaah) na Tahmiid (Alhamdu Lillaah) mara thalathini na tatu, na Takbira (Allaahu Akbar) mara thalathini na nne.

Ni katika Suna mtu anapotaka kulala aseme “Sub-haanallaah” mara thalathini na tatu, na “Alhamdulillaah” mara thalathini na tatu, na “Allaahu Akbar” mara thalathini na nne. Jambo hili lina fadhila kubwa sana, nayo ni kuwa linaupa mwili nguvu katika siku yake.

Na ushahidi wa hili ni Hadithi ya Ali – RAA – “Kwamba, Fatma alilalamika juu ya ugumu aliokuwa akiupata katika mkono wake kutokana na jiwe la kusagia nafaka, na Mtume – SAW – alikuwa amepata mateka. Fatma akaondoka kwenda kwa Mtume – SAW – (ili apewe mfanyakazi wa nyumbani), lakini hakumkuta, na akakutana na Aisha na kumwambia (shida yake ya kuomba kupewa mfanyakazi). Mtume – SAW – alipokuja, Aisha alimwabia kuhusu kuja kwa Fatma. Mtume –SAW- akaja kwetu, tukiwa tumeshajilaza. Tukataka kuinuka, na Mtume –SAW- akatuambia “**Tulieni hivyo hivyo mlivyo”**, na akakaa kati yetu mpaka nikapata ubaridi wa miguu yake katika kifua change. Kisha akasema: **“Je, mnaonaje nikufundisheni kilicho bora zaidi kuliko kile mlichokiomba? Mnapoenda kulala mtakaseni Allah mara thalathini na tatu, na Mhimidini mara thalathini na tatu na mtukuzeni mara thalathini na nne. Hayo ni bora zaidi kwenu kuliko (kutafuta) mfanyakazi”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (3705) na Muslim kwa nambari (2727).

Na katika mapokezi mengine imenukuliwa kwamba Ali –RAA- alisema kuwa: **“Sikuyaacha maneno hayo tangu nilipoyasikia kwa Mtume –SAW-. Akaulizwa: Hata katika usiku wa (vita vya) Siffin? Akajibu: Hata katika usiku wa (vita vya) Siffin”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5362) na Muslim kwa nambari (2727).

8. **“Allaahumma, innii aslamtu nafsiy ilayka, wafawwadhwtu amriy ilayka, wa wajjahtu waj-hiya ilayka, wa-alja-tu dhwahriy ilayka, raghbatan warahbatan ilayka. Laa malja-a walaa man-jaa Minka illaa ilayka. Aamantu Bikitaabikal-ladhiy Anzalta wabinabiyyikal-ladhiy Arsalta”, (Ewe Allah, nimeisalimisha nafsi yangu kwako, na nimekuachia wewe mambo yangu, na nimeuelekeza uso wangu kwako, na nimeugemeza mgongo wangu kwako (nakutegemea wewe katika kusimamia mambo yangu kamwa mwanadamu anavyotegemea mgongo katika kusimama), kwa**

> **matajarajio (ya kupata rehema zako) na kwa kukuogopa (adhabu yako). Hakuna sehemu ya kukimbilia wala ya kujiokoa ila kwako tu. Nimekiamini kitabu chako ulichokiteremsha na Nabii wako uliyemtuma).** Ameipokea Bukhari kwa nambari (247) na Muslim kwa nambari (2710). Katika mwisho wa Hadithi Mtume – SAA – amesema kuwa: **"Na yafanye maneno hayo yawe maneno yako ya mwisho. Ukifariki usiku huo utafariki ukiwa katika maumbile ya asili (ya Tawhiid= kumwamini Allah tu).** Na katika upokezi wa Muslim imenukuliwa kwamba Mtume amesema: **"Na ikiwa utapambazukiwa, utapambazukiwa ukiwa katika kheri".**

Na katika Hadithi hii kuna ubainifu wa Suna nyingine. Suna hii ni kwamba, mtu anatakiwa afanye uradi huu uwe maneno yake ya mwisho anayoyatamka kabla hajalala. Pia kuna tuzo kubwa, nayo ni kwamba lau kama mtu atakadiriwa kufa usiku huo, atakuwa katika wale walokufa katika maumbile ya asili; yaani atakufa akiwa katika Suna katika mila ya Ibrahimu –AS-. Na akipambazukiwa atakuwa amepambazukiwa juu ya kheri katika riziki yake, na kazi yake. Uradi huo ni tamko lenye kukusanya yote yaliotangulia na mengine, na Allah ni Mjuzi zaidi.

Na miongoni mwa mambo yanayopasa kutolewa angalizo ni: Uradi mkubwa ambao ni sababu ya kupata fadhila kubwa. Allah Aliye Mtukufu amejigamba kwa uradi huo uliokuja katika Sahihi Bukhari, ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Shadad bin Aus – RAA – akimnukuu Mtume –SAW- kwamba amesema kuwa: **"Bwana wa kuomba maghfira (Dua kubwa) ni kusema, Allaahumma, anta Rabbiy, laa ilaaha illaa Anta. Khalaqtaniy wa-ana 'abduka. Wa ana 'alaa 'ahdika wa wa'adika mastatwa'atu. A'uudhu bika min-sharri maa swana'atu. Abuu-u laka bini'imatika 'alayya, wa abu-u laka bidhan-biy, faghfirliy, fa-innahuu laa yaghfirudh-dhunuuba illaa anta", (Ewe Allah, wewe ni Mola wangu, hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa wewe tu. Umeniumba na mimi ni mja wako, na mimi nimo katika kutekeleza maamrisho yako kadiri niwezavyo. Ninaomba kinga kwako dhidi ya kila shari niliyoitenda, Ninakiri neema zako kwangu, na ninakiri kukukosea. Kwa hivyo, nisamehe kwa sababu hakuna mwenye kusamehe madhambi isipokuwa wewe tu.** Akasema: **Atakayesema hayo wakati wa mchana akiwa na yakini nayo, na akafa siku hiyo kabla ya usiku kuingia, huyo ni katika watu wa Peponi. Na atakayesema hayo wakati wa usiku akiwa na yakini nayo, na akafa kabla ya asubuhi kuingia, huyo ni katika watu wa Peponi".** Ameipokea Bukhari kwa nambari (6306).

## SUNA KATIKA NDOTO

Anachokiona mwenye kulala hakitoki nje ya hali tatu zilizokuja katika Hadithi ya Abuhuraira –RAA- iliyopo katika mapokezi ya Muslim:

1. Ndoto njema ambayo ni bishara kutoka kwa Allah-SWT. Ndoto hii ina adabu zake na zitakuja.
2. Ndoto ya kuhuzunisha ambayo inatoka kwa shetani. Ndoto hii haimdhuru mja kama atafuata adabu zake, na zitakuja.
3. Kuota yale aliyokuwa akiyazungumza nafsini mwake kabla ya kulala. Ndoto hii haina maana yoyote.

### Na miongoni mwa Suna katika mlango huu ni yale mafundisho yalokuja katika Hadithi hizi zifuatazo:

Imenukuliwa kwa Abusalama –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa: **"Nilikuwa nikiota ndoto na kunipa ugonjwa".** Akasema: **"Nikakutana na Abukatada (nikamwambia naye), akasema: "Na mimi pia nilikuwa nikiota ndoto na kunipa ugonjwa, mpaka nilipomsikia Mtume – SAW - akisema: "Ndoto njema inatoka kwa Allah. Akiota mmoja wenu jambo analolipenda asimzungumzie ila yule anayempenda tu. Na akiota jambo asilolipenda anatakiwa apulize kushotoni kwake mara tatu, kisha aombe kinga kwa Allah dhidi ya shari ya shetani na shari ya alichokiota, wala asimhadithie yeyote, kwa sababu ndoto hiyo haitamdhuru".**

Na akasema Abusalama: **"Na nilikuwa naota ndoto nzito kwangu kuliko mlima. Tangu niliposikia Hadithi hii sikuijali ndoto hiyo".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5747) na Muslim kwa nambari (2261). Na katika mapokezi mengine kuna nukuu kwamba: "**Ndoto njema inatoka kwa Allah na ndoto mbaya inatoka kwa shetani. Akiona mmoja wenu ndoto anayoiogopa basi apulize kushotoni kwake, na aombe kinga kwa Allah dhidi ya shari yake, kwa sababu haitamdhuru**". Imepokelewa na Bukhari kwa nambari (3292) na Muslim kwa nambari (2261).

Na katika Hadithi ya Jabir –RAA- katika mapokezi ya Muslim, kuna nukuu kwamba Mtume –SAW-amesema: **"Na aombe kinga kwa Allah mara tatu dhidi ya shari ya shetani, na ageukie ubavu mwingine".** Ameipokea Muslim kwa nambari (2262).

Na katika Hadithi ya Abusaid Alkhudriy –RAA-katika mapokezi ya Bukhari kuna nukuu kwamba: **"Anapoota mmoja wenu ndoto anayoipenda, hakika**

**hiyo inatokana na Allah, na amhimidi Allah kwa ndoto hiyo”**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (7045).

### Tunapata katika Hadithi zilizopita kwamba:

1. Mwenye kuota ndoto nzuri ni Suna afanye yafuatayo:

   **Kwanza:** Amhimidi Allah kwa ndoto hiyo, kwa sababu inatoka kwake Sub-haanahuu Wata'aalaa.

   **Pili:** Aizungumze. Na asimzungumzie isipokuwa tu yule anayempenda.

2. Na kwamba yule aliyeota ndoto ambayo haipendi, ni Suna kwake kufanya yafuatayo:

   **Kwanza:** Ateme cheche za mate, au apulizie mate upande wa wake wa kushoto mara tatu.

   **Pili:** Aombe kinga kwa Allah – Aliyetukuka – dhidi ya Shetani, na dhidi ya shari ya alichokita. Afanye hivyo mara tatu, kwa kusema: “A'uudhu Billaahi Minash-shaitwaan, Wamin Sharrihaa” (Najikinga kwa Allah na shetani na shari ya nilichokiota**)** mara tatu.

   **Tatu:** Asimwambie yeyote. Akifanya hivyo, hakika haitamdhuru kama alivyoeleza Mtume – SAW -. Na akizidisha juu ya hayo:

   **Nne:** Ageuze upande ambao alikuwa amelalia. Ikiwa alikuwa amelala chali, alalie ubavu wake, n.k.

   **Tano:** Asimame na kuswali rakaa mbili.

Na inapatikana faida katika Hadithi zilizotangulia kwamba: Ndoto ya Muislamu ni sehemu ya unabii, na kwamba mtu mwenye ndoto za kweli zaidi ni yule mkweli zaidi katika mazungumzo anapokuwa macho. Hali hii inatokana na athari kusema kweli na baraka zake kwa Muislamu, hata anapokuwa usingizini.

### **Mwenye kuamka usiku ni Suna kwake kusema uradi huu:**

Uradi umekuja katika Hadithi ya Ubada bin Swamit – RAA – akimnukuu Mtume –SAW- kwamba, amesema kuwa: **“Atakayeshtuka usiku akasema: Laa ilaaha illa-llaah, Wahdahuu laa shariyka Lah, Lahul-Mulku walahul-Hamdu, wa-Huwa 'alaa kulli shay-in Qadiyr, Alhamdu lillaah, wa Subhaana-Allaah, walaa ilaaha illa-llaah, wa-llaahu Akbar, walaa hawla walaa quwwata**

**illaa biLlaah**", **(Hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allah Pekee, hana mshirika. Ufalme ni wake yeye tu, na Himdi ni Zake yeye tu, na yeye ni Muweza wa kila kitu. Himdi ni za Allaah, na ametakasika Allah, na hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allah tu, na Allah ni Mkubwa. Na hakuna uwezo (wa kufanya mema) wala nguvu (ya kuepuka maovu) ila kwa (msaada wa) Allaah tu".** Kisha akasema**: Rabbigh-fir-liy [Ewe Allah, nisamehe] au akaomba, ataitikiwa maombi yake. Na akitawadha na kuswali itakubaliwa Swala yake".** Imepokelewa na Bukhari kwa nambari (1154).

Imam Ibnul-athiir – Allah amrehemu - amesema kuwa: **"Atakayeshtuka usiku"** maana yake ni: Atakayezinduka katika usingizi wake na akaamka". Angalia kitabu: Annihaaya Fii Ghariibil-athar cha Ibnul-thiir, ukurasa wa 108.

Katika hii Hadithi kuna bishara mbili kubwa. 1) Ni kwamba, mwenye kuzinduka usiku katika kulala kwake na akasoma uradi huu: **Laa ilaaha illallaah, Wahdahuu Laa Shariika Lah, Lahulmulku, Walahulhamdu, Wahuwa Alaa Kulli Shay-in Qadiir, Alhamdulillaah, Wasub-haanallah, Walaa ilaaha illallah, Wallaahu Akbar, Walaahawla, Walaaquwwata illaa Billaah," (Hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allah Pekee, Hana mshirika, Ufalme ni wake yeye tu, na Himdi ni zake yeye tu, Na yeye ni Muweza wa kila kitu. Ametakasika Allah, na Himdi ni za Allah, na hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allah tu, Allah ni Mkubwa kabisa, na hakuna uwezo (wa kufanya mema) wala nguvu (ya kuepuka maovu) ila kwa (msaada wa) Allah).** Mwenye kusema uradi huu ana bishara mbili:

> **Ya kwanza:** Akisema "Allahumma Ghfirlii", **(Ewe Mola wangu, nisamehe)**, au akiomba dua, hakika dua yake itajibiwa.
>
> **Ya pili:** Ikiwa atasimama, atatawadha na kuswali swala yake itakubaliwa. Tunashukuru Allah ambaye ametutunuku fadhila hizi. Tunamuomba atuwezeshe kuyafanyia kazi haya kwa vitendo.

Na kwa Suna hii tunamalizia kueleza Suna zilizowekewa nyakati maalumu, kwa sababu zinazokuja baada ya hapo ni Suna za kuamka kutoka usingizini, ambazo tumeanza nazo na ya mwanzo ni kupiga mswaki, na kusema "**Alhamdulillaahilladhii Ah-yaanaa, Ba'adamaa Amaatanaa, Walaihinnushuur**", **(Sifa zote njema ni za Allah ambayo ametuhuisha baada ya kutufisha, na kwake yeye tu ndio marejeo).**







# SUNA ZISIZOWEKEWA NYAKATI MAALUMU

Hiki ni kigawanyo cha pili katika Suna za kila siku. Mlango wa Suna za aina hii ni mpana, ni nyingi. Kuna zile zinazokuwa tofauti kutokana na tofauti za hali, watu, mahali na nyakati.

Nitafanya bidii ya kuonesha Suna zinazojirudiarudia usiku na mchana, nikimuomba Allah Mtukufu msaada na ufanisi.

**KITU CHA KWANZA KATIKA SUNA ZA KIGAWANYO HIKI NI:**

## Moja: Sunnah Za Chakula



### 1 KUTAJA JINA LA ALLAH MWANZO WA KULA.

Imenukuliwa kwa Umar bin Abusalama – RAA – akisema kuwa: **"Nilikuwa kijana mdogo chini ya ulezi wa Mtume wa Allah, na mkono wangu ulikuwa ukizungukazunguka hovyo katika sinia (ya chakula). Mtume wa Allah akaniambia: "Ewe kijana! Taja jina la Allaah na kula kwa mkono wako wa kulia, na ule kilicho mbele yako". Basi huo ukawa ndio mtindo wangu wa kula baadaye.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5376) na Muslim (2022).

Na mtu akisahau kutaja jina la Allah: Ni Suna aseme pale anapokumbuka; **"Bismillaahi Awwalahuu Wa-aakhirah", ({nakula} Kwa jina Allah Mwanzo wake na mwisho wake).**

Kwa mujibu wa Hadithi ya Aisha – RAA – kwamba, Mtume wa Allah–SAW- amesema kuwa: **"Anapokula mmoja wenu ataje jina la Allah. Na akisahau kutaja jina la Allah mwanzo wake aseme: "Bismillaahi Awwalahuu Wa-aakhirah".** Imepokewa na Abudaud kwa nambari (3767) na Tirmidhi kwa nambari (1858). Na Shekh Albani amesema kuwa ni Hadithi sahihi, kama ilivyotangulia kuelezwa.

Pia Hadithi hii ni ushahidi kwamba, mwanadamu anatakiwa ale kwa mkono wake wa kulia ili asijifananishe na shetani. Muislamu anapokuwa hajataja

jina la Allah, shetani hushirikiana naye katika chakula chake. Na anapokula au kunywa kwa mkono wake wa kushoto, anajifananisha na shetani kwa kufanya hivyo, kwa sababu shetani anakula na kunywa kwa mkono wake wa kushoto.

Na hoja ya hili ni:

Hadithi ya Abdallah bin Umar – RAA – kwamba, Mtume wa Allah–SAW- amesema kuwa: **"Asile mmoja wenu kwa mkono wake wa kushoto, wala asinywe kwa mkono huo, kwa sababu Shetani anakula kwa mkono wake wa kushoto na anakunywa kwa mkono huo".** Na Imam Naafi alikuwa anazidisha: **"Wala asipokee (kitu) kwa mkono huo (wa kushoto) na wala asitoe (kitu kumpa mtu) kwa mkono huo (wa kushoto)".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2020).

Na Shetani hutaka sana kuingia katika majumba ili alale humo na ashirikiane na watu wa majumba hayo chakula na kinywaji. Imepokewa kwa Jabir bin Abdallah- RAA- kwamba, alimsikia Mtume –SAW-akisema kuwa: **"Mtu anapoingia nyumbani kwake au anapokula akamtaja Allah wakati wa kuingia kwake na wakati wa kula kwake, Shetani husema (kuwaambia mashetani wenzake kuwa): "Hmna mahali pa kukaa wala chakula". Lakini mtu akiingia bila ya kumtaja Allah, Shetani husema (kuwaambia mashetani wenzake kuwa): "Mmepata mahali pa kukaa". Na Muislamu asipomtaja Allah wakati wa kula, Shetani husema (kuwaambia mashetani wenzake kuwa): "Mmepata mahali pa kukaa na chakula".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2018).

## 2 KULA KILICHO MBELE.

Kwa mujibu wa Hadithi iliyotangulia ya Umar bin Abusalama -RAA-. Ndani ya Hadithi hiyo kuna kauli ya Mtume –SAW- : **"Na kula kilicho mbele yako".**



## 3 KUOKOTA TONGE ILIYOANGUKA, KUTOA UCHAFU ILIOUPATA NA KUILA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Jabir – RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, nilimsikia Mtume –SAW- akisema kwamba: **"Hakika, Shetani anamuandama mmoja wenu katika kila jambo lake. Anamuandama hata kwenye chakula chake. Kwa hiyo, inapomuanguka mmoja wenu tonge ya chakula, aondoe**

**sehemu iliyoingia taka na aile, na wala asimuachie shetani. Akimaliza (kula) arambe vidole vyake, kwa sababu mtu hajui baraka ipo katika chakula chake kipi"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (2033).

Anayeiangalia Hadithi hii atakuta kwamba, Shetani ana shauku kubwa ya kutaka kushirikiana na mwanadamu katika mambo yake yote, ili aondoe baraka katika maisha yake, na amharibie mambo yake mengi. Miongoni mwa ushahidi unao onesha kuwa shetani anamuandama mja katika mambo yake yote ni kauli ya Mtume -SAW- isemayo kuwa: "**Hakika, Shetani anamuandama mmoja wenu katika kila jambo lake**".

## 4 KURAMBA VIDOLE.



Na "Kuramba vidole" ni kaviramba kwa kutumia ulimi wake. Suna ni kuviramba, au kumrambsha mtu mwengine kama vile mkewe kwa mfano. Lakini Suna sio kupangusa chakula kinachobaki katika mkono wake kwa kitambaa, na mfano wake. Suna ni avirambe.

Na hoja ya hilo ni: Hadithi ya Jabir- RAA- iliyopita.

Na katika Sahiih Bukhararii na Sahiih Muslim kuna nukuu ambayo ni sehemu ya Hadithi ya Ibniabass –RAA- kwamba Mtume –SAW- amesema kuwa: **"Anapokula mmoja wenu asifute mkono wake mpaka aurambe au aurambishe"**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (5456) na Muslim kwa nambari (2033).

## 5 KUKOMBA SAHANI.



Makusudio ya kukomba sahani ni: Mlaji kusafisha eneo lake alilokulia chakula chake. Kwa mfano: Anayekula wali, ni katika Suna kutobakisha chochote katika eneo la sahani yake anayokulia. Anatakiwa apanguse kinachobaki katika sahani yake na akile, kwa sababu inaweza kuwa baraka ya chakula hicho iko katika hiki kilichobaki katika sahani yake.

Na hoja ya hilo ni Hadithi ya Anas -RAA- aliyenukuliwa kusema kwamba: **“Na - Mtume –SAW- ametuamrisha kukomba (chakula kwenye) sahani”**. Ameipokea Muslim kwa nambari (2034). Na katika upokezi wa Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira -RAA- kuna nukuu kwamba: **“Na akombe mmoja wenu (chakula kwenye) sahani”**. Ameipokea Muslim kwa nambari (2035).

Shekhe wetu Ibniuthaimin – Allah amrehemu – amesema kuwa: **“(Suna hii ina maana kwamba: Ufuatilie chakula kilichobaki katika sahani kwa kutumia vidole vyako na uvirambe. Hii vilevile ni katika Suna ambazo, kwa masikitiko, watu wengi, hata wanazuoni, wamezipuuza, pia”.** Angalia Sharhu Riyaadhusswaalihiin (1/892).

### 6 KULA KWA VIDOLE VITATU.



Na Suna ni kula kwa kutumia vidole vitatu. Hii ni katika vyakula vinavyochukulika kwa vidole vitatu, kama tende mfano. Ni Suna ale chakula cha aina hiyo kwa vidole vitatu.

Na hoja ya hili ni: Hadithi ya Kaabi bin Maalik -RAA-akinukuliwa kusema kuwa: **“Mtume -SAW- alikuwa anakula kwa vidole vitatu, na anaramba mkono wake kabla ya kuupangusa”.** Ameipokea Muslim kwa nambari: (2032).

### 7 KUPUMUA NJE YA CHOMBO MARA TATU.



Ni katika Suna kunywa kwenye chombo funda tatu, na apumue baada ya kila funda moja.

Na hoja ya hilo ni: Hadithi ya Anas –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa: “Mtume –SAW- alikuwa akipumua mara tatu katika kunywa kinywaji, na anasema: **“Hakika, njia hiyo inakata kiu zaidi, na inapozesha zaidi, na inaburudisha zaidi”.** Anas -RAA- amesema**: “Mimi napumua mara tatu nikinywa kinywaji”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5631), na Muslim kwa nambari (2028).

Makusudio ya kupumua katika chombo ni: Kupumua wakati wa kunywa kwake katika chombo, kwa maana ya kwamba: anapumua nje ya chombo, kwa sababu kupumua ndani ya chombo ni makuruhu, kwa mujibu wa Hadithi ya Abukatada – RAA – iliopo katika Sahiih Bukhaariy na Sahiih Muslim kwamba, Mtume –SAW- amesema kuwa: **“Anapokunywa mmoja wenu asipumulie ndani ya chombo**”. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5630) na Muslim kwa nambari (267).

## 8 KUMHIMIDI ALLAH BAADA YA CHAKULA.




Na hoja ya Suna hii ni:

Hadithi ya Anas bin Malik –RAA- aliyenukuliwa kusema kwamba, Mtume –SAW- amesema kuwa: **“Hakika, Allah anamridhia mja alapo chakula kisha akamhimidi Allah kwa chakula hicho, au anywapo kinywaji kisha akamhimidi Allah kwa kinywaji hicho”.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2743).

Kuhimidi kuna matamshi mbalimbali. Miongoni mwa hayo ni:

1. **“Alhamdulillaahi Kathiiraa, Twayyiban, Mubaarakan Fiih, Ghayra Makfiiyyin Walaa Muwadda’in, Walaa Mustaghnaan ‘Anhu Rabbanaa”,** (**Sifa njema ni za Allah, sifa nyingi nzuri, zenye baraka ndani yake. Allah asiyetoshelezwa wala kususwa, wala kutohitajika Eee Mola wetu**). Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5458).
2. **“Alhamdulillaahilladhii Kafaanaa, Wa-arwaanaa, Ghayr Makfiyyin Wala Makfuur”, (Sifa Njema ni za Allah ambaye ametutosha, na ametuondoshea kiu, asiyetoshwa wala kukanwa).** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5759).

(**Asiyetoshwa**) Inamaanisha asiyemhitaji yeyote. Yeye ndiye huwapa chakula waja wake na kuwatosheleza. (**Kutengwa**) Yaani: Haachwi. (**Kafaanaa**) Ametutosha. Na (**Katuondoshea kiu**) ametupa maji. (**Kukanwa**) hakuna wa kupinga fadhila na neema zake.

## 9 KUJUMUIKA KWA AJILI YA CHAKULA.



Ni katika Suna kujumuika kwa ajili ya chakula, na kutokaa mbalimbali.

Ushahidi wa hilo ni: Hadithi ya Jabir bin Abdallah -RAA- akinukuliwa kusema kuwa: **“Nilimsikia Mtume wa Allah –SAW- akisema kuwa: “Chakula cha mtu mmoja kinawatosha watu wawili, na chakula cha watu wawili kinawatosha watu wanne, na chakula cha watu wanne kinawatosha watu wanane”.** Imepokelewa na Muslim kwa nambari (2059).

## 10 KUSIFU CHAKULA ANAPOKIPENDA.

Ni katika Suna mtu kukisifia chakula kikimpendeza. Na hakuna shaka kwamba mtu hakisifii chakula isipokuwa tu ni kwa sababu ya kilichomo ndani yake.

Na ushahidi wa hili ni: Hadithi ya Jabir bin Abdallah -RAA- kwamba, Mtume –SAW- alimuomba mke wake kitoweo, na wakasema: Hatuna isipokuwa siki tu. Akaomba apewe. Akawa anakula huku akisema: **“Kitoweo bora ni siki. Kitoweo bora ni siki”.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2052). Siki ni aina ya kitoweo chao (wakati huo) na ni tamu, sio chachu kama siki yetu hivi sasa.

Shekhe wetu Ibniuthaimini -Allah amrehemu- amesema kuwa: **“Na hii pia ni katika mwongozo wa Mtume-SAW-kwamba, mtu akikipenda chakula akisifie. Kwa mfano: kama umevutiwa na mkate na ukataka kuusifia, unasema: Mkate mzuri ni mkate wa Fulani, au mfano wa maneno kama hayo. Hii nayo ni Suna ya Mtume –SAW-.**” Angalia Sharhu Riyaadhusswaalihiin (2/1057).

Mwenye kuangalia hali yetu ya sasa atakuta kwamba, mara nyingi watu wanafanya tofauti na Suna ya Mtume. Sio kwamba wameacha Suna tu, lakini pia wanaipinga kwa kukitia ila chakula wakati mwingine, jambo ambalo ni kinyume na muongozo wa Mtume-SAW-. Katika Sahiih Bukhararii na Sahiih Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira –RAA- amenukuliwa kusema kuwa: **“Mtume –SAW- katu hakukitia dosari chakula. Alipokipenda alikila na alipokuwa hakipendi alikiacha”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (3563) na Muslim kwa nambari (2064).

### 11 KUMUOMBEA DUA MWENYE CHAKULA.

Na hoja ya hili ni Hadithi ya Abdallah bin Busri - RAA-aliyenukuliwa kusema kuwa: **"Mtume –SAW- alikuja kwa baba yangu akiwa mgeni. Akasema (Abdallah bin Busri) kuwa: "Na tukamkaribisha (Mtume) chakula; tende na mseto (wa tende, maziwa yaliyokaushwa na samli), na akala. Kisha akaletewa tende, akawa anakula na kutupa kokwa zake kati ya vidole vyake, na anakunja kidole cha shahada na cha katikati. Kisha akaletewa kinywaji akanywa, na kisha akampa aliyekuwa upande wake wa kulia.** Akasema (Abdallah bin Busri) kuwa**: "Baba yangu akiwa ameshika hatamu ya mnyama wa Mtume na alimwambia (Mtume) kuwa: "Tuombee Mungu. Mtume akasema: "Ewe Allah, wabariki katika riziki uliyowapa, na wasamehe, na warehemu".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2042).

**Mseto (huu):** Ni aina ya chakula cha mchanganyiko wa tende, maziwa yaliyokaushwa na samli.

### 12 Kupendekezwa kumpa kinywaji mtu aliyepo upande wake wa kulia kabla ya aliyepo upande wa kushoto.

Kinachokusudiwa ni kuwa, ni katika Suna mtu akinywa ampe aliyepo upande wake wa kulia kabla ya aliyepo upande wa kushoto.

Na ushahidi juu ya hilo ni Hadithi ya Anas bin Malik-RAA- alinukuliwa kusema kuwa: **"Alitujia Mtume –SAW- katika nyumba yetu. Akaomba kinywaji, na tukamkamulia mbuzi. Kisha nikachanganya maziwa (hayo ya mbuzi) na maji ya kisima changu hiki.** Akasema Anas**: Nikampa Mtume –SAW- na akanywa huku Abubakar akiwa kushotoni mwake, Umar akiwa mbele yake na Bedui mmoja akiwa upande wake wa kulia. Mtume wa Allah alipomaliza kunywa, Umar akamwambia Mtume: Huyu hapa Abubakar ewe Mtume wa Allah, akimwashiria. Mtume akampa Bedui, na kuwacha Abubakar na Umar, na kusema: Wa kuliani (kwanza). Wa kuliani (kwanza). Wa kuliani (kwanza)".** Akasema Anas –RAA-: **"Hiyo ni Suna. Hiyo ni Suna. Hiyo ni Suna"**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (2571) na Muslim kwa nambari (2029).

### 13 MWENYE KUWAGAWIA WATU KINYWAJI AWE WA MWISHO KUNYWA.

Ni Suna kwa mwenye kuwapa kinywaji watu awe wa mwisho wao kunywa.

Na hoja juu ya hilo: Ni Hadithi ndefu ya Abukatada –RAA-, na ndani ya Hadithi hiyo kuna nukuu kwamba: "Akawa Mtume –SAW- anajaza (kinywaji



kwenye chombo) na mimi nawapa wanywe, mpaka ikawa hakubakia yeyote ila mimi tu na Mtume –SAW. Kisha Mtume –SAW- akajaza (chombo) na kuniambia "Kunywa". Nikamwambia: "Hapana, sinywi mpaka unywe wewe (kwanza) ewe Mtume wa Allah. Akasema: "Hakika, mwenye kuwanywesha watu ndiyo wa mwisho wao kunywa". Akasema Anas: Nikanywa na Mtume-SAW- naye akanywa". Imepokewa na Muslim kwa nambari (681).

**Faida:** Na ni katika Suna kwa mwenye kunywa maziwa asukutue kwa maji baada ya kunywa maziwa, ili aondoe lehemu iliyopo mdomoni mwake inayotokana na maziwa hayo. Na hoja ya hili ni Hadithi ya Ibniabass -RAA- akinukuliwa kusema kuwa: **"Mtume – SAW - alikunywa maziwa kisha akaomba maji. Akasukutua na kusema: "Hakika, (maziwa) yana lehemu".** Imepokewa na Bukhari (211) na Muslim kwa nambari (358).

## 14 KUFUNIKA CHOMBO NA KUTAJA JINA LA ALLAH MTUKUFU USIKU UNAPOINGIA



Ni Suna kufunika chombo ambacho kiko wazi wakati usiku unapoingia, na kufunika mitungi ya maji kama ina kifuniko, na kutaja jina la Allah wakati ukifanya hivyo.

Na hoja ya hilo ni Hadithi ya Jabir bin Abdallah -RAA-aliyenukuliwa kusema kuwa: "Nimemsikia Mtume wa Allah –SAW- akisema kuwa: **Funikeni vyombo, na fungeni viriba. Hakika, katika mwaka kuna usiku mmoja ambao huteremka ndani yake ugonjwa. (Ugonjwa huo) Haukipitii chombo ambacho hakijafunikwa, au kiriba (mtungi) ambao hauna kifuniko, isipokuwa kwamba huingia humo".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2014). Na mapokezi ya Bukhari ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Jabir - RAA- pia kuna nukuu kwamba: **"Na fungeni viriba vyenu, na tajeni jina la Allah, na funikeni vyombo vyenu na tajeni jina la Allah. (Funikeni) hata kama ni kwa kuwekea kitu (chochote) juu"**. Imepokewa na Bukhari (5623).

## Mbili: Sunnah Za Salamu, Kukutana Na Kikao



### 1 Ni katika Suna kusalimu.

Na hoja ya Suna hii ni nyingi mno. Miongoni mwa hoja hizo ni: Hadithi ya Abuhuraira -RAA- akinukuliwa kusema kwamba, Mtume-SAW- amesema kuwa: **"Haki za Muislamu kwa Muislamu (mwenzake) ni sita. Mtume aliulizwa: Ni zipi haki hizo ewe Mtume wa Allah? Mtume akasema: Ukikutana naye msalamie, na akikualika muitikie, na akikutaka ushauri mshauri, na akipiga chafya akamhimidi Allah (yaani akasema Alhamdulillaah), muombee Rehema (Mwambie: Yarhamukallaahu), na akiugua mtembelee, na akifa sindikiza jeneza lake".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2162).

Ama kujibu Salamu ni: wajibu. Na hoja juu ya hili ni:

Kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa: {**Na mtakapoamkiwa kwa maamkizi yoyote, itikieni kwa maamkizi yaliyo mazuri zaidi kuliko hayo au yarudisheni hayo hayo. Hakika, Allah daima ni Mwenye kuhesabu kila kitu**}. (Sura Annisaa: 86).

Na asili katika amri ni lazima, madamu amri hiyo haijaondolewa na cha kuiondoa (katika ulazima). Wanazuoni wengi wamenukulu makubaliano juu ya wajibu wa kujibu Salamu. Miongoni mwa wanazuoni hao ni Ibnihazmi, Ibniabdulbari, Sheikh Taqiyyudiin na wengine – Allah awarehemu wote-. Angalia: Al-aadaab Ash-shar-iyya (1/356), chapisho la Mu-assasaturrisaala.

Na tamko bora na kamilifu mno la kusalimu na kujibu Salamu ni: **(Assalaamu Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh = Amani iwe kwenu na rehema za Allah na Baraka zake)**. Tamko hii ndio salamu bora zaidi na timilifu zaidi.

Ibnulqayyim –Allah amrehemu- amesema kuwa: **"Na muongozo wa Mtume -SAW- ulikuwa kuishia Salamu mpaka: (Wabarakatuh)".** Angalia: Zaadul Ma'ad (417/2).

Na kutangaza Salamu sio kwamba ni Suna tu, lakini pia ni Suna iliyotiwa ushawishi kwamba ina fadhila kubwa, kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhurara -RAA- akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah-SAW- amesema kwamba: **"Nina apa kwa (Allah) ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake, hamtaingia Peponi hadi muamini. Na hamuwezi kuamini hadi mpendane. Je, nikufahamisheni jambo ambalo mtakapolifanya mtapendana? Tangazeni Salamu baina yenu"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (54).

## 2 KUPENDEKEZWA KURUDIA SALAMU MARA TATU, PANAPOKUWA NA HAJA YA KUFANYA HIVYO.

Kama vile mtu kuwa na shaka kwamba, aliyemsalamia hakusikia alipomsalamia mara ya kwanza. Hapo, inapendekezwa arudie mara ya pili. Na kama hakusikia, arudie mara ya tatu. Ni kama hivyo mtu akiingia pahala penye mjumuiko wa watu wengi; kama vile mtu kuingia katika kikao kikubwa chenye watu wengi. Akisalimia mara tu pale mwanzo anapoingia, hawatasikia salamu hiyo isipokuwa tu wale walioko mwanzoni. Katika hali hiyo. inahitajika asalamie mara tatu ili wasikie watu wote walio katika kikao.

Na hoja juu ya hili ni Hadithi ya Anas –RAA- akinukuu kwamba, Mtume –SAW-: **"Mtume alikuwa akiongea neno hulirudia mara tatu; mpaka lifahamike. Na akiwajia watu na kuwasalamia, huwasalamia mara tatu".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (95).

Na inachukuliwa katika Hadithi ya Anas -RAA- iliyotangulia kwamba ni Suna kurudia neno mara tatu kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo, kama mtu kuzungumza na maneno yake yakawa hayajafahamike. Ni Suna kurudia, na kama hayajafahamika arudie mara tatu.

### 3 NI KATIKA SUNA KUSALIMIA WOTE; UNAYEMJUA NA USIYEMJUA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abdallah bin Amri –RAA- kwamba: “Mtu mmoja alimuuliza Mtume wa Allah kwamba: Uisilamu upi ni bora? Mtume akasema: **“lisha chakula, na msalimie unayemjua na usiyemjua”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (12), na Muslim kwa nambari (39).

### 4 SUNA NI KUANZA KUMSALIMU YULE AMBAYE SUNA IMETAJA AANZE KUSALIMIWA.

Imenukuliwa kwa Abuhuraira –RAA- akisema kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema: **“Aliyepanda (chombo cha usafiri) amsalimie anayetembea kwa mguu, na mwenye kutembea kwa mguu amsalimie aliyeketi, na wachache wawasalamie wengi”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari: (6233) na Muslim kwa nambari (2160). Na katika mapokezi ya Bukhari kuna nukuu kwamba: **“Mdogo amsalimie mkubwa, na mwenye kupita amsalimie aliyekaa, na wachache wawasalamie wengi”**. Ameipokea Bukhari kwa nambari (6234).

Kufanya tofauti ya utaratibu bora katika kusalimia haimaanishi kwamba ni makruhu. Hakuna ubaya kufanya hivyo, lakini ni kufanya tofauti iliyo bora; kama mkubwa kumsalamia mdogo, mwenye kutembea kwa miguu kumsalimia aliye katika chombo cha usafiri, na mfano wa hivyo.

### 5 NI KATIKA SUNA KUWASALAMIA WATOTO.



Kwa mujibu wa Hadithi ya Anas bin Malik -RAA- akinukuliwa kusema kwamba, **“Alikuwa akitembea na Mtume –SAW- na akapita kwa watoto na Mtume akawasalimia”**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6247) na Muslim (2168).

Katika kuwsalamia watoto kuna: Kuifanya nafsi kuwa na unyenyekevu, na kuzoesha watoto waizowee nembo hii ya dini na kuifanya iwe hai katika nyoyo zao.

### 6 NI KATIKA SUNA KUSALIMIA WAKATI WA KUINGIA NYUMBANI.

Na hii inaingia katika ujumla wa kusalimia. Na hayo ni baada ya kupiga mswaki, kwa sababu kupiga mswaki unapoingia nyumbani ni Suna. Hii ndio



sehemu ya nne katika sehemu ambazo Suna ya kupiga mswaki inasisitizwa. Sehemu hiyo ni: Wakati wa kuingia nyumbani, kwa mujibu wa Hadithi ya Bi Aisha –RAA- katika mapokezi ya Muslim. Aisha amenukuliwa kusema kuwa: **"Mtume –SAW- alikuwa anapoingia nyumbani kwake anaanza kwa kupiga mswaki".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (254). Mtume alikuwa akianza kuingia nyumbani kwake kwa kupiga mswaki kisha huingia na kuwasalamia waliomo humo. Baadhi ya Wanazuoni wamesema kuwa: Ni katika Suna kusalimia unapoingia kwenye nyumba yoyote, hata kama ndani ya nyumba hiyo hakuna mtu yeyote, kwa mujibu wa kauli ya Allah kwamba: **{Na mtakapoingia majumbani salimianeni (kama kuna watu, na kama hakuna watu jisalimieni wenyewe); maamkizi kutoka kwa Allah, yenye Baraka, mazuri. Kama hivyo Allah anakubainishieni Aya ili mpate kutia akilini}.** Sura Annuur, aya 61.

Ibnihajar- Allah amrehemu amesema kuwa: "Na inaingia katika ujumla wa kutangaza Salamu kwa mtu mwenye kuingia sehemu ambayo hakuna mtu yeyote, kwa mujibu wa kauli ya Aliyetukuka kwamba: {**Na mtakapoingia majumbani toleaneni salamu (kama kuna watu, na kama hakuna watu jisalimieni wenyewe)**}. Angalia: Fat-hulbaariy, Hadithi (6235), mlango wa kutoa Salamu.

**Faida: Imepatikana kutoka katika maelezo yaliyopita kwamba kuna Suna za aina tatu wakati wa kuingia ndani nyumba:**

1. **Ya kwanza:** Kutaja jina la Allah, na hasa usiku.

   Kwa mujibu wa Hadithi ya Jabir bin Abdallah -RAA- kwamba, alimusikia Mtume - SAW- akisema kuwa: **"Mtu anapoingia nyumbani kwake, na akamtaja Allah wakati wa kuingia kwake, na wakati wa kula kwake, shetani husema (kuwaambia wenzake): Hakuna pa kulala leo wala chakula cha jioni. Na mtu anapoingia (nyumbani kwake) na hukumtaja Allah, shetani husema (kuwaambia wenzake): Mmepata pa kulala. Na kama hakumtaja Allah wakati wa kula kwake, shetani husema (kuwaambia wenzake): mmepata pa kulala, na chakula cha jioni".** Imepokewa na Muslim (2018).

2. **Ya pili:** Kupiga mswaki, kwa mujibu wa Hadithi ya Bibi Aisha –RAA- iliyotangulia kutajwa hapo nyuma.

3. **Tatu**: Kuwasalimia walioko nyumbani.

### 7 NI KATIKA SUNA KUPUNGUZA SAUTI WAKATI WA KUWASALIMIA WATU AMBAO MIONGONI MWAO WAMO WALIOLALA.

Na hivyo ndivyo alivyokuwa akifanya Mtume-SAW- kama ilivyo katika Hadithi ya Mikidadi bin Al-as-wad- RAA-. Katika Hadithi hiyo, amesema Mikidadi kuwa: **"……..Na tulikuwa tunakama na kila mtu anakunywa fungu lake, na tunampelekea Mtume-SAW- fungu lake. Akasema: Na (Mtume) anakuja usiku na anasalamia Salamu ambayo haimwamshi aliyelala, na aliye macho anaisikia".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2055).

### 8 NI KATIKA SUNA KUFIKISHA SALAMU.

Kufikisha Salamu ni Suna, kama vile mtu akuambie: "Nisalamie fulani". Kwa hakika, ni katika Suna kwako kuifikisha Salamu hii kwa aliyesalimiwa.

Na hoja ya hili ni Hadithi ya Aisha –RAA- kwamba, Mtume –SAW- alimwambia: **"Hakika, Jibrili anakusalamia. (Aisha) Akasema: Na nikajibu: Na Amani na iwe ju yake na rehema za Allah".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (3217), na imepokewa na Muslim kwa nambari (2447).

Katika Hadithi hii kuna (maelekezo ya) kufikisha Salamu kwa aliyesalimiwa, kama Mtume -SAW- alivyofikisha Salamu za Jibrili -AS- kwa Bi Aisha-RAA-. Pia katika Hadithi hii iliyotangulia tunajifunza kwamba ni Suna kumtuma mtu apeleke Salamu.

### 9 KUTOA SALAMU WAKATI WA KUINGIA KATIKA KIKAO, NA WAKATI WA KUONDOKA KIKAONI PIA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema kwamba: **"Anapoingia mmoja wenu katika kikao asalimie. Na anapotaka kuondoka asalamie, kwa sababu sio kwamba Salamu ya kwanza ina haki zaidi kuliko Salamu ya mwisho".** Ameipokea Ahmad kwa nambari (9664), Abudaudi kwa nambari (5208) na Tirmidhiy kwa nambari (2706). Shekh Albaniy amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Sahiihuljaami'u 1/132).



### 10 WAKATI WA KUKUTANA NI SUNA KUPEANA MIKONO PAMOJA NA KUSALAMIANA.

Na hivi ndivyo Swahaba, Allah awawie radhi, walivyokuwa wakifanya. Hoja ya hili

ni: Hadithi ya Katada –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa: **“Nilimwambia Anas: Je, Swahaba wa Mtume walikuwa wanasalamiana kwa kupeana mikono? Akasema: Naam”.** Imepokewa na Bukhaari kwa nambari (6263).



## 11 NI SUNA KUTABASAMU NA KUONESHA BASHASHA YA USO WAKATI WA KUKUTANA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abudhari -RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, “Mtume-SAW- aliniambia: **Usidharau jambo lolote katika mema, hata kama ni kukutana na ndugu yako kwa uso wa bashasha”.** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2626). Na kwa nukuu ya Tirmidhiy ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abudhari -RAA- imenukuliwa kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema kwamba: **“Kutabasamu kwako katika uso wa ndugu yako ni sadaka kwako”**. Imepokewa na Tirmidhiy kwa nambari (1956), na Shekh Albaniy amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Silisila Swahiha 572).

## 12 MANENO MAZURI NI SUNA NA NI SADAKA.

Ni sawa maneno mazuri hayo ni wakati wa kukutana, au kikaoni, au katika hali yeyote ile. Maneno mazuri ni Suna, kwa sababu ni sadaka.
Na hoja ya hili ni: Hadithi ya Abuhuraira - RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah -SAW- amesema kwamba: **“Na maneno mazuri ni sadaka”.**

Imepokewa na Bukhari, kwa nambari (2989), na Muslim kwa nambari (1009).

Na mara nyingi watu wamekuwa wakizungumza maneno mazuri. Lau kama wangenuia kupata thawabu wangelipwa kheri nyingi, na wangepata fungu kubwa la sadaka hizi.

Shekhe wetu Ibniuthaimini - Allah amrehemu - amesema kuwa: **“Maneno mazuri ni kama kumwambia (mwenzako): Hujambo? Uhali gani? Vipi ndugu zako?”**

**Ihali gani familia yako? Na maneno mengine yanayofanana na hayo, kwa sababu haya ni katika maneno mazuri ambayo yanaingiza furaha kwa mwenzako. Kila neno zuri ni sadaka kwako mbele ya Allah, ni malipo na ni thawabu”.** Angalia: Sharhu Riyaadhusswaalihiina ya Shekhe wetu (2/996), mlango wa: Kupendekezwa kwa maneno mazuri, na kuoneshana uso wa bashasha wakati wa kukutana.

## 13 KUPENDEKEZWA KUMTAJA ALLAH KATIKA KIKAO.

Hadithi katika kuelezea fadhila za vikao vya kumtaja Allah, na kuhimiza hilo ni nyingi. Katika hizo ni Hadithi ya Abuhuraira - RAA- akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah-SAW-amesema kwamba: **“Hakika, Allah ana Malaika wanaozunguka katika njia, wakitafuta watu wanaomtaja Allah. Wanapokuta watu wanaomtaja Allah huitana (na kuambiana): Njooni kwenye haja yenu (Mliyokuwa mkiitafuta). Mtume akasema: Watawafunika kwa mbawa zao mpaka katika uwingu wa dunia**”. Imepokewa na Bukhari kwa nambari: (6408) na Muslim kwa nambari (2689).

## 14 NI SUNA KUFUNGA KIKAO KWA (DUA YA KAFARA YA KIKAO)

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira –RAA- akinukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah- SAW- amesema kwamba: **“Atakayekaa katika kikao kikawa na kelele nyingi, na akasoma (dua ifuatayo) kabla ya kuondoka katika kikao chake hicho: “Sub-haanakallaahumma wabihamdika, Ash-hadu Allaa ilaaha illaa Anta, Astaghfiruka wa-atuubu ilayka”, “Umetakasika Ewe Mola wangu, na Himidi ni zako, Nakiri kuwa hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa wewe tu. Nakuomba maghfira (msamaha) na natubu kwako”. Atasamehewa yaliyotokea katika kikao chake hicho”.** Imepokewa na Tirmidhi kwa nambari (3433), na Shekh Albani amesema kuwa ni Hadithi sahihi. Swahiihuljaamiu (2/1065).



## Tatu: Sunnah Za Mavazi Na Mapambo



### 1 NI KATIKA SUNA KUANZA MGUU WA KULIA KATIKA KUVAA VIATU.



Ni katika Suna Muislamu anapotaka kuvaa viatu vyake aanze na mguu wa kulia, na anapotaka kuvivua aanze na mguu wa kushoto.

Na hoja ya hili ni Hadithi ya Abuhuraira –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema kwamba: **"Mmoja wenu anapovaa viatu aanze kulia, na anapovua aanze kushoto. Mguu wa kulia uwe wa mwanzo kuvalishwa kiatu na uwe wa mwisho kuvuliwa".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (5856).

Na katika matamshi mengine ya Muslim kuna nukuu kwamba: **"Asitembee mmoja wenu akiwa kavaa kiatu kimoja. Yatakikana avae vyote au avivue vyote".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2097).

**Katika Hadithi hizi mbili kuna Suna tatu:**

1. Aanze mguu wa kulia wakati wa kuvaa viatu.
2. Aanze mguu wa kushoto wakati wa kuvua viatu.
3. Avae viatu vyote viwili au avue vyote, ili asitembee akiwa kava kiatu kimoja.

## 2 NI KATIKA SUNA KUVAA NGUO NYEUPE.

Linalokusudiwa ni kuvaa nguo ya rangi nyeupe, kwa sababu hiyo ni katika Suna, kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniabbass –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –RAA- amesema kwamba: **"Katika nguo zenu, vaeni nyeupe, kwa sababu hizo ndio nguo zenu bora zaidi, na muwakafini maiti wenu kwa nguo hizo"**. Imepokewa na Ahmad kwa nambari (2219), Abudaudi kwa nambari (3878) na Tirmidhi kwa nambari (994). Shekh Albani amesema kuwa ni Hadithi sahihi. Swahiihulljaamiu (1/267).



Sheikh wetu Ibniuthamini -Allah amrehemu- amesema kuwa **"Na (kauli) hiyo inajumuisha kuvaa nguo zote nyeupe kama vile: kanzu, vikoi, suruali. Zote hizo yatakikana ziwe nyeupe. Hilo ni bora zaidi. Lakini kama mtu atavaa nguo ya rangi nyingine hapana ubaya, kwa sharti kwamba nguo hiyo isiwe katika mavazi maalumu yanayovaliwa na wanawake"**. Angalia: Sharhu Riyaadhusswaalihiin, ya Shekhe wetu (2/1087).

## 3 NI KATIKA SUNA KUTUMIA MANUKATO.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Anas –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume wa Allah –SAW- amesema kwamba: **"Katika dunia yenu nimefanywa kupenda wanawake na manukato, na burudani yangu imewekwa katika kuswali".** Imepokewa na Ahmad kwa nambari (12293), na Nasai kwa nambari (3940). Na amesema Shekhe Albani katika "Swahiih Annasaaiy" kuwa "Ni Hadithi Hassan (inayokubalika)".

Ama matamshi: "**Katika dunia yenu nimefanywa kupenda vitu vitatu"** ni dhaifu.



Na Mtume - SAW- alikuwa anachukia kunuka harufu mbaya. Katika Hadithi ndefu iliyopokewa na Bukhari akimnukuu Bibi Aisha-RAA- kwamba, amesema kuwa: **"Na ilikuwa ni jambo kubwa kwa Mtume wa Allah -SAW- kuwa ananuka harufu mbaya"**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6972).

**NI MAKURUHU KUKATAA MANUKATO.**

Kwa mujibu wa Hadithi ya Anas -RAA- aliyenukuliwa kusema kwamb, "Mtume –SAW- alikuwa hakatai manukato". Imepokewa na Bukhari kwa nambari (2582).

## 4 NI KATIKA SUNA KUANZA NA UPANDE WA KULIA WAKATI WA KUCHANA NYWELE.



Ni katika Suna kuanza na upande wa kulia kisha upande wa kushoto katika kuchana nywele.

**Na hoja ya hili ni:**

Hadithi ya Aisha-RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, **"Mtume wa Allah –SAW- alikuwa akipenda kuanza upande wa kulia katikaa kuvaa kwake viatu, kutembea kwake, kujitwaharisha kwake na katika kila mambo yake yote".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (168) na Muslim (268).

## Nne: Sunnah Za Kupiga Chafya Na Kupiga Miayo



### SUNA ZA KUPIGA CHAFYA:

1 Ni Suna kwa mwenye kupiga chafya aseme: “Alhamdulillaah”.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira –RAA- akimnukuu Mtume –SAW- kwamba amesema kuwa: **“Anapopiga chafya mmoja wenu aseme: Alhamdulillah, (Himdi Anastahiki Allah). Kisha ndugu yake au mwenzake amwambie: Yarhamukallaah (Allah akurehemu). Na yeye amwambie: Yahdiykumullaahu Wayuswlihu baalakum.** “**Allah akuhidi na akutengenezee mambo yako”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6224).

Na ni Suna kwake kutamka sampuli tofauti tofauti za dua hii. Mara nyingine anaweza kuseme: **“Alhamdulillaahi Alaa Kulli Haal” (Himdi anastahiki Allah kwa kila hali)**. Katika mapokezi ya Abudaudi imekuja nukuu kwamba: **“Anapopiga chafya mmoja wenu aseme: “Alhamdulillaahi Alaa Kulli Haal”.** Ameipokea Abudaudi kwa nambari (5031). Na Ibnulqayyim -Allah amrehemu- amesema katika kitabu chake cha Zaadulmaad (2/436) juu ya Hadithi hii kwamba: “Isnadi yake (orodha ya wapokeaji wake) ni sahihi”.

Na mwenye kumuombea mwenye kupiga chafya amwambie mwenye kupiga chafya: **"Yarhamukallaah" "Allah akurehemu"**. Na ni Suna kwa mwenye kupiga chafya amrejeshee mwenye kumuombea kwa kusema: **"Yahdiikumullaahu Wayuslihu baalakum"** "**Allah akuhidi na akutengenezee mambo yako"**. Yote haya yamepatikana katika Hadithi ya Abuhuraira - RAA- iliyotangulia.

## 2 SUNA NI KUWA KAMA MWENYE KUPIGA CHAFYA HAJAMHIMIDI ALLAH, HAOMBEWI "YARAHAMUKA LLAAH".

Kama mwenye kupiga chafya hajamhimidi Allah – sio katika Suna sisi kumuombea "Yarhamukallaah", lakini Suna ni kutomuombea, kwa mujibu wa Hadithi ya Anas –RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa: **"Walipiga chafya watu wawili mbele ya Mtume –SAW-. Mmoja wao akahimidi Allah, na mwengine hakumhimidi Allah. Mtume alimuombea dua mmoja wao na mwengine hakumuombea. Akasema (yule ambaye hakuombewa dua) kwamba: Ewe Mtume wa Allah, umemuombea huyu na mimi hukuniombea. Mtume akasema: "Hakika, huyu amemhimidi Allah na wewe hukumhimidi Allah"**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6225). Na hii ni katika kitendo cha Mtume - SAW-. Na katika kauli ya Mtume-SAW- imekuja Hadithi iliyopokewa na Muslim ikiwa ni nukuu kutoka kwa Abumusa aliyesema kuwa, Mtume –SAW- amesema kwamba: **"Mmoja wenu atakapopiga chafya kisha akamhimidi Allah muombeeni dua (yaani mwambieni Yarhamukallaah). Na kama hakumhimidi Allah msimuombee dua (yaani msimwambie Yarhamukallaah)".** Ameipokea Muslim namba (2992).

Lakini inapokuwa mazingira ni ya kufundisha, kama vile baba kumlea mtoto wake, au mwalimu kuwafundisha wanafunzi wake, au mfano wa hivyo, hapo anaweza kumwambia: **Sema "Alhamdulillah"** ili amlee katika kuijua na kuitekeleza Suna hii, kwa sababu inawezekana akawa Suna hii haijui.

Pia yule aliye na ugonjwa wa mafua, haombewi dua ya **"Yarhamukallaah"** baada ya kupiga chafya mara ya tatu. Akipiga chafya mara ya tatu ataombewa dua ya **"Yarhamukallaah",** na baada ya hapo hataombewa.

Na hoja ya hili ni: Ile Hadithi aliyoipokea Abudaudi katika kitabu chake cha Sunan ikiwa ni nukuu kwa Abuhuraira RAA- ikiwa Mawquuf (Iliyohusishwa na Swahaba tu) na Marfuu (iliyohusishwa na Mtume s.a.w.) kwamba: **"Muombee ndugu yako aliyepiga chafya dua ya "Yarhamukallaah" mara tatu. Na ikizidi mara tatu huo ni ugonjwa wa mafua"**. Imepokewa na Abudaudi kwa nambari (5034). Shekh Albani -Allah amrehemu- amesema kuwa Hadithi hii

ni "Hasan (inakubalika) ikiwa Mauquuf (imehusishwa na Swahaba tu)" na ni "Hasan (inakubalika) ikiwa Marfuu (imehusishwa na Mtume)". (Swahiih Abudaudi 4/308).

Na Hadithi hii inapewa nguvu na Hadithi iliyopokewa na Muslim katika kitabu chake cha Swahiih Muslim, ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Salama bin Ak-wai -RAA- kwamba, wakati kuna mtu alipiga chafya mbele ya Mtume, alimsikia Mtume –SAW- akimwambia: **"Yarhamukallaah".** Kisha yule mtu akapiga chafya mara nyingine, Mtume –SAW akamwambia: **"Mtu huyu ana mafua".** Ameipokea Muslim kwa nambari (2993).

**Imebainika katika maelezo yaliyotangulia kuwa mwenye kupiga chafya haombewi dua ya "Yarhamukallaah" katika hali mbili:**

1. Kama mpiga chafya hakusema "Alhamdulillaah"
2. Anapozidisha kupiga chafya mara tatu, kwa sababu atakuwa na Mafua.

## SUNA ZA KUPIGA MIAYO.

### NI KATIKA SUNA KUZUIA MIAYO AU KUFUNIKA MDOMO KWA MKONO.

Na hoja ya hilo ni:

Hadithi ya Abuhuraira- RAA- akimnukuu Mtume –SAW- kwamba, amesema kuwa: **"Hakika, Allah anapenda chafya na anachukia miayo. Mtu akipiga chafya akamhimidi Allah, ni haki kwa kila Muisilamu aliyesikia amuombee dua ya "Yarhamukallaah". Ama miayo, hakika hiyo inatokana na shetani, na kwa sababu hiyo, mtu aizuie kadiri awezavyo. Kama mtu atasema: "haaa", Shetani humcheka".** Ameipokea Bukhari kwa nambari (2663).

Na kwa mapokezi ya Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abusaid – RAA - imenukuliwa kwamba, Mtume-SAW- amesema kuwa: **"Mmoja wenu anapopiga miayo, aweke mkono wake kwenye mdomo wake, kwa sababu Shetani huingia".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2995). Kuzuia kupiga miayo kunakuwa kwa kuudhibiti ama kwa kufunga mdomo ili kuzuia usifunuke, au kwa kubananisha meno, au kwa kuweka mkono mdomoni, na mfano wa hivyo.

Na pia iliyo bora kwa mwenye kupiga miayo asitoe sauti yake kwa kupiga miayo, kama kusema (haa), au (aaaah) na mfano wa sauti kama hizo, kwa sababu kufanya hivyo kunapelekea mtu kuchekwa na Shetani.

**Na hoja ya hilo ni:**

Hadithi ya Abuhuraira -RAA- akimnukulu Mtume –SAW- kwamba, amesema kuwa: **"Kupiga miayo kunatokana na shetani. Mmoja wenu anapopiga miayo, ajizuie kadiri awezavyo, kwa sabab anaposema: "Aaah" shetani humcheka".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (3298) na Muslim kwa nambari (2994).

**Angalizo:** Baadhi ya watu wamezoea kusema "Auudhu Billaahi Minash-haytwaanirrajiim"= "Naomba hifadhi kwa Allah dhidi ya shetani aliyetengwa" baada ya kupiga miayo. Hakuna hoja juu ya hilo, bali ni kufanya tofauti ya mwongozo wa Mtume-SAW-, kwa sababu mwenye kufanya hivyo atakuwa ameleta uradi ambao hakuufundisha Mtume -SAW- katika pahala hapa.



## SUNA NYINGINE ZA KILA SIKU



### KUSOMA URADI ULIONUKULIWA WAKATI WA KUINGIA NA KUTOKA CHOONI.



Ni Suna kwa mwenye kuingia chooni, aseme zile nyiradi zilizonukuliwa kwa Mtume na ambazo zipo katika Swahiih Bukhaarii na Swahiih Muslim::

Imenukuliwa kwa Anas –RAA- kwamba, "Mtume wa Allah -SAW- anapoingia chooni alikuwa anasema: **"Allaahuma Innii Auudhubika Minalkhubuthi Walkhabaa-ith** au **Minalkhub-thi**" **(Ewe Allah, Hakika mimi ninakuomba kinga dhidi ya majini wa kiume na majini wa kike** au unikinge dhidi ya uovu**)**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6322) na Muslim kwa nambari (375).

Maombi ya kinga ni dhidi ya mashetani wa kiume na wa kike.

Na (**Uovu**) ni nafsi zenye shari. Kwa hiyo, maombi ya kinga ni dhidi ya shari na wenye shari. Na nukuu hii ina maana pana zaidi.

### Ni Suna kwa anayetoka chooni aseme:

Uradi uliopokewa katika Hadithi iliopo katika kitabu cha Musnad Ahmad, Sunan Abiidaauud na Tirmidhiy, na Shekh Albani amesema kuwa ni sahihi. Imenukuliwa kwa Aisha–RAA- kwamba, amesema kuwa: **"Mtume –SAW- anapotoka chooni alikuwa anasema "Ghufraanaka"** (Naomba msamaha wako (Ewe Allah)" Imepokewa na Ahmad kwa nambari (25220), Abudaud kwa nambari (30) na Tirmidhi kwa nambari (7). Shekhe Albani na amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Tahqiiqu Mishkaatilmaswaabiih 1/116).

## NI SUNA KUANDIKA WASIA.



Kuandika wasia ni Suna kwa kila Muislamu akiwa mgonjwa au mzima, kwa mujibu wa kauli ya Mtume -SAW-kwamb: "Si haki kwa mtu Muislamu ambaye ana jambo analotaka kulitolea usia, alale siku mbili bila ya wasia wake kuwa anao (na) umeandikwa". Ameipokea Bukhari kwa nambari (2783) na Muslim kwa nambari (1626) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Ibniumar-RAA-. Na kutajwa siku mbili katika Hadithi sio kwamba imefungika. Kinachokusudiwa ni kuwa, usimpitikie mtu muda mfupi isipokuwa wasia wake awe nao umeandikwa, kwa sababu hajui atakufa lini. Suna hii ni ya watu wote.

Ama wasia katika mambo ambayo ni haki ya Allah -SWT- kama Zaka, Hija, au Kafara au haki za binadamu, kama deni, kutekeleza amana za watu, ni wajibu na sio Suna, kwa sababu unafungamana na utekelezaji wa haki ambazo ni wajibu, hasa kama hakuna yeyote anayejua haki hizi **[ Na jambo ambalo wajibu hautimii ila kwalo, nalo ni wajibu ].**

## KUSAMEHE NA UPOLE KATIKA BIASHARA.

Hilo linapatikana kwa kila mmoja kati ya muuzaji na mnunuzi kuwa na sifa ya kusamehe na upole wakati wa kuuza au kununua. Mmoja wao amsifanyie ugumu mwenzake katika kupatana bei na kuwa mbishi katika hilo. Lakini wanatakiwa wanasameheane.



**Na hoja ya hili ni:**

Hadithi ya Jabir bin Abdallah-RAA- kwamba, Mtume wa Allah –SAW-amesema kuwa: **“Allah amrehemu mtu msamehevu anapouza, na anaponunua, na anapodai”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (2076).

Pia mtu anapodai kulipwa haki yake, ni katika Suna adai kwa wepesi na upole, kwa mujibu wa kauli ya Mtume –SAW-:“**Na anapodai**”.

## KUSWALI RAKAA MBILI BAADA YA KILA UDHU.



Hii ni katika Suna za kila siku ambazo zina ambatana na fadhila kubwa, ambayo ni kuingia Peponi. Imepokewa kwa Abuhuraira –RAA- kwamba: “Mtume–SAW-alimwambia Bilali wakati wa swali ya Alfajiri kwamba: **“Ewe Bilali, niambie amali unayotarajia sana malipo yake ambayo umeifanya katika Uislamu, kwa sababu mimi nimesikia mlio wa viatu vyako mbele yangu peponi”. Bilali akasema: “Sikufanya amali ambayo nina matarajio nayo isipokuwa kwamba sikujitwaharisha tohara yoyote usiku au mchana ila niliswali kwa tohara hiyo nilichojaliwa kuswali”.** Ameipokea Bukhari kwa nambari (1149) na Muslim kwa nambari (2458).

## KUSUBIRI SWALA.



Kusubiri swala ni katika Suna ambazo zina fadhila kubwa.

Na hoja ya hilo ni:

Hadithi ya Abuhuraira -RAA- kwamba, Mtume (SAW) amesema kuwa: **“Mmoja wenu ataendelea kuwa katika swala madamu swala inamfunga (kwa maana kwamba) hakuna kilichomzuia kwenda kwa familia yake isipokuwa swala tu”.** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (659), na Muslim kwa nambari (649). Mtu kwa kungoja kwake (kuswali) anapata ujira wa swala.

Na imepokewa kwa Abuhuraira –RAA- kwamba, Mtume wa Allah amesema kuwa: **"Malaika wanamuombea rehema mmoja wenu madamu yungali katika sehemu yake ya kuswalia, na madamu hajauvunja udhu wake. (Malaika wanaomba) Ewe Allah, msamehe. Ewe Allah, mrehemu. Mmoja wenu ataendelea kuwa katika swala madamu swala imemfunga, (kwa maana kwamba) hakuna kilichomuzuii kwenda kwa familia yake ila swala tu**". Imepokewa na Bukhari kwa nambari (659), na Muslim kwa nambari (649). Na kauli ya Mtume kwamba: **"Madamu hajavunja udhu wake"** ina maana madamu hajafanya jambo lenye kutengua udhu. Na imekuja nukuu kwa mapokezi ya Muslim kwamba:

**"Madamu hajaudhi ndani yake, madamu haja pata la kutengua Udhu ndani yake"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (649). Maana ni kwamba, thawabu hizi katika kuzipata zimewekewa sharti kuwa, asimuudhi mtu yeyote hapo alipokaa na Udhu wake usitenguke.

## KUPIGA MSWAKI



Kupiga mswaki ni katika Suna ambazo hazifungamani na wakati; na ambazo hufanywa wakati wowote. Mtume –SAW - alikuwa akisisitiza sana kupiga mswaki mpaka akasema: **"Nimekithirisha sana kukuambieni kuhusu mswaki".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (8888) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Anas –RAA-. Pia Mtume –SAW- amesema kuwa: **"Mswaki ni kisafisha mdomo na ni kiridhisha Mola"**. Ameipokea Ahmad kwa nambari (7) na Nasai kwa nambari (5) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Aisha- RAA-, na Shekhe Albani amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Al-irwaa 1/105).

Na Suna ya kupiga mswaki inasisitizwa zaidi katika sehemu ambazo baadhi yake zimetangulia kutajwa, hasa zile ambazo zinajirudiarudia katika siku, kama kisimamo cha usiku, wakati wa kutawadha, wakati wa kila swala na wakati wa kuingia nyumbani. Allah ndiye Mjuzi zaidi.

## KURUDIA KUTAWADHA UPYA KWA KILA SWALA.

Ni Suna kwa Muislamu kurudia upya kutawadha kwa kila swala. Kama mtu alitawadha kwa ajili ya swala ya Magharibi, kwa mfano, kisha akaswali Magharibi. Ikija swala ya Isha, ni Suna kwake kutawadha hata kama Udhu



anao. Suna ni mtu kutawadha udhu mpya kwa kila swala.

Na hoja ya hilo ni:

Hadithi iliopo kwa Bukhari aliyenukuu na kusema kwamba: **"Mtume-SAW- alikuwa anatawadha wakati wa kila swala".** Imepokewa na Bukhari (214).

Pia ni katika Suna mtu kuwa na twahara siku yake yote, kwa mujibu wa Hadithi ya Thauban -RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, Mtume –SAW- amesema kwamba: **"Na hadumu kuwa na Udhu ila mtu mumini tu"**. Imepokewa na Ahmad kwa nambari (22434), Ibnimaja kwa nambari (277), Daarimi kwa nambari (655), na Shekhe Albani amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Swahiihuljaamiu 1/225).

## DUA.

**Ufafanuzi wa mambo ambayo ni Suna Muislamu kuyafanya anapotaka kuomba Dua. Ni katika Suna:**

### 1 AOMBE DUA AKIWA NA TWAHARA.

Kwa mujibu wa Hadithi ya Abumusa -RAA- iliopo katika Swahiih Bukhaariy na Swahiih Muslim, na kisa chake yeye na ami yake Abuamir -RAA- pale Mtume -SAW- alipomtuma kwenda kupambana na jeshi la Autwaas. Katika Hadithi hiyo kuna nukuu kwamba: **"Abuamir-RAA- aliuawa na (kabla ya kuuawa) alimuusia Abumusa –RAA- amsalamie Mtume -SAW- na kumuomba amuombee Dua. Abumusa -RAA- akasema: Nikamhabarisha Mtume habari yetu na habari ya Abuamir, na kumwambia: Amesema Abuamir: Mwambie Mtume aniombee maghfirah. Mtume –SAW- akaagiza aletewe maji. Alitawadha, kisha akainua mikono yake, kisha akasema: "Ewe Mola wangu, mghufirie Abeid Abuamir" mpka nikaona weupe wa kwapa zake. Kisha Mtume akasema: "Ewe Mola wangu, mjaalie Siku ya Kiama awe juu ya viumbe wako wengi, au juu ya watu wengi".** Ameipokea Bukhari kwa nambari (4323) na Muslim kwa nambari (2498).

### 2 KUELEKEA KIBLA.

Imenukuliwa kwa Abdallah bin Abbas –RAA- akisema kuwa: **"Amenisimulia Umar bin Khatwab -RAA- na kusema: Ilipokuwa siku ya (vita vya) Badri, Mtume –SAW-aliwaangalia Makafiri wakiwa elfu moja, na Swahaba zake**

**wakiwa watu mia tatu na kumi na tisa. Mtume wa Allah akaelekea Kibla, kisha akanyanyua mikono yake akaanza kumuomba Mola wake: Ewe Mola wangu, nitimizie uliyoniahidi. Ewe Mola wangu, nipe kile ulichoniahidi. Ewe Mola wangu, kikiangamia hiki kikundi cha Waislamu wachache hutoabudiwa katika ardhi. Mtume aliendelea kumuomba Mola wake huku akiwa amenyanyua mikono yake na kuelekea Kibla, hadi Kashida yake iliyokuwa mabegani ikamdondoka. Abubakar akamfuata Mtume, akaokota Kashida kisha akaitupia katika mabega ya Mtume. Kisha Abubakar akasimama nyuma ya Mtume na kumwambia: "Ewe Mtume wa Allah, yatosha ulivyomuomba Mola wako. Hakika, atakutimizia alichokuahidi".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (1763).

### 3 KUINUA MIKONO.

Na hoja ya hili ni Hadithi ya Ibniabbas –RAA- iliyopita. Na katika Hadithi hiyo kuna nukuu kwamba: **"Mtume wa Allah akaelekea Kibla, kisha akanyanyua mikono yake"**. Hadithi zinazohusu Suna hii ni nyingi.



### 4 KUANZA KWA KUMSIFU ALLAH –SWT- NA KUMSWALIA MTUME -SAW-.

Kwa mujibu wa Hadithi aliyoipokea Tirmidhi akimnukuu Fudhala bin Abeid- RAA- aliyesema kuwa, wakati Mtume –SAW- akiwa ameketi, aliingia mtu mmoja na kuswali kisha akasema: "**Ewe Mola wangu, nisamehe na nirehemu" Mtume-SAW- akasema: "Umefanya haraka ewe mwenye kuswali. Unaposwali na kuketi, mhimidi Allah kwa sifa zake anazostahiki, kisha niswalie, kisha muombe Allah**". Imepokewa na Tirmidhi kwa nambari (3476), na Shekhe Albani amesema kuwa ni Hadithi sahihi. (Swahiihuljaamiu 1/172).

### 5 KUMUOMBA ALLAH KWA MAJINA YAKE MAZURI.

Mtu achague katika majina ya Allah yale majina yaliyo mazuri kulingana na maudhui ya dua yake. Akimuomba Allah riziki aseme: **"Yaa Razzaaq" (Ewe Mwenye kuruzuku).** Akimuomba Allah –SWT- rehema aseme: "**Yaa Rahmaan, Yaa Rahiim" (Ewe Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu).** Akimuomba Allah nguvu na utukufu aseme: **"Ya Aziiz" (Ewe Mwenye ezi).** Akimuomba Allah maghfira aseme: **"Yaa Ghafuur" (Ewe Mwingi wa**

**kusamehe). A**kimuomba Allah kupona ugonjwa aseme: **"Yaa Shaafii" (Ewe Mwenye kuponya).**

Aombe kwa kutumia majina (ya Allah) yanayonasibiana na maombi yake, kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa: **{Na Allah ana majina mazuri kabisa, hivyo muombeni kwayo}**. (Sura Al-aaraaf: 180).

### 6 KURUDIA DUA NA KUOMBA KWA MSISITIZO.

Na hoja ya hili ni Hadithi ya Ibniabass –RAA-ambayo imetangulia kutajwa ambapo Mtume -SAW- amenukuliwa kusema kuwa: **"Ewe Mola wangu, nitimizie uliyoniahidi. Ewe Mola wangu, nipe uliyoniahidi"**. Mtume hakuacha kumuomba Mola wake mpaka Kashida yake ikamuanguka, na Abubakar akiwa nyuma yake akimwambia: "Ewe Mtume wa Allah, yanatosha ulivyomuomba Mola wako". Imepokewa na Muslim kwa nambari (1763).

Na vilevile kuna Hadithi katika Swahiih Bukhaari na Swahiih Muslim ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira -RAA- kwamba, Mtume -SAW- alipowaombea (kabila la) Daus, alisema: **"Ewe Mola wangu, waongoze Daus na walete. Ewe Mola wangu, waongoze Daus na walete".** Imepokewa na Bukhari kwa nambari (2937), na Muslim kwa nambari (2524).

Na vilevile kuna Hadithi katika Swahiih Muslim kuhusu: **"Mtu anayesafiri safari ndefu, akiwa kachafuka, kajaa mavumbi na huku anayanyua mikono yake mbinguni akiomba: "Ewe Mola wangu! Ewe Mola wangu**". Ameipokea Imamu Muslim kwa nambari (1015). Huku ni kurudia ambako ndani yake kuna msisitizo.

Na Suna ni kuomba mara tatu, kwa mujibu wa Hadithi ya Ibnimasoud -RAA- iliopo katika Swahiih Bukhaari na Swahiih Muslim). Ndani ya Hadithi hiyo kuna nukuu kwamba, "Anapo omba alikuwa anaomba mara tatu, kisha anasema: **"Ewe Mola wangu, wakamate (wadhibiti) Wakuraishi**" mara tatu". Imepokewa na Bukhari kwa nambari (240) na Muslim kwa nambari (1794).

### 7 KUOMBA DUA KWA SIRI.

Kwa mujibu wa kauli ya Allah –SWT- isemayo kuwa: {**Muombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri**....}. (Sura Al-aaraf: 55). Kuomba dua kwa siri kuna uhalisia zaidi wa kumkusudia Allah (Ikhlasi). Kwa sababu hiyo, Allah amemsifu Zakaria -AS- na kusema: {**Alipomuomba Mola wake maombi ya siri**} [Sura Maryam: 3] akitafuta ikhlasi kwa mujibu wa moja ya kauli za wanazuoni wa Tafsiri ya Kurani.

**Faida**: Baadhi ya watu wanaweza kuuliza: Niseme nini katika Dua yangu?



**Jawabu ni kwamba:** Omba unachotaka, katika mambo ya dunia na ya akhera. Na katika dua yako jitahidi kutumia maneno yanayojumuisha maana nyingi. Hizi ni dua ambazo zimo katika Kurani na Suna. Ndani ya Dua hizo kuna kuomba mema ya duniani na akhera. Hebu tafakari hili swali aliloulizwa Mtume –SAW- naye akalijibu kwa kutumia maneno makubwa, yenye kumkusanyia Mwislamu dunia na akhera. Ni bishara kubwa sana, na ni tunu iliyosheheni. Tumia Dua hizo na zitie akilini.

Imenukuliwa kwa Abumalik Al-ashjai naye akimnukuu baba yake –RAA- kwamba **"Alimsikia Mtume –SAW- akiwa amefuatwa na mtu aliyeuliza hivi: Ewe Mtume wa Allah, Vipi niseme pindi ninapomuomba Mola wangu? Mtume akasema: "Sema: Ewe Allah, nighufurie na nirehemu na nipe uzima na niruzuku, na (Mtume alikuwa) anakusanya vidole vyake pomoja ila dole gumba. (Mtume aliendelea kusema): Hakika, maneno haya yanakukusanyia dunia yako na akhera yako".** Imepokelewa na Muslim kwa nambari (2697).

Na katika mapokezi mengine ya Imam Muslim kuna nukuu kwamba: "Mtu alipokuwa anaingia katika dini ya Kiislamu, Mtume –SAW- alikuwa anamfundisha Swala, kisha anamuamrisha kuomba dua kwa kutumia maneno haya: **"Ewe Allah, nighufurie na nirehemu na niongoze na nipe uzima na niruzuku".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2697).

**Faida nyingine:** Ni Suna kwa mwanadamu kumuombea dua ndugu yake ambaye hayupo naye. Hii ni dua yenye kujibiwa, kwa uwezo wa Allah-SWT-. Mwenye kuombea naye anapata fadhila kubwa ambazo zimeelezwa katika Hadithi aliyoipokea Imamu Muslim katika kitabu chake cha Swahiih Muslim akimnukuu Abudardai - RAA- kwamba, Mtume -SAW- amesema kuwa: **"Maombi ya Muislamu kwa nduguye akiwa hayupo naye ni yenye kujibiwa. Kwenye kichwa chake kuna Malaika aliyepewa kazi maalumu. Kila Muislamu atakapomuombea kheri ndugu yake, Malaika yule anasema: Aamin, nawe upate kama hayo (uliyomuombea nduguyo)".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2733).

### NA KATIKA SUNA ZA KILA SIKU NI KUMTAJA ALLAH-SWT-

Na uradi mkubwa sana ni: Kusoma kitabu cha Allah-SWT-. Kufanya ibada ya kusoma kitabu cha Allah kulifanya Wema Waliotangulia wakeshe na kuacha wazi vitanda vyao. {**Walikuwa wakilala kidogo tu katika usiku, na (muda wa) kabla ya Alfajiri ni wenye kuomba maghufira**}. (Sura Adh-dhaariyaat 18). Wamekusanya katika usiku wao kusoma kitabu cha Allah aliyetukuka na nyiradi nyingine zilizopokewa kwa Mtume –SAW. Ni uzuri ulioje wa usiku ambao umekuwa mzuri kwa watu wake kuufanya kuwa hai (kwa kufanya ibada), na ni hasara ilioje kwetu kwa kufanyia uzembe muda wetu wa usiku na pia muda wetu wa kabla ya alfajiri, kama (muda wetu huo wa usiku na wa kabla ya alfajiri) haujasalimika na maasi tunayomfanyia Mola wetu, isipokuwa tu wachache wetu waliopata rehema za Allah.

Imenukuliwa kwa Hamadi bin Zaid naye akinukuu kwa Atwaa bin Saib kwamba, Abuabdulrahman amesema kuwa: **“Tumejifunza Kur’ani kwa watu ambao wametuambia kuwa walikuwa wakisoma aya kumi, hawazipiti na kuziendea aya kumi nyingine mpaka wajue yaliyomo ndani ya aya hizo. Tulikuwa tunajifunza Kur’ani na kuifanyia kazi. Na watarithi Kur’ani baada yetu watu watakaokuwa wakiinywa mithili ya unywaji wa maji, haivuki koo zao”.** Angalia: Siyar Aalaamunnubalaa (4/269).



Ni Kubwa Liliyoje Hitajio Lako La Kukaa Faragha Na Nafsi Yako Ukaihesabu, Na Ukamdhukuru Mola Wako Hasa Hasa Katika Zama Zilizokithiri Mishughuliko Na Kughafilika Ndani Yake

## URADI UNA UHAI WA NYOYO.



Wetu wengi hasa katika zama hizi, na mihangaiko mingi wanalalamika nyoyo zao kupata kutu na kughafilika. Uhai wa moyo unapatikana kwa kumtaja Allah -SWT-. Katika Swahiih Bukhaari, ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abumusa-RAA- aliyenukuliwa kusema kwamba, Mtume wa Allah –SAW- amesema kuwa: "**Mfano wa anayemtaja Mola wake na asiyemtaja Mola wake ni mfano wa aliye hai na maiti**". Na katika matamshi ya Imamu Muslim imenukuliwa kwamba, Mtume-SAW- amesema: **"Mfano wa nyumba ambayo Allah anatajwa humo na nyumba ambayo Allah hatajwi humo ni mfano wa aliye hai na maiti"**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6407), na Muslim kwa nambari (779).

## ALLAH AMEHIMIZA KUTAJWA KATIKA MAENEO MENGI. MIONGONI MWA MAENEO HAYO NI:

1. Allah amewahimiza waja wake wamtaje sana. Amesema : {**Enyi mlioamini, mtajeni sana Allah, na mtakaseni asubuhi na jioni.** (Sura Al-ahzaab 41: 42)**.**

2. Allah Mtukufu amewaahidi wenye kumtaja, wake kwa waume, kwamba atawapa msamaha, thawabu na malipo makubwa. Amesema: {**Na wanaume wanaomtaja Allaah kwa wingi na wanawake, Allah amewaandalia maghufira na malipo makubwa**}. (Sura Al-ahzaab: 35).

3. Na Allah -SWT- ametuhadharisha sifa za wanafiki. Wao wanamtaja Allah -SWT-, lakini hebu tafakari kiwango chao cha kumtajaji. Amesema Allah -SWT- kuwa: {**Hakika, wanafiki (wanadhani) wanamhadaa Allah, na hali yeye (Allah) ndiye Mwenye kuwahadaa. Na wanaposimama kuswali husimama kwa uvivu, wakijionesha kwa watu na wala hawamtaji Allah isipokuwa kidogo tu**}. (Annisaa: 142).

4. Allah –SWT- ametuhadharisha juu ya kushugulishwa na mali na watoto tukapuuza kumdhukuru. Amesema Allah aliyetukuka kuwa: {**Enyi mlioamini, zisikupuuzisheni mali zenu na watoto wenu mkaacha kumdhukuru Allah. Na yeyote atakayefanya hivyo basi hao tu ndio waliohasirika**} (Sura Almunaafiquun: 9).

5. Hebu tafakari pamoja nami huu ujira mkubwa na utukufu wa hali ya juu kabisa! Amesema Allah -SWT- kuwa: {**Basi nitajeni na Mimi nitakukumbukeni**}. Na Allah amesema katika Hadithi Kudusi kwamba: **"Mimi niko vile mja wangu anavyonidhania. Niko pamoja naye anaponitaja. Anaponitaja katika nafsi yake, name namtaja katika nafsi yangu. Anaponitaja katika hadhara, nami namtaja katika hadhara bora zaidi kuliko hadhara yao"**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (7405), na Muslim kwa nambari (2675) ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira.

Na aina za nyiradi za kumtaja Allah zilizopokewa katika Suna ya Mtume -SAW- ni nyingi. Miongoni mwa niyiradi hizo ni hizi zifuatazo:

1. Imenukuliwa kwa Abuhuraira -RAA- kwamba, Mtume –SAW- amesema kuwa: **"Mwenye kusema: "Laa ilaaha illallaah Wahdahuu Laashariika Lah, Lahulmulku, Walahulhamdu, Wahuwa Alaa Kulli Shay-in Qadiir. (Hakuna Muabudiwa kwa haki ila Allah peke yake, hana mshirika. Ni wake yeye tu ufalme na ni zake yeye tu Sifa njema, na yeye ni Muweza wa kila kitu) mara mia moja kwa siku, atakuwa na ujira wa sawa na kuacha huru watumwa kumi, na ataandikiwa mema mia moja, na atafutiwa madhambi mia moja, na atakuwa na kinga dhidi ya shetani kwa siku yake hiyo, mpaka afikiwe na jioni. Na hatakuja mtu yeyote Siku ya Kiyama na kilicho bora zaidi ya alichokuja nacho yeye, isipokuwa tu yule aliyesema mfano wa hayo aliyosema au akazidisha juu ya hayo. Na mwenye kusema: Sub-haanallaah wabihamdihii (Ametakasika Allah na sifa zote njema ni zake) mara mia moja kwa siku, atasamehewa dhambi zake hata kama ziko (nyingi) kama povu la bahari**". Imepokewa na Bukhari kwa nambari (3293), na Muslim kwa nambari (2691).

2. Na imenukuliwa kwa Abuayoub -RAA- akisema kuwa, amesema, Mtume –SAW- kwamba: **"Mwenye kusema: "Laa ilaaha ilallaah Wahdahuu Laashariika Lah, Lahulmulku, Walahulamdu, Wahuwa Alaa Kulli Shay-in Qadiiru (Hakuna Muabudiwa kwa haki ila Allah peke yake, hana mshirika. Ni wake yeye tu ufalme na ni zake yeye tu Sifa njema, na yeye ni Muweza wa kila kitu) mara kumi, atakuwa kama aliyeacha huru watumwa wanne katika watoto wa Ismaili**". Imepokewa na Bukhaari kwa nambari (6404) na Muslim kwa nambari (2693).

3. Na imenukuliwa kwa Saad bin Abiwakas –RAA- akisema kuwa: **"Tulikuwa mbele ya Mtume-SAW- akasema: Hivi anashindwa mmoja wenu kuchuma kila siku mema elfu moja? Muulizaji katika wale waliokuwa wameketi katika kikao kile akamuuliza Mtume: Atapataje mmoja wetu hayo mema elfu moja? Mtume akasema: Asabihi Tasibihi mia moja (yaani aseme Sub-haanallaah mara mia moja). Akifanya hivyo, ataandikiwa mema elfu moja au atafutiwa madhambi elfu moja"**. Imepokewa na Muslim kwa nambari (2698).

4. Imenukuliwa kwa Abuhuraira -RAA- kwamba, Mtume-SAW- amesema kuwa: **"Mwenye kusema Sub-haanallaah wabihamdihii (Ametakasika Allah na sifa zote njema ni zake) mara mia moja kwa siku, ataghufuriwa makosa yake japokuwa ni (mengi) mfano wa povu la bahari.**" Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6405), na Muslim kwa nambari (2692). Na katika mapokezi ya Muslim kuna nukuu kwamba: **"Mwenye kusema Sub-haanallaah wabihamdihii (Ametakasika Allah na sifa zote njema ni zake) mara mia moja asubuhi na jioni, hatakuja mtu yeyote Siku ya Kiyama na kilicho bora zaidi ya alichokuja nacho yeye isipokuwa yule aliyesema mfano wa hayo aliyosema au akazidisha juu ya hayo".** Imepokewa na Muslim kwa nambari (2692).

Na Hadithi katika kuelezea aina za nyiradi na fadhila zake ziko nyingi. Hizo zilizotangulia kutajwa ni katika nyiradi sahihi na mashuhuri zaidi, lakini zipo nyingine nyingi zilizonukuliwa. Imenukuliwa kwa Abumousa Al-ashari -RAA- akisema kuwa, amesema Mtume-SAW-: **"Je nikufahamishe hazina miongoni mwa hazina za peponi?, Nikasema: Naam. Mtume akasema: "Sema: Laa Hawla Walaa Quwwata illaa Billaah", (Hakuna uwezo (wa kufanya mema) wala mbinu (za kuacha maovu) ila kwa msaada wa Allah tu)**. Imepokewa na Bukhari kwa nambari (4202), na Muslim kwa nambari (2704).

Na imenukuliwa kwa Abuhuraira –RAA- akisema kuwa, amesema Mtume -SAW- kwamba: "**Kwa yakini kabisa, kusema kwangu: Sub-haanallaah, Walhamdulillaah, walaa ilaaha illallaah, wallaahu Akbar- Utakasifu ni wa Allah na himdi anazistahiki Allah, na hakuna Muabudiwa wa haki ila Allah tu, na Allah ni Mkubwa; kusema hayo ni bora kwangu kuliko kila kilichoangaziwa na jua**". Imepokewa na Muslim kwa nambari (2695).

Kumuomba msamaha Allah ni aina ya uradi pia. Imepokewa kwa Aghari Almuzani –RAA- akisema kuwa, amesema Mtume –SAW- kwamba: "**Hakika**

**mimi (kama mwanadamu) moyo wangu hushughulishwa (na mambo mbalimbali ya kidunia). Na mimi, kwa hakika, namuomba msamaha Allah kwa siku mara mia moja**". Imepokewa na Muslim kwa nambari (2702).

Huu ni ushahidi wa Mtume-SAW- alivyokuwa yeye mwenyewe akiomba msamaha. Pia amehimiza, kwa maneno yake, kuomba msamaha kama ilivyo katika Swahiih Muslim ikinukuliwa kwa Aghari -RAA- pia kwamba, amesema Mtume –SAW- kuwa: "**Enyi watu, tubuni kwa Allah. Hakika, mimi natubu kwa Allah kwa siku mara mia moja**". Imepokewa na Muslim kwa nambari (2702).

Na katika upokezi wa Bukhaari ikiwa ni sehemu ya Hadithi ya Abuhuraira -RAA- imenukuliwa kuwa amesema: "**Nimemsikia Mtume wa Allah (Rehema na amani ya Allah iwe juu yake) akisema: Nina apa kwa Allah kwamba mimi namuomba msamaha Allah na natubu kwake zaidi ya mara sabini katika siku moja**". Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6307). Inampasa mja kutopuuza kumuomba Allah msamaha.

Na namalizia Suna ya kumtaja Allah - na pia Suna zote za kila siku- kwa kutaja uradi mkubwa uliopokewa katika Swahiih Bukhaarii na Swahiih Muslim. Ni Hadithi ya Abuhuraira- RAA- aliyenukuliwa kusema kuwa, amesema Mtume –SAW- kwamba: "**Maneno mawili ni mepesi juu ya ulimi, ni mazito katika mizani, yanapendwa na (Allah) Mwingi wa rehema. Ni: Sub-haanallaah Wabihamdihii, Sub-haanallahil-adhwiim": "Ametakasika Allah, na sifa njema ni zake. Ametakasika Allah aliye Mtukufu**". Imepokewa na Bukhari kwa nambari (6406), na Muslim kwa nambari (2694).

**SIFA ZOTE NJEMA NI ZA ALLAH AMBAYE KWA NEEMA ZAKE MAMBO MEMA YANATIMIA.**

Kiswahili



Utangulizi 

Suna za kabla ya Alfajiri 

Suna za wakati wa Alfajiri 

Suna za wakati wa Dhuha 

Suna za Adhuhuri na Alasiri 

Suna za wakati wa Magharibi 

Suna za wakati wa Isha 

Suna za chakula 

Suna za salamu, kukutana na kikao 

Suna katika mavazi na mapambo 

Suna za kupiga chafya na kupiga miayo 

Suna nyingine 


# SUNA ZA MTUME (SAW) NA NYIRADI ZAKE ZA KILA SIKU

اللغة السواحلية
KISWAHILI LANGUAGE

جميع لغات المشروع
ALL LANGUAGES